Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.

Budget Documents Budget Guidelines

2021

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022-23

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/394

Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23

NOVEMBA, 2021

YALIYOMO

ORODHA YA VIFUPISHO ..... **iv**
MUHTASARI ..... **vi**
SEHEMU YA KWANZA ..... **ix**
SERA NA MFUMO WA BAJETI YA SERIKALI ..... **ix**
SURA YA KWANZA **1**
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI **1**
1.1 Utangulizi 1
1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda 1
1.3 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei 3
1.4 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania 4
1.5 Deni la Serikali 10
1.6 Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania 11
SURA YA PILI 13
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22 13
2.1 Utangulizi 13
2.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2021/22 13
2.3 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika kipindi cha robo ya Kwanza kwa Mwaka 2021/22 15
2.3.1 Mapato 15
2.2.2 Matumizi 15
2.4 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22 16
SURA YA TATU 20
MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23 20
3.1 Utangulizi 20
3.2 Malengo na Shabaha ya Uchumi Jumla 20
3.3 Misingi ya Uchumi Jumla 20
3.4 Vipaumbele katika Muda wa Kati 20
3.5 Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati 21
3.6 Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati 24
3.7 Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati 24
3.8 Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti 28
3.9 Mfumo wa Bajeti 29
SURA YA NNE **36**
VIHATARISHI VYA UKUAJI WA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO **36**
4.1 Utangulizi 36
4.2 Vihatarishi vya ukuaji wa uchumi 36
4.3 Vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali 36
4.4 Hatua za kukabiliana na vihatarishi 37

SEHEMU YA PILI.....39
MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23 39

MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23.....40
1.1. Utangulizi 40
1.2. Uandaaji wa Mpango na Bajeti 40
1.3. Uzingatiaji wa Masuala ya Muungano.....40
1.4 Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti.....41
1.4.1 Kamati za Bajeti.....41
1.4.2 Maandalizi ya Makadirio na Mgawanyo wa Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 41
1.4.3 Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara 42
1.5 Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti 42
1.6 Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma 51
1.7 Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.....52
1.7.1 Sekretarieti za Mikoa.....52
1.7.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa 53
1.8 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep....58
1.9 Uchambuzi wa Mpango na Bajeti 58
1.10 Uwasilishaji wa Randama 59
1.11 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji 59
1.11.1 Ufuatiliaji na Tathmini 59
1.11.2 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji 60
SURA YA PILI.....61
MUUNDO WA UANDAAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23.....61
1.1 Utangulizi 61
1.2 Maandalizi ya Mpango na Bajeti 61
1.3 Utekelezaji wa Bajeti.....62
1.4 Taarifa za Utekelezaji 63
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI 128
1.1 Utangulizi 128
1.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2020/21.....128
1.2.1 Mapato na Matumizi 128
1.2.2 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti 130
1.2.3 Mafanikio mengine yaliyopatikana 150
1.2.4 Changamoto zilizojitokeza Katika Utekelezaji wa Bajeti.....157
1.2.5 Hatua Zinazochukuliwa Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti.....158

ORODHA YA VIFUPISHO

ASDP	Agriculture Sector Development Programme
ATCL	Air Tanzania Company Limited
BRELA	Business Registration and Licensing Agency
CBMS	Centralized Budget and Management System
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CFR	Council Financial Report
CFS	Consolidated Fund Service
DADPs	District Agricultural Development Plans
DCF	Development Co-operation Framework
DEV	Development
EAC	East African Community
EFD	Electronic Fiscal Device
EFDMS	Electronic Fiscal Device Management System
EPZ	Export Processing Zone
FFARS	Facility Financial Accounting and Rreporting System
FY	Financial Year
FYDP	Five Year Development Plan
GAMIS	Government Asset Management Information System
GAMS	Government Arrears Management System
GePG	Government Electronic Payment Gateway
GFS	Government Finance Statistics
HCMIS	Human Capital Management Information System
iCHF	Community Health Fund
IMF	International Monetary Fund
LGAs	Local Government Authorities
LGRCIS	Local Government Revenue Collection Information System
LNG	Liquefied Natural Gas
M3	Extended Broad Money Supply
MDAs	Ministries, Independent Departments and Agencies
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MTSPBM	Medium Term Strategic Plan and Budget Manual
MUSE	Mfumo wa Ulipaji Serikalini
MW	Megawatts
NACSAP	National Anti - Corruption Strategy and Action Plan
NHIF	National Health Insurance Fund
NPMIS	National Project Management Information System
OC	Other Charges
ORTAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
OTRMIS	Office of Treasury Registrar Management Information System

PE	Personal Emoluments
PIM - OM	Public Investment Management – Operational Manual
PlanRep	Planning and Reporting Database
PPP	Public-Private-Partnership
PSRP	Public Sector Reform Program
PSSSF	Public Service Social Security Fund
RSs	Regional Secretariats
SADC	Southern Africa Development Community
SDG	Sustainable Development Goals
SEZ	Special Economic Zone
SGR	Standard Gauge Railway
SMT	Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
SMZ	Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
TANePS	Tanzania National e-Procurement System
TANESCO	Tanzania Electric Supply Company Limited
TBA	Tanzania Buliding Agency
TBS	Tanzania Bureau of Standards
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEMESA	Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency
TeSWs	Tanzania Electronic Single Window System
TIKA	Tiba Kwa Kadi
TRA	Tanzania Revenue Authority
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UVIKO – 19	Ugonjwa wa Virushi vya Korona
VAT	Value Added Tax
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WAVIU	Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI
WCF	Workers Compensation Fund
ZSSF	Zanzibar Social Security Fund

MUHTASARI

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake za mwaka 2015. Uandaaji wa Mwongozo huu umefanyika kwa kurejea nyaraka za kitaifa ikiwemo Sera na Mipango, Sheria, Miongozo na Waraka mbalimbali za Serikali pamoja na makubaliano ya kikanda na kimataifa yaliyoridhiwa na Tanzania. Baadhi ya nyaraka zilizorejewa ni pamoja na: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa (2021/22 – 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020; Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara; Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/21 -2029/30); Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada, Sura 134; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; Agenda ya Afrika Mashariki 2050; Agenda ya Afrika 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Lengo la Mwongozo huu ni kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu maandalizi ya mpango na bajeti za Mafungu kwa mwaka 2022/23 ili kufikia malengo ya kiuchumi na kijamii yaliyobainishwa katika vipaumbele vya Taifa.

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Sera na Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 ambayo inajumuisha: Mapitio ya mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi nchini, kikanda na dunia kwa mwaka 2020 na robo ya kwanza ya mwaka 2021; mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22; Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23 ambao unaainisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23 na muda wa kati pamoja na sera na mikakati ya kusimamia mapato na matumizi; na uchambuzi wa vihatarishi vya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa mpango na bajeti na mikakati ya kukabiliana navyo. Sehemu ya pili inatoa maelekezo ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli katika uandaaji, uwasilishaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23.

Katika mwaka 2020, uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 5.5 na ukuaji halisi wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Ukuaji wa uchumi ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kilimo (asilimia 26.9) ikifuatiwa na ujenzi (asilimia 14.4), biashara (asilimia 8.7), viwanda (asilimia 8.4) na

uchukuzi (asilimia 7.5). Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na athari za UVIKO-19 katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo utalii. Aidha, katika mwaka 2021, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.0 na kuendelea kuimarika hadi ukuaji wa wastani wa asilimia 5.4 katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024. Matarajio ya kuimarika kwa uchumi ni kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo: kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotarajiwa kuwa na matokeo makubwa kwenye uchumi; na kusambaza na kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19 hali ambayo inatarajiwa kuchochea utalii.

Katika mwaka 2020/21, Serikali imekusanya shilingi bilioni 31,280.1 sawa na asilimia 89.7 ya lengo ambapo shilingi bilioni 20,594.6 ni mapato ya ndani; na shilingi bilioni 10,685.5 ni misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ilitumia shilingi bilioni 31,280.1 kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo na kawaida. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 20,613.0 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 10,667.1 ni matumizi ya maendeleo.

Mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22 yameonesha kuwa Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi bilioni 36,681.9 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 423.1 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 36,258.8 yaliyopendekezwa katika Mwongozo. Mabadiliko hayo yalitokana na vipaumbele vya Serikali na maboresho mbalimbali ya kisera yaliyofanyika wakati wa uidhinishaji wa bajeti. Nyongeza hiyo ilielekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo barabara za mijini na vijijini pamoja na kugharamia mkongo wa taifa wa mawasiliano. Aidha, mapitio hayo yamebainisha uwepo wa haja ya kuendelea kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli kufuatilia utekelezaji ili kutatua changamoto zinazokabili Mafungu na kuleta ufanisi katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imekusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi bilioni 5,492.1 sawa na asilimia 89.0 ya lengo la shilingi bilioni 6,170.9. Mapato hayo yanajumuisha shilingi bilioni 4,719.5 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, mapato yasiyo ya kodi shilingi bilioni 579.8 ikijumuisha shilingi bilioni 64.4 zitokanazo na tozo ya miamala ya kutuma na kutoa fedha na shilingi bilioni 3.6 kodi ya majengo pamoja na shilingi bilioni 192.8 zilizokusanywa na Mamlaka za serikali za Mitaa. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imepokea misaada ya shilingi bilioni 152.8 sawa na asilimia 68.9 ya lengo; mikopo yenye masharti nafuu shilingi bilioni 381.6 sawa na asilimia 100.2 ya lengo; na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 1,171.9 sawa na asilimia 96.7 ya lengo. Mikopo ya ndani ilifikia jumla ya shilingi bilioni 1,220.9 sawa na asilimia 117.0 ya lengo la kipindi hicho. Vilevile, katika kipindi cha robo ya

kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imetoa ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 8,065.6 sawa na asilimia 89.3 ya lengo la shilingi 9,028.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,517.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,547.9 ni fedha za miradi ya maendeleo zikijumuisha shilingi bilioni 2,367.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 180.7 fedha za nje. Kadhalika, kiasi cha shilingi bilioni 353.7 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi.

Katika mwaka 2022/23, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 28,567.9 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 26,384.7 mwaka 2021/22. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.3 na kufikia shilingi bilioni 32,565.5 mwaka 2024/25. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 71.9 mwaka 2021/22 hadi asilimia 72.5 mwaka 2022/23 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 74.8 mwaka 2024/25. Katika kipindi hicho, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 39,387.5 kutoka shilingi bilioni 36,681.9 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Makadirio haya ni sawa na asilimia 22.4 ya Pato la Taifa. Katika muda wa kati, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 5.9 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 43,524.7 mwaka 2024/25. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 5,354.3 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi bilioni 4,348.3 kutoka vyanzo vya nje kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti kwa mwaka 2022/23.

Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutoa msukumo katika kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Vipaumbele hivyo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na uwekezaji; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Aidha, Serikali itahakikisha sera za mapato na matumizi katika muda wa kati zinajikita katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa. Hivyo, katika mwaka 2022/23, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia: Miradi ya kielelezo inayoendelea; Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; deni la Serikali; mishahara ya watumishi; na huduma za jamii zikiwemo afya, elimu na maji.

Utekelezaji wa Mpango na Bajeti unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali vinavyoweza kusababisha kutofikiwa kwa shabaha za vipaumbele vya Taifa. Hivyo, Mwongozo umeainisha mikakati mbalimbali itakayosaidia kuepuka au kupunguza athari za vihatarishi hivyo.

SEHEMU YA KWANZA

SERA NA MFUMO WA BAJETI YA SERIKALI

SURA YA KWANZA
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

1.1 Utangulizi

1. Sura hii inaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa Tanzania, kikanda na dunia kwa mwaka 2020, na mwelekeo wake katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024. Mapitio ya hali ya uchumi wa Tanzania yamezingatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/21 ambayo ni ya mwisho katika utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17- 2020/21). Vipaumbele hivyo ni: Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Maendeleo ya Watu; Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; na Kuimarisha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango. Aidha, mapitio ya hali ya uchumi yamezingatia: Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020; Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; Agenda 2063 ya Umoja wa Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 ya Umoja wa Mataifa.

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Sehemu hii inaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia na kikanda kwa mwaka 2020 na mwelekeo wake kwa mwaka 2021 na 2022 na athari za hali ya uchumi wa dunia na kikanda katika uchumi wa Tanzania.

1.2.1 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

3. Uchumi wa Dunia uliporomoka kutoka ukuaji wa asilimia 2.8 mwaka 2019 hadi ukuaji hasi wa asilimia 3.2 mwaka 2020. Hali hii ilitokana na athari za mlipuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19), ambapo mfumo wa uzalishaji, uhitaji wa huduma na bidhaa, na biashara ulivurugika kutokana na nchi nyingi kuchukua hatua za kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo zikiwemo kuzuia watu kutoka nje ya makazi yao, kuzuia safari za ndege za abiria, kuzuia mikusanyiko na kufunga mipaka ya nchi.

4. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Julai 2021, uchumi wa dunia unatarajiwa kuimarika kufikia ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2021 na asilimia 4.9 mwaka 2022. Hali hii inatokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na nchi mbalimbali kuimarisha uchumi, ikiwemo kuongeza matumizi katika maeneo yanayochochea shughuli za uchumi yaliyoathirika pamoja na sera za fedha za kuongeza ukwasi katika uchumi. Aidha, uchumi wa dunia utaimarika kutokana na kuimarika kwa huduma za afya ikiwemo chanjo katika kupunguza athari za UVIKO-19.

1.2.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi kwa Nchi Zilizoendelea na Zinazoendelea

5. Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea ulipungua na kufikia asilimia hasi 4.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.6 mwaka 2019. Aidha, ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea na kuibukia kiuchumi kwa mwaka 2020 ulipungua kufikia asilimia hasi 2.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.7 mwaka 2019. Kuporomoka kwa ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea kulitokana na athari za UVIKO-19. Katika mwaka 2021 uchumi wa nchi zilizoendelea unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.6 na uchumi wa nchi zinazoendelea na kuibukia kiuchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.3. Kuimarika kwa ukuaji wa uchumi katika nchi hizo kunatokana na kuimarika kwa huduma za afya katika kukabiliana na janga la UVIKO-19, kuongezeka kwa huduma za chanjo pamoja na hatua za kisera zinazoendelea kuchukuliwa na nchi hizo.

1.2.3 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara

6. Kulingana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), uchumi wa nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara uliathirika mwaka 2020 kutokana na milipuko wa UVIKO-19. Ukuaji wa uchumi katika ukanda huo ulipungua kufikia ukuaji hasi wa asilimia 1.8 mwaka 2020 kutoka ukuaji wa asilimia 3.2 mwaka 2019. Katika mwaka 2020, nchi 32 kati ya 45 zilikuwa na ukuaji hasi wa uchumi. Aidha, nchi mbili (Jamhuri ya Afrika ya Kati na Gambia) zilikuwa na ukuaji wa asilimia sifuri na nchi 11 ikiwemo Tanzania zilikuwa na ukuaji chanya. Miongoni mwa maeneo yaliyoathirika zaidi ni mauzo ya bidhaa nje na shughuli za utalii. Uchumi wa ukanda huo unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 mwaka 2021 na asilimia 4.1 mwaka 2022, kutokana na kuimarika kwa shughuli za biashara na uwekezaji duniani.

Jedwali Na. 1.1: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Maoteo (Asilimia)

	Halisi		**Maoteo**	
	2019	**2020**	**2021**	**2022**
Dunia	2.8	-3.2	6.0	4.9
Nchi Zilizoendelea	1.6	-4.6	5.6	4.4
Nchi Zinazoendelea na Kuibukia Kiuchumi	3.7	-2.1	6.3	5.2
China	6.0	2.3	8.1	5.7
India	4.0	-7.3	9.5	8.5
Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara	3.2	-1.8	3.4	4.1

Chanzo: *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Julai, 2021*

1.2.4 Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

7. Katika mwaka 2020, mwenendo wa uchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliathiriwa na mlipuko wa UVIKO-19, kwa kiasi kidogo ukilinganisha na

kanda nyingine. Kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kufikia asilimia 2.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na kuvurugika kwa biashara na shughuli za kiuchumi kulikosababishwa na hatua zilizochukuliwa na baadhi ya nchi wanachama kukabiliana na mlipuko wa UVIKO-19 zikiwemo kuzuia watu kutoka nje ya makazi yao, kuzuia safari za ndege za abiria, kuzuia mikusanyiko na kufunga mipaka ya nchi. Ukuaji wa uchumi katika baadhi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2020 ni kama ifuatavyo: Tanzania asilimia 4.8; Rwanda asilimia hasi 3.4, Uganda asilimia hasi 0.8 na Kenya asilimia hasi 0.3.

1.3 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

8. Kulingana na taarifa ya IMF ya mwezi Julai 2021 mfumuko wa bei wa dunia kwa mwaka 2020, ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.2, ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2019. Kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kilitokana na kutengamaa kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma. Hata hivyo, katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei uliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.5 mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 10.8 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilisababishwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame kwenye baadhi ya nchi.

9. Mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa asilimia 3.8 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2019/20. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula kwa baadhi ya nchi wanachama na kupungua kwa mahitaji ya mafuta. Aidha, viwango vya mfumuko wa bei vya nchi wanachama vilikuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko usiozidi asilimia 8. Mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.2.**

Jedwali Na. 1.2: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi	**Mfumuko wa Bei (Asilimia)**	
	2019/20	**2020/21**
Tanzania	3.5	3.3
Uganda	2.9	2.5
Kenya	5.4	5.3
Rwanda	6.3	4.2
Burundi	4.7	NA
Sudani ya Kusini	NA	NA
Wastani kwa Afrika Mashariki*	4.5	3.8

Chanzo: *Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi Husika*

NA: Hakuna takwimu

***** Wastani kwa Afrika Mashariki bila kujumuisha nchi ya Sudani ya Kusini mwaka 2019/20 na nchi za Burundi na Sudani ya Kusini mwaka 2020/21

1.4 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

1.4.1 Pato la Taifa

10. Katika mwaka 2020, uchumi ulikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 5.5 na ukuaji halisi wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na athari za UVIKO-19. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji, Tanzania iliweza kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizokuwa na ukuaji chanya wa uchumi katika mwaka 2020. Hali hii ilitokana na hatua ya Serikali ya kutositisha shughuli za biashara na uzalishaji wakati wa mlipuko wa UVIKO-19 (isipokuwa kwa kipindi kifupi tu cha robo ya pili ya mwaka 2020 ambapo baadhi ya shughuli zinazohusisha mikusanyiko ya watu kama shule, sanaa na burudani zilisitishwa kwa muda). Shughuli za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa mwaka 2020 ni pamoja na: ujenzi (asilimia 9.1); habari na mawasiliano (asilimia 8.4); na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.4). Aidha, sekta ya kilimo iliendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa mwaka 2020, ikichangia asilimia 26.9 ikifuatiwa na ujenzi (asilimia 14.4), biashara (asilimia 8.7), viwanda (asilimia 8.4) na uchukuzi (asilimia 7.5).

Kielelezo Na. 1.1: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa Mwaka 2020



11. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021, uchumi umekua kwa asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kupungua kwa kasi ya ukuaji katika kipindi hicho kumetokana na athari za UVIKO-19 katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Baadhi ya shughuli za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na habari na mawasiliano (asilimia 10.7), umeme (asilimia 9.6) na maji safi na maji taka (asilimia 8.7). Aidha, malazi na huduma za chakula

ndio shughuli ya kiuchumi iliyokuwa na kasi ndogo ya ukuaji (asilimia 1.0) lakini ikiwa imeimarika kutoka ukuaji hasi wa asilimia 6.7 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020. Hali hii ilisababishwa na athari za UVIKO-19 katika shughuli za malazi na huduma za chakula zinazojumuisha huduma za utalii. Shughuli nyingi za kiuchumi zimeendelea kuwa na viwango chanya vya ukuaji ingawa kasi yake ilipungua ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2020.

Kielelezo Na. 1.2: Ukuaji wa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020 na 2021



1.4.2 Mfumuko wa Bei

12. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Katika mwaka ulioishia mwezi Juni 2021, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Hali hii ilichangiwa na uzalishaji na usambazaji wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani, viwango tulivu vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme pamoja na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Aidha, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.0 mwezi Septemba 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

13. Mfumuko wa bei za vyakula ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 katika mwaka ulioishia Juni 2021, ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za vyakula kwenye masoko ya ndani. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula na nishati ulifikia asilimia 3.2 mwaka ulioishia Juni 2021

ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka ulioishia Juni 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa zikiwemo saruji na mafuta ya kupikia kulikosababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa hizo.

Kielelezo Na. 1.3: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei



1.4.3 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo

14. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Benki Kuu iliendelea kusimamia Sera ya Fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei ili uendelee kuwa tulivu na ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Aidha, sera hiyo ililenga kuongeza ukwasi katika sekta ya benki ili kuwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya kukuza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kufuatia usimamizi huo, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi[1] (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 7.6 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na asilimia 10.0 mwaka 2019/20. Kiwango cha ukuaji wa M3 kilikuwa chini ya lengo la mwaka 2020/21 la asilimia 10.0 kutokana na kupungua kwa shughuli za kiuchumi, hususan shughuli za biashara, utalii, na uwekezaji katika sekta binafsi.

15. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 4.3 katika mwaka 2020/21, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.1 katika mwaka 2019/20. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilitokana na athari za UVIKO-19 kwa

[1] Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi (Extended Broad Money - M3) hujumuisha fedha taslimu, amana za hundi, akiba za muda maalum, pamoja na amana za fedha za kigeni.

uchumi wa dunia, ambapo baadhi ya shughuli za biashara na uwekezaji nchini ziliathirika, hususan zinazohusiana na utalii na usafirishaji. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa kwenye shughuli binafsi, biashara na uzalishaji viwandani. Ukuaji wa mikopo unatarajiwa kuimarika katika mwaka 2021/22 kutokana na hatua za kiutawala na kisera zilizochukuliwa pamoja na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini na duniani.

Kielelezo Na 1.4: Mwenendo wa Ukuaji wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi



1.4.4 Mwenendo wa Viwango vya Riba

16. Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2021, riba za mikopo kwa ujumla zilipungua kufikia wastani wa asilimia 16.60 kutoka asilimia 16.80 Juni 2020. Kupungua kwa riba za mikopo kulitokana na Sera ya Fedha iliyolenga kuongeza ukwasi na usimamizi wa hatua mbalimbali za kupunguza riba na mikopo chechefu, ikiwemo matumizi ya kanzidata ya taarifa ya kumbukumbu za wakopaji. Vile vile, riba za mikopo za mwaka mmoja zilipungua kufikia asilimia 15.80 Juni 2021, kutoka asilimia 16.22 Juni 2020. Katika kipindi hicho, wastani wa riba za amana za miezi 12 ilifika wastani wa asilimia 8.43 Juni 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.65 katika kipindi kama hicho 2020. Kufuatia mwenendo huo, tofauti ya viwango vya riba vya kukopa na riba ya amana ya mwaka mmoja ilipungua na kufikia asilimia 7.37 kutoka asilimia 7.57 Juni 2021. Aidha, katika kipindi hicho riba za dhamana za Serikali kwa ujumla zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.75 kutoka asilimia 5.85.

1.4.5 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

17. Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara dhidi ya sarafu za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni katika kipindi chote cha mwaka 2020/21. Hali hii

imechangiwa na: utulivu wa bei nchini; utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti; usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni; kuimarika kwa urari wa biashara; na utulivu wa bei ya mafuta katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,309.58 ikilinganishwa na shilingi 2,301.30 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Badiliko hilo lilikuwa la kiasi cha asilimia 0.40 kwa mwaka ikilinganishwa na asilimia 0.36 katika mwaka uliopita. Kiwango hicho kilikuwa kidogo na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizoweza kuwa na utulivu wa kiwango cha kubadilisha fedha dhidi ya fedha za kigeni licha ya athari za UVIKO-19.

1.4.6 Mwenendo wa Sekta ya Benki

18. Katika mwaka 2020/21, mapato na faida kutokana na uwekezaji katika rasilimali na mtaji yaliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/20. Katika kipindi hicho, faida ya benki itokanayo na mali (*Returns on Asset - ROA*) ilifikia wastani wa asilimia 2.42 kutoka wastani wa asilimia 2.19 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20 na faida ya benki itokanayo na mtaji (*Returns on Equity - ROE*) ilifikia wastani wa asilimia 10.47 kutoka wastani wa asilimia 9.88 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Mwenendo huu unaonesha kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki ambapo kumekuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya kila siku ya wenye amana na wakopaji.

19. Katika mwaka unaoishia Juni 2021, mikopo chechefu ilipungua kufikia asilimia 9.30 kutoka asilimia 10.84 kwa mwaka ulioishia Juni 2020. Hali hii inaashiria kuimarika kwa thamani ya rasilimali za benki nchini. Mwenendo huu ulichochewa na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu ikiwa ni pamoja na: Kutoa maelekezo kwa benki kuendelea kutumia kanzidata ya taarifa za wakopaji (*credit reference system*) katika utoaji wa mikopo; kuimarisha mifumo ya udhibiti wa benki; benki kuendelea kuimarisha viwango vya uchambuzi wa maombi ya mikopo; kusimamia maadili ya wafanyakazi wa benki; kufanya ukaguzi maalum wa wafanyakazi (*staff audit*) wa benki mara kwa mara; na kuzielekeza benki na taasisi za fedha kutekeleza mikakati ya kupunguza mikopo chechefu na kutoa taarifa kila robo mwaka. Aidha, Benki Kuu ilitoa tamko mwezi Februari 2021 kuzielekeza benki za biashara kutotoa gawio au motisha (*bonuses*) kwa wanahisa au wafanyakazi endapo mikopo chechefu itazidi asilimia 5.0 ambalo limeendelea kutekelezwa.

1.4.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

20. Sekta ya nje iliathirika moja kwa moja na athari za UVIKO-19, hususan shughuli za usafiri wa anga na utalii. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2021, urari wa malipo ya kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,414.2

ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,127.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

21. Kwa mwaka ulioishia Juni 2021, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 8,850.3 kutoka dola za Marekani milioni 9,347.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Mauzo ya bidhaa asilia yalifikia dola za Marekani milioni 578.4 kutoka dola za Marekani milioni 995.9 Juni 2020. Hali hii ilitokana na kupungua kwa bei na thamani ya baadhi ya bidhaa asilia. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 5,567.8 kutoka dola za Marekani milioni 4,574.9 Juni 2020 kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za mbogamboga, bidhaa za viwandani na madini. Mauzo ya dhahabu nje ya nchi yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 3,028.8 Juni 2021 kutoka dola za Marekani milioni 2,591.3 Juni 2020 kutokana na kuimarika kwa bei katika soko la dunia na jitihada zinazofanywa na Serikali kuimarisha sekta ya madini.

22. Thamani ya bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ilipungua kufikia dola za Marekani milioni 9,869.7 katika mwaka unaoishia Juni 2021 kutoka dola za Marekani milioni 10,043.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Hali hii ilitokana na kushuka kwa uagizaji wa vyakula na bidhaa za uzalishaji kama vile vifaa vya usafiri pamoja na bidhaa za ujenzi kutokana na kuathirika kwa usambazaji wa bidhaa hizo duniani kufuatia mlipuko wa UVIKO-19.

23. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Juni 2021, kulikuwa na akiba ya fedha za kigeni ya dola za Marekani bilioni 5.2, ambayo inatosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 6.1. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jedwali Na. 1.4: Urari wa Malipo ya Kawaida

	2019/20	2020/21	Badiliko (%)
Bidhaa	-2,566.7	-2,129.2	-17.0
Mauzo Nje	5,868.7	6,457.9	10.0
Uagizaji Nje	8,435.4	8,587.0	1.8
Huduma	1,870.4	1,109.7	-40.7
Mapato	3,478.7	2,392.4	-31.2
Malipo	1,608.3	1,282.7	-20.2
Bidhaa na Huduma	-696.3	-1,019.4	---
Mauzo ya bidhaa na huduma	9,347.4	8,850.3	-5.3
Uagizaji bidhaa na huduma	10,043.7	9,869.7	-1.7
Mapato ya Vitega uchumi	-895.1	-831.2	-7.1
Mapato	194.4	59.7	-69.3
Malipo	1,089.5	890.9	-18.2
Uhamisho wa Mali	464.4	436.4	-6.0
Zilizoingia	518.0	488.8	-5.6
Kwa Serikali Kuu	203.0	75.3	---
Zilizotoka	53.6	52.4	-2.4
Urari wa Malipo ya Kawaida	-1,127.0	-1,414.2	25.5

Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*

1.5 Deni la Serikali

24. Deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 64,497.83 Juni 2021, ikilinganishwa na shilingi bilioni 56,449.8 Juni 2020, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 45,563.5 na deni la ndani ni shilingi bilioni 18,934.3. Mwenendo huo wa deni umetokana na kupokelewa kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo hususan inayochochea ukuaji wa uchumi. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2020 inaonesha kuwa Deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo unaokubalika kimataifa kwa viashiria vyote muhimu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa: uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; uwiano wa thamani ya sasa ya deni la

nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 17.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240.

1.6 Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania

1.6.1 Pato la Taifa

25. Katika mwaka 2021, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.0 kutoka maoteo ya awali ya asilimia 5.6. Kupungua kwa maoteo ya ukuaji wa uchumi kunatokana na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa baadhi ya viashiria muhimu vya uchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021 pamoja na hali isiyotabirika ya mwenendo wa UVIKO-19 duniani. Viashiria vya uchumi vilivyokuwa na mwenendo usioridhisha ni pamoja na: Ukuaji wa asilimia 4.7 wa Pato la Taifa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020; kupungua kwa mapato ya kodi[2] kwa asilimia 0.6 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2020; kupungua kwa uzalishaji wa saruji kwa asilimia 0.5 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na nusu ya kwanza ya mwaka 2020; na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi hadi wastani wa asilimia 3.4 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, maoteo ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2021 yamezingatia hali halisi ya athari za UVIKO-19 ambayo yalisababisha ukuaji halisi wa uchumi kwa mwaka 2020 kuwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na maoteo ya ukuaji wa asilimia 5.5.

26. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na: Kusambaza na kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19 hali ambayo inatarajiwa kuchochea utalii; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotarajiwa kuwa na matokeo makubwa kwenye uchumi; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; ulipaji wa madai na madeni; na kuimarisha ukusanyaji wa mapato pamoja na kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Kwa kuzingatia hatua hizo pamoja na matarajio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.4 katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024. Aidha, kuimarika kwa uchumi wa dunia kunatarajiwa kuongeza msukumo katika ukuaji wa uchumi kutokana na kuimarika kwa masoko ya bidhaa nje ya nchi na uwekezaji wa mitaji kutoka nje ya nchi.

[2] Kodi zilizopungua ni ushuru wa bidhaa ndani, kodi za mapato na kodi ya ongezeko la thamani ndani, ikiashiria kushuka kwa uzalishaji wa ndani.

Kielelezo Na. 1.5: Ukuaji na Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania



1.6.2 Mfumuko wa Bei

27. Mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kuendelea kubaki ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3 hadi 5 pamoja na kuendana na vigezo (*convergency criteria*) vilivyowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Matarajio ya kasi ndogo ya mfumuko wa bei yanatokana na: kupungua kwa gharama za uzalishaji kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya gesi na umeme; usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti; na matarajio ya upatikanaji wa chakula kwenye masoko ya ndani na nchi jirani kutokana na hali nzuri ya hewa.

SURA YA PILI
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

2.1 Utangulizi

28. Sura hii inaeleza mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22 na utekelezaji wa bajeti katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22. Mapitio hayo yamefanyika kwa kuzingatia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika mwongozo huo, mrejesho wa vikao vya uchambuzi wa bajeti za mafungu kwa mwaka 2021/22, maoni ya wadau katika vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21, maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 pamoja na maoni ya wadau yaliyotolewa katika vikao kazi mbalimbali vya Serikali kuhusu maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Aidha, maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/21 yapo katika **Kiambatisho B**.

2.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2021/22

29. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22, ulipendekeza kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 36,258.8. Kufuatia vipaumbele vya Serikali na maboresho mbalimbali ya kisera yaliyofanyika wakati wa uidhinishaji wa bajeti, Sura ya bajeti ya Serikali ilibadilika kutoka mapendekezo ya shilingi bilioni 36,258.8 hadi shilingi bilioni 36,681.9 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 423.1 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.1.** Nyongeza hiyo iliyotokana na tozo ya shilingi 100 kwenye bidhaa ya mafuta ya petroli ilielekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo barabara za mijini na vijijini pamoja na kugharamia mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Jedwali Na.1: Mapendekezo ya Bajeti ya Mwongozo na Bajeti Iliyoidhinishwa

Shilingi Bilioni

	Mapendekezo ya Bajeti ya Mwongozo	Bajeti Iliyoidhinishwa
Mapato ya Ndani	**26,032,576**	**26,384,735**
Mapato ya Kodi (TRA)	21,468,230	21,841,656
Mapato Yasiyo ya Kodi (TRA)	629,447	629,447
Mapato Yasiyo ya Kodi	3,071,042	3,049,774
Mapato ya Halmashauri	863,858	863,858
Misaada	**1,127,188**	**1,138,076**
Misaada ya Kibajeti	-	-
Misaada ya Maendeleo	904,618	915,506
Mifuko ya Kisekta	222,570	222,570
Mikopo Nafuu	**1,757,802**	**1,817,847**
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	-	-
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,698,066	1,758,111
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	59,736	59,736
Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje	**2,352,107**	**2,352,107**
Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani	**4,989,133**	**4,989,133**
Mikopo ya Kugharamia Miradi	1,838,796	1,838,796
Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani	3,150,337	3,150,337
JUMLA YA MAPATO	**36,258,806**	**36,681,898**
Matumizi ya Kawaida	**23,002,951**	**23,002,951**
Mishahara	8,150,509	8,150,509
Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni & CFS)	10,663,278	10,663,278
Matumizi Mengineyo	4,189,164	4,189,164
Matumizi ya Maendeleo	**13,255,855**	**13,678,946**
Miradi ya Fedha za Ndani	10,370,865	10,723,023
Miradi ya Fedha za Nje	2,884,990	2,955,923
JUMLA MATUMIZI	**36,258,806**	**36,681,898**

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

2.3 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika kipindi cha robo ya Kwanza kwa Mwaka 2021/22

2.3.1 Mapato

30. Mapato yaliyokusanywa kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje katika kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka 2021/22 ni shilingi bilioni 8,419.3 sawa na asilimia 93.3 ya lengo la shilingi bilioni 9,028.7. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 5,492.1 sawa na asilimia 89.0 ya lengo la shilingi bilioni 6,170.9. Mapato ya ndani yanajumuisha; shilingi bilioni 4,719.5 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; shilingi bilioni 579.8 ni mapato yasiyo ya kodi; na shilingi bilioni 192.8 ni mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 534.4 sawa na asilimia 88.6 ya lengo la shilingi bilioni 602.9. Kwa upande wa mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia shilingi bilioni 1,220.9 sawa na asilimia 117.0 ya lengo la shilingi bilioni 1,043.2 na mikopo ya nje ilifikia shilingi bilioni 1,171.9 sawa na asilimia 96.6 ya lengo la shilingi bilioni 1,211.6. Mikopo ya ndani ilivuka lengo katika robo husika kutokana na mwitikio mzuri wa wawekezaji, hususan katika hatifungani za muda mrefu. Hata hivyo, Serikali itahakikisha kwamba ukomo uliowekwa kwa mwaka 2021/22 utazingatiwa ili kutoathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

31. Kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya ndani katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kukwepa kodi hususan kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa stakabadhi za kielektroniki wakati mauzo yanapofanyika hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato pamoja na uwepo wa UVIKO – 19 ulioathiri shughuli za kiuchumi na kibiashara.

2.2.2 Matumizi

32. Ridhaa ya matumizi zilizotolewa katika kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka 2021/22 ni shilingi bilioni 8,065.6 sawa na asilimia 89.3 ya lengo la shilingi 9,028.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,517.7 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,547.9 ni fedha za maendeleo. Aidha, fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa zinajumuisha: shilingi bilioni 2,053.0 kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 1,935.6 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali; na shilingi bilioni 1,529.2 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 2,367.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 180.7 fedha za nje. Vilevile, kiasi cha shilingi bilioni 353.7 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi.

2.4 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/22

33. Sehemu hii inaelezea utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22. Maelekezo hayo ni pamoja na:

34. **Uzingatiaji wa Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22.** Kifungu Na. 15 (1) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, kimebainisha kutakuwa na Kamati ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ambapo wajumbe wametajwa kwenye Kanuni. Mapitio ya utekelezaji wa matakwa ya sheria yamebaini kuwa Kamati ya Kitaifa ya maandalizi ya Mwongozo iliundwa na kukamilisha jukumu lake kwa wakati. Mwongozo uliidhinishwa na mamlaka zote zinazohusika ndani ya Serikali na Bunge kwa muda uliopangwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali mwezi Februari 2021.

35. Mapitio ya utekelezaji yameonesha kuwa, ratiba ya maandalizi ya mpango na bajeti ilizingatiwa na Maafisa Masuuli kama ilivyobainishwa kwenye mwongozo ambapo vitabu vya mapendekezo ya mpango na bajeti viliwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, mapendekezo ya mipango na bajeti yaliwasilishwa katika Kamati husika za Kudumu za Bunge.

36. **Mgawanyo wa Matumizi ya Fedha za Mapato ya Ndani kulingana na Makundi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa:** Katika uandaaji wa ukomo wa bajeti, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilikamilisha uandaaji wa madaraja ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kulingana na uwezo wa kukusanya mapato ambapo Halmashauri 16 zinazokusanya mapato zaidi ya shilingi bilioni 5 ziliwekwa katika Daraja A na Halmashauri 168 zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni 5 ziliwekwa katika Daraja B. Aidha, wakati wa uchambuzi wa bajeti ilibainika kuwa Halmashauri za Daraja A zilipanga kutumia asilimia 60 ya bajeti zao kwa ajili ya maendeleo na asilimia 40 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Halmashauri za daraja B zilitenga asilimia 40 kwa ajili ya maendeleo na asilimia 60 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kama ilivyoelekezwa.

37. **Utengaji wa Asilimia 10 ya Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa ajili ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**: Halmashauri zote zilizingatia maelekezo ya mwongozo ya kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya wanawake (asilimia 4), vijana (asilimia 4) na watu wenye ulemavu (asilimia 2). Taarifa ya mikopo ya asilimia 10 iliyotolewa kwa kila halmashauri kwa mwaka 2020/21 imeainishwa katika **Kiambatisho A**.

38. **Utendaji wa Kamati za Bajeti**: Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 Kifungu cha 18(2) na Kanuni ya 17(2) vinaelekeza Maafisa Masuuli kuunda Kamati za Bajeti ambazo zinapaswa kushiriki kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa Mipango na Bajeti za Mafungu yao. Kupitia vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa kuna umuhimu wa kuziimarisha Kamati hizo ili kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake kikamilifu.

39. **Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Mapato:** Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia maelekezo ya kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Kupitia vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa baadhi ya mifumo bado ina changamoto za kiufundi, kutowasiliana mfano Local government Revenue Collection Information System (LGRCIS) na Government Of Tanzania Hospital Management Information System (GoT-HoMIS), sanjari na upungufu wa wataalamu.

40. **Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP):** Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 na Kanuni zake za mwaka 2020, kifungu cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 vimebainisha na kuelekeza kuhusu kujumuisha miradi ya PPP katika mpango na bajeti. Wakati wa uchambuzi wa bajeti 2021/22 ilibainika kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kujenga uwezo wa Mafungu ili kuyawezesha kuandaa miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ili ijumuishwe katika bajeti ya Serikali.

41. **Uzingatiaji wa Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha Katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na Waraka wa Hazina Na. 1 wa Mwaka 2020:** Miongozo hii inatoa maelekezo kuhusu utaratibu wa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/22. Kutokana na mapitio ya utekelezaji wa miongozo hiyo, ilibainika kuwa baadhi ya Mafungu hayakuzingatia kwa ukamilifu maelekezo ya miongozo husika. Aidha, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa upo umuhimu wa kuendelea kuwajengea uelewa wataalamu kuhusu utekelezaji wa miongozo hiyo.

42. **Hatua za Kudhibiti Matumizi:** Serikali imetoa miongozo mbalimbali kwa lengo la kudhibiti matumizi ya mali na fedha za umma. Wakati wa vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa baadhi ya maelekezo hayakuzingatiwa kikamilifu, hivyo Mwongozo wa mwaka 2022/23 umeendelea kuwasisitiza Maafisa Masuuli

kuzingatia miongozo husika ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Miongozo hiyo ni pamoja na: Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha Katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Waraka wa Hazina Na. 1 wa Mwaka 2020 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2020/21 na Waraka wa Hazina Na. 1 wa mwaka 2018/19 kuhusu Mkakati wa Kudhibiti Madeni ya Serikali.

43. **Uwasilishaji wa Michango na Gawio:** Serikali imeendelea kusimamia Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kuelekeza mashirika na taasisi za umma kuwasilisha michango na gawio stahiki katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ambapo, kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina ya Mwaka 2020/21 jumla ya mashirika na taasisi za umma 204 kati ya 237 ziliwasilisha michango na gawio. Hivyo, wakati wa vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha taasisi na mashirika ya umma ili yaweze kujiendesha kwa ufanisi na kuchangia kikamilifu katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

44. **Kuhuisha Mipango Mikakati na Wasifu wa Taasisi za Umma:** Maafisa Masuuli walielekezwa kuhuisha Mipango Mikakati na wasifu wa taasisi zao ili ziendane na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Kupitia vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa baadhi ya mafungu walitekeleza na wengine wanaendelea na uhuishaji katika mwaka 2021/22.

45. **Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti:** Kwa mujibu wa Kifungu Na. 55(4) na Kanuni ya 29(5) za Sheria ya Bajeti, Sura 439, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa bajeti za kila robo mwaka katika muda wa siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka. Kutokana na mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22 ilibainika kuwa upo umuhimu wa kuendelea kuhimiza na kufuatilia uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa wakati.

46. **Uzingatiaji Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada**: Kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kupokea kwa niaba ya Serikali misaada yoyote inayotolewa kwa Serikali. Utekelezaji wa sheria hiyo umeendelea kuzingatiwa katika upokeaji wa misaada, mikopo na utoaji wa dhamana ambapo serikali imeendelea kupokea misaada na mikopo nafuu ikiwemo ya kupamabana na janga la UVIKO-19 na katika programu na miradi ya mbalimbali ya maendeleo kwa sekta za kilimo, afya, ujenzi, nishati, fedha na elimu. Aidha,

kumekuwa na changamoto ya uzingatiaji wa sheria hiyo hususan katika miradi inayotekelezwa na Asasi Zisizo za Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hivyo kuleta changamoto katika upokeaji na matumizi ya fedha husika.

SURA YA TATU
MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

3.1 Utangulizi

47. Sura hii inaainisha malengo, misingi na shabaha ya uchumi jumla kwa kuzingatia mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi wa Tanzania kikanda na dunia. Aidha, inaainisha sera na mikakati ya kuongeza mapato ya ndani na nje ya nchi, matumizi pamoja na ugharamiaji wa nakisi ya bajeti. Sura hii pia, imeainisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23 na katika kipindi cha muda wa kati. Vilevile, sura hii imeainisha vipaumbele vitakavyotekelezwa katika kipindi cha muda wa kati. Kwa mujibu wa Kifungu 21(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, Serikali ina wajibu wa kuandaa na kutekeleza sera wezeshi za kibajeti ili kuchochea ukuaji wa uchumi, kuongeza uwekezaji na kuboresha ustawi wa wananchi. Sera zilizoainishwa katika sura hii zinalenga kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) wenye dhima ya ***"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"***.

3.2 Malengo na Shabaha ya Uchumi Jumla

48. Mwaka 2021, Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.0 na kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2022; mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 5.0 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya ndani kufikia asilimia 16.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2022/23; nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na kuhakikisha kuwa viashiria vya ustawi wa jamii vinaimarika.

3.3 Misingi ya Uchumi Jumla

49. Misingi itakayozingatiwa kufikia shabaha za uchumi jumla ni pamoja na: kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili; kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa; kuendelea kuwa na utoshelevu wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani.

3.4 Vipaumbele katika Muda wa Kati

50. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutoa msukumo katika kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Vipaumbele hivyo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na

uwekezaji; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu. Aidha, Serikali itahakikisha sera za mapato na matumizi katika muda wa kati zinajikita katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa. Hivyo, katika mwaka 2022/23, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia: Miradi ya kielelezo inayoendelea; Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; deni la Serikali; mishahara ya watumishi; na huduma za jamii zikiwemo afya, elimu na maji.

3.5 Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati

3.5.1 Sera za Mapato ya Ndani

51. Sera za mapato ya ndani katika muda wa kati zinalenga kuongeza makusanyo kwa kutekeleza hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero;

(ii) Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari na kuongeza wigo wa kodi;

(iii) Kurasimisha sekta isiyo rasmi kwa kuzitambua na kuzisajili shughuli zisizo rasmi katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato;

(v) Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato; na

(vi) Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa na kuzuia matumizi mabaya ya misamaha.

3.5.2 Makadirio ya Mapato ya Ndani

52. Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 28,567.9 mwaka 2022/23 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 26,384.7 mwaka 2021/22. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.3 na kufikia shilingi bilioni 32,565.5 mwaka 2024/25. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 71.9 mwaka 2021/22 hadi asilimia 72.5 mwaka 2022/23 na kuongezeka hadi asilimia 74.8 mwaka 2024/25. Mapato ya ndani kwa Pato la Taifa yanakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 16.2 katika muda wa kati.

53. Katika mwaka 2022/23, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (Kodi na Yasiyo ya Kodi) yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 7.9 hadi shilingi bilioni 24,237.8 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 22,471.10 mwaka 2021/22. Katika muda wa kati, mapato hayo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.2 hadi shilingi bilioni 27,709.5 mwaka 2024/25. Mchanganuo wa mapato ya ndani ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 3.1.**

Kielelezo Na. 3.1: Makadirio ya Mapato ya Ndani katika Muda wa Kati

Shilingi bilioni



54. Katika muda wa kati, Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 3,913.6 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 4,330.1 mwaka 2022/23 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 4,855.9 mwaka 2024/25. Mapato hayo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.5 katika muda wa kati. Mchanganuo wa mapato yasiyo ya kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 3.2.**

Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) katika Muda wa Kati

Shilingi bilioni



55. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mahsusi ya kisera na kiutawala ili kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani. Mikakati hiyo ni pamoja na:

(i) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (BLUEPRINT);

(ii) Kuwatengea wafanyabiashara na watoa huduma wadogo maeneo maalum na kuwapatia huduma muhimu za kijamii kwa lengo la kukuza biashara zao pamoja na kutoa fursa kwa wafanyabiashara walio rasmi kulipa kodi stahiki;

(iii) Kupanua wigo wa kodi kwa kutekeleza Kampeni ya Mlango kwa Mlango inayolenga kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili walipakodi pamoja na kuwatambua walipakodi wapya na kuwasajili;

(iv) Kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ili kurahisisha ulipaji kodi na uwasilishaji wa ritani za kodi kielektroniki (electronic filing);

(v) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashine za kutolea stakabadhi za kielektroniki (EFD) kwa kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Mashine za Utoaji Stakabadhi Kielektroniki (EFDMS) na Mfumo wa Kihasibu wa Mlipa Kodi (Virtual EFD) ambazo zitawezesha kupata taarifa za ununuzi kwa wakati kwa kila muamala. Aidha, Serikali itaboresha mashine za EFD (Protocal 2.1) zenye uwezo wa kutoa taarifa za ununuzi na mauzo kwa wakati;

(vi) Kuendelea na utaratibu wa kuingia makubaliano na walipakodi ili kuwawezesha kulipa madeni yao kwa awamu;

(vii) Kutumia Mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki la Tanzania (TeSWs) ili kurahisisha uondoshwaji wa mizigo inayoingia na kutoka kupitia vituo vya forodha mipakani na hivyo kupunguza gharama za kufanya biashara nchini;

(viii) Kuimarisha ushirikiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na vyombo vya ulinzi na usalama nchini kwa kufanya doria kwenye mipaka yote nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo;

(ix) Kuendelea kutumia Mpango wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Compliance Risk Management Plan) ili kuongeza uhiari wa ulipaji kodi;

(x) Kuimarisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuhimiza malipo ya Serikali kutumia Namba ya Kumbukumbu ya Malipo (Control Number);

(xi) Kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati;

(xii) Kujenga uwezo wa wataalam katika kushughulikia biashara mtandao ili kutoza kodi stahiki; na

(xiii) Kudhibiti ukwepaji kodi unaofanywa na biashara za kimataifa katika uhamishaji wa faida na kumomonyoa wigo wa kodi (Base Erosion and Profit

Shifting – BEPS) kwa kuendelea kuwajengea uwezo wataalam.

3.6 Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati

Sera za Misaada

56. Serikali itaendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha na kuratibu juhudi za pamoja za Serikali na Washirika wa Maendeleo za upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Aidha, Serikali itazingatia misingi ifuatayo ya kisera katika ushirikiano na Washirika wa Maendeleo:

(i) Kuratibu na kusimamia ratiba za majadiliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo;
(ii) Kuhakikisha sehemu kubwa ya fedha za misaada inaelekezwa kwenye maeneo yenye tija na matokeo chanya kwa Taifa;
(iii) Kuhamasisha Washirika wa Maendeleo kuzingatia mifumo na vipaumbele vya Serikali katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti;
(iv) Kuzingatia misingi ya utawala bora na utawala wa sheria;
(v) Kusimamia utaratibu wa kisera wa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo;
(vi) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo; na
(vii) Kuchambua, kuhakiki na kuwasilisha kwa Washirika wa Maendeleo nyaraka zinazoakisi gharama halisi za utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo.

57. Misaada ya Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 1,117.0 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,138.1 mwaka 2021/22 na kubaki katika viwango hivyo 1,102.6 mwaka 2024/25. Misaada kupitia Mifuko ya Pamoja ya Kisekta inatarajiwa kubaki katika viwango vilivyokadiriwa katika mwaka 2021/22 kwa kipindi cha muda wa kati. Aidha, misaada ya miradi ya maendeleo inatarajiwa kupungua kutoka shilingi bilioni 915.5 mwaka 2021/22 kufikia shilingi bilioni 824.0 mwaka 2022/23 na kuwa shilingi bilioni 861.3 mwaka 2024/25. Kupungua kwa misaada kunatokana na kubadilika kwa sera za nchi zinazotoa misaada kwa kutenga kiwango kikubwa katika mikopo na kupunguza misaada.

3.7 Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati

Sera za Matumizi

58. Sera za Matumizi zitajumuisha yafuatayo:

(i) Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma;

(ii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;

(iii) Kutenga fedha na kulipa madeni yaliyohakikiwa na kudhibiti uzalishaji wa madeni mapya na ulimbikizaji wa madeni;

(iv) Kuboresha mishahara ya watumishi wa umma na kugharamia Deni la Serikali kwa kutumia mapato ya ndani;

(v) Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya asili na athari za magonjwa ya mlipuko ikiwa ni pamoja na UVIKO – 19;

(vi) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi;

(vii) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kudhibiti matumizi ya Serikali na kujenga uwezo wa wataalam wa ndani katika eneo la ulinzi na usalama wa mifumo (systems security) inayodhibiti matumizi; na

(viii) Kugharamia Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

59. **Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Mapato na Matumizi**: Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, OR - TAMISEMI, eGA na NIDC (National Internet Data Center) itaendelea kufanya tathmini ya mifumo ya usimamizi wa fedha ili kubainisha mifumo yenye matumizi yanayofanana na kuunganishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa mifumo. Kwa upande wa mapato, juhudi zinafanyika ili kuwa na 'billing system' moja kwa taasisi zenye majukumu ya kufanana.

3.7.1 Makadirio ya Matumizi

60. Katika mwaka 2022/23 matumizi ya Serikali yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 39,387.5 kutoka shilingi bilioni 36,681.9 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Makadirio haya ni sawa na asilimia 22.4 ya Pato la Taifa. Katika muda wa kati, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 5.9 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 43,524.7 mwaka 2024/25. Maeneo yanayotarajiwa kuwa na matumizi makubwa ni pamoja na: mahitaji ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikijumuisha ulipaji wa deni la Serikali; kugharamia mishahara ya Watumishi wa Umma; pamoja na kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo inayoendelea. **Kielelezo Na. 3.3** kinaonesha makadirio ya matumizi katika muda wa kati

Kielelezo Na. 3.3: Mwenendo wa Makadirio ya Matumizi katika Muda wa Kati

Shilingi bilioni



61. Katika mwaka 2022/23, matumizi ya kawaida yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 24,708.6 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 23,003.0 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Makadirio haya ni sawa na asilimia 14.1 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, gharama za kuhudumia Deni la Serikali ikijumuisha gharama nyingine za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali (CFS) zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 11,421.6 mwaka 2022/23 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 10,673.5 mwaka 2021/22 na Mishahara kwa Watumishi wa Umma inakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 9,139.1 mwaka 2022/23 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 8,150.5 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Ongezeko hili linatokana na mapendekezo ya nyongeza ya mishahara ya Watumishi wa Umma na ajira mpya. Matumizi Mengineyo (OC) yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4,147.9 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4,152.9 mwaka 2021/22.

62. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 14,678.9 mwaka 2022/23. Makadirio ya matumizi ya maendeleo yamezingatia: kuendelea kwa miradi ya kimkakati; kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; kugharamia elimumsingi bila ada; kulipa madeni ya wakandarasi; kugharamia miradi ya kielelezo kama inavyooneshwa kwenye mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.6 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 16,103.4 mwaka 2024/25. Mgawanyo wa matumizi ya kawaida na maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 3.4.**

Kielelezo Na. 3.4 Makadirio ya Aina Kuu za Matumizi

Shilingi Bilioni



3.7.2 Makadirio ya Matumizi Kisekta

63. Matumizi kisekta yanajumuisha matumizi kwa kuzingatia majukumu na shughuli za Serikali. Matumizi haya yamegawanyika katika sekta za: Huduma za Utawala na Deni la Serikali; Maendeleo ya Uchumi; Elimu; Ulinzi, Sheria na Usalama; Afya; Hifadhi ya Jamii; na Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii.

64. Katika muda wa kati, makadirio ya matumizi katika sekta ya Huduma za Utawala na Deni la Serikali yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 14,396.9 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 15,229.7 mwaka 2022/23 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 17,530.2 mwaka 2024/25. Aidha, makadirio ya matumizi katika sekta ya Maendeleo ya Uchumi yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 8,330.7 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 9,030.6 mwaka 2022/23 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 9,717.3 mwaka 2024/25. Vilevile, matumizi katika sekta ya Elimu yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 5,257.3 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 5,699.1 mwaka 2022/23 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 6,132.4 mwaka 2024/25.

65. Matumizi katika sekta ya Ulinzi, Sheria na Usalama yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 3,532.7 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 3,829.6 mwaka 2022/23 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 4,120.6 mwaka 2024/25. Matumizi katika sekta ya Afya yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 2,019.2 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 2,188.9 mwaka 2022/23

na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 2,355.3 mwaka 2024/25. Matumizi katika sekta ya Hifadhi ya Jamii yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 1,853.4 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 2,009.2 mwaka 2022/23 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 2,161.9 mwaka 2024/25. Matumizi katika sekta ya Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 1,291.8 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 1,400.3 mwaka 2022/23 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 1,506.8 mwaka 2024/25. Mgawanyo wa makadirio kwa kila Sekta umeoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3.6 na Jedwali Na. 3.6.**

Kielelezo Na. 3.6: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kisekta

Shilingi bilioni



3.8 Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti

66. Katika muda wa kati, Serikali itagharamia nakisi ya bajeti kwa kuendelea kukopa kutoka vyanzo vya ndani na nje ili kugharamia miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Madeni (2020/21-2023/24). Serikali itatumia fursa ya mikopo yenye masharti nafuu kutoka Taasisi za Fedha za Kimataifa na Wakala wa Mikopo wa Kimataifa wanaotoa mikopo kwa utaratibu wa *Export Credit Agencies* ili kugharamia miradi mikubwa ya kimkakati. Serikali itakopa kwa masharti ya kibiashara pale kutakapokuwa na uhaba wa mikopo ya masharti nafuu.

3.8.1 Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani

67. Mikopo kutoka soko la ndani itaendelea kuwa chanzo muhimu cha kugharamia bajeti ya Serikali. Hivyo, Serikali itaendelea na hatua mbalimbali za kukuza na kuendeleza chanzo hiki kwa kutoa elimu na kuboresha miundombinu kwa lengo la kuongeza wigo wa wawekezaji. Katika mwaka 2022/23, Serikali

inatarajia kukopa shilingi bilioni 5,354.3 ambapo shilingi bilioni 3,300.0 ni kwa ajili ya kulipia mikopo itakayoiva na shilingi bilioni 2,054.3 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Katika muda wa kati, mikopo kutoka vyanzo vya ndani itakopwa kwa kiwango ambacho hakitaathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

3.8.2 Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje

68. Katika mwaka 2022/23, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 4,348.3 kutoka vyanzo vya nje ambapo, mikopo yenye masharti nafuu ni shilingi bilioni 1,926.4 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ni shilingi bilioni 2,421.9. Katika muda wa kati, Serikali inatarajia kukopa wastani wa shilingi bilioni 4,524.3 kwa mwaka.

3.9 Mfumo wa Bajeti

69. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti katika kipindi cha muda wa kati ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3.1 hadi 3.5**

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati

Shilingi Milioni

	2021/22 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)	**26,384,735**	**28,567,860**	**30,470,270**	**32,565,460**
Mapato ya Ndani	**25,520,877**	**27,630,809**	**29,513,331**	**31,571,105**
Mapato ya TRA (Kodi na Yasiyo Ya Kodi)	22,471,103	24,237,760	25,851,539	27,709,536
Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika)	3,049,774	3,393,050	3,661,792	3,861,569
Mapato ya Halmashauri	**863,858**	**937,051**	**956,939**	**994,355**
Jumla ya Matumizi	**30,480,207**	**33,097,797**	**35,124,594**	**36,867,214**
Matumizi ya Kawaida	16,801,260	18,418,851	19,984,453	20,763,846
Malipo ya Riba Nje	1,151,376	1,140,366	1,271,596	1,409,006
Malipo ya Riba Ndani	1,561,637	1,770,159	2,687,549	2,975,899
Mishahara	6,912,184	7,927,932	8,058,743	8,191,712
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	1,247,149	1,655,652	1,673,036	1,690,603
Bidhaa/ Huduma/ Ruzuku	**5,928,914**	**5,924,741**	**6,293,528**	**6,496,625**
o/w Matumizi Mengineyo	**2,938,449**	**2,938,449**	**3,160,420**	**3,291,567**
Matumizi ya Maendeleo	**13,678,946**	**14,678,946**	**15,140,141**	**16,103,368**
Fedha za Ndani	10,723,023	11,635,464	11,905,595	12,850,362
Fedha za Nje	2,955,923	3,043,482	3,234,546	3,253,006
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	**-4,095,472**	**-4,529,937**	**-4,654,324**	**-4,301,754**
Misaada	**1,138,076**	**1,117,043**	**1,108,107**	**1,102,566**
Misaada ya Kibajeti	0	0	0	0
Misaada ya Maendeleo	1,138,076	1,117,043	1,108,107	1,102,566
Mifuko ya Kisekta	222,570	293,017	259,675	241,235
Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada	**-2,957,396**	**-3,412,894**	**-3,546,217**	**-3,199,188**
Jumla ya Nakisi	**-2,957,396**	**-3,412,894**	**-3,546,217**	**-3,199,188**
Kuziba Nakisi	**2,957,396**	**3,412,894**	**3,546,217**	**3,199,188**
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	**1,118,600**	**1,358,569**	**1,487,271**	**1,086,531**
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0	0	0	0
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,758,111	1,868,924	2,071,884	2,098,975
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	59,736	57,514	54,555	51,464
Mikopo ya Kibiashara	2,352,107	2,421,853	2,454,244	2,493,535
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-3,051,354	-2,989,724	-3,093,412	-3,557,444
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	**1,838,796**	**2,054,325**	**2,058,945**	**2,112,657**
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,150,337	3,300,000	3,050,000	3,100,000
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-3,150,337	-3,300,000	-3,050,000	-3,100,000
Pato la Taifa (Ghafi)	**165,165,614**	**175,781,352**	**188,019,106**	**200,782,111**

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

Jedwali Na. 3.2 Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa Katika Muda wa Kati

	2021/22 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)	16.0%	16.3%	16.2%	16.2%
Mapato ya Ndani	15.5%	15.7%	15.7%	15.7%
Mapato ya TRA (Kodi na Yasiyo Ya Kodi)	13.6%	13.8%	13.7%	13.8%
Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika)	1.8%	1.9%	1.9%	1.9%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
		0.0%	0.0%	0.0%
Jumla ya Matumizi	18.5%	18.8%	18.7%	18.4%
Matumizi ya Kawaida	10.2%	10.5%	10.6%	10.3%
Malipo ya Riba Nje	0.7%	0.6%	0.7%	0.7%
Malipo ya Riba Ndani	0.9%	1.0%	1.4%	1.5%
Mishahara	4.2%	4.5%	4.3%	4.1%
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	0.8%	0.9%	0.9%	0.8%
Bidhaa/ Huduma/ Ruzuku	3.6%	3.4%	3.3%	3.2%
o/w Matumizi Mengineyo	1.8%	1.7%	1.7%	1.6%
		0.0%	0.0%	0.0%
Matumizi ya Maendeleo	8.3%	8.4%	8.1%	8.0%
Fedha za Ndani	6.5%	6.6%	6.3%	6.4%
Fedha za Nje	1.8%	1.7%	1.7%	1.6%
		0.0%	0.0%	0.0%
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	-2.5%	-2.6%	-2.5%	-2.1%
		0.0%	0.0%	0.0%
Misaada	0.7%	0.6%	0.6%	0.5%
Misaada ya Kibajeti	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Misaada ya Maendeleo	0.7%	0.6%	0.6%	0.5%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.2%	0.1%	0.1%
		0.0%	0.0%	0.0%
Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada	-1.8%	-1.9%	-1.9%	-1.6%
		0.0%	0.0%	0.0%
Jumla ya Nakisi	-1.8%	-1.9%	-1.9%	-1.6%
Kuziba Nakisi	1.8%	1.9%	1.9%	1.6%
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	0.7%	0.8%	0.8%	0.5%
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1.1%	1.1%	1.1%	1.0%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Mikopo ya Kibiashara	1.4%	1.4%	1.3%	1.2%
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-1.8%	-1.7%	-1.6%	-1.8%
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	1.1%	1.2%	1.1%	1.1%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	1.9%	1.9%	1.6%	1.5%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-1.9%	-1.9%	-1.6%	-1.5%
Pato la Taifa (Ghafi)	**165,165,614**	**175,781,352**	**188,019,106**	**200,782,111**

Chanzo: *Wizara ya Fedha na Mipango*

Jedwali Na.3.3: Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati

Shilingi Milioni

	2021/22 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**36,681,898**	**39,387,521**	**41,268,006**	**43,524,658**
Mapato ya Ndani ikijumuisha Mapato ya Halmashauri	**26,384,735**	**28,567,860**	**30,470,270**	**32,565,460**
Mapato ya Ndani	25,520,877	27,630,809	29,513,331	31,571,105
Mapato ya Halmashauri	863,858	937,051	956,939	994,355
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0	0	0	0
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	2,673,617	2,692,950	2,920,316	2,960,307
Mifuko ya Kisekta	282,306	350,532	314,230	292,699
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,150,337	3,300,000	3,050,000	3,100,000
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	1,838,796	2,054,325	2,058,945	2,112,657
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	2,352,107	2,421,853	2,454,244	2,493,535
II. JUMLA YA MATUMIZI	**36,681,898**	**39,387,521**	**41,268,006**	**43,524,658**
MATUMIZI YA KAWAIDA	23,002,951	24,708,574	26,127,865	27,421,291
Mfuko Mkuu wa Serikali	10,699,563	11,421,611	12,358,275	13,333,115
Mishahara	8,150,509	9,139,108	9,368,996	9,521,024
Matumizi Mengineyo	2,938,449	2,938,449	3,160,420	3,291,567
MATUMIZI YA MAENDELEO	13,678,946	14,678,946	15,140,141	16,103,368
Fedha za Ndani	10,723,023	11,635,464	11,905,595	12,850,362
Fedha za Nje	2,955,923	3,043,482	3,234,546	3,253,006
Pato la Taifa (Ghafi)	**165,165,614**	**175,781,352**	**188,019,106**	**200,782,111**

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

Jedwali Na. 3.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa katika Muda wa Kati

	2021/22 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**22.2%**	**22.4%**	**21.9%**	**21.7%**
Mapato ya Ndani ikijumuisha Mapato ya Halmashauri	**16.0%**	**16.3%**	**16.2%**	**16.2%**
Mapato ya Ndani	15.5%	15.7%	15.7%	15.7%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	1.6%	1.5%	1.6%	1.5%
Mifuko ya Kisekta	0.2%	0.2%	0.2%	0.1%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	1.9%	1.9%	1.6%	1.5%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	1.1%	1.2%	1.1%	1.1%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	1.4%	1.4%	1.3%	1.2%
II. JUMLA YA MATUMIZI	**22.2%**	**22.4%**	**21.9%**	**21.7%**
MATUMIZI YA KAWAIDA	13.9%	14.1%	13.9%	13.7%
Mfuko Mkuu wa Serikali	6.5%	6.5%	6.6%	6.6%
Mishahara	4.9%	5.2%	5.0%	4.7%
Matumizi Mengineyo	1.8%	1.7%	1.7%	1.6%
MATUMIZI YA MAENDELEO	8.3%	8.4%	8.1%	8.0%
Fedha za Ndani	6.5%	6.6%	6.3%	6.4%
Fedha za Nje	1.8%	1.7%	1.7%	1.6%

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

Jedwali Na. 3.5: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Bajeti Yote katika Muda wa Kati

	2021/22 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2022/23 MAKADIRIO YA BAJETI	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**100.0%**	**100.0%**	**100.0%**	**100.0%**
Mapato ya Ndani ikijumuisha Mapato ya Halmashauri	**71.9%**	**72.5%**	**73.8%**	**74.8%**
Mapato ya Ndani	69.6%	70.2%	71.5%	72.5%
Mapato ya Halmashauri	2.4%	2.4%	2.3%	2.3%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	7.3%	6.8%	7.1%	6.8%
Mifuko ya Kisekta	0.8%	0.9%	0.8%	0.7%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	8.6%	8.4%	7.4%	7.1%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	5.0%	5.2%	5.0%	4.9%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	6.4%	6.1%	5.9%	5.7%
II. JUMLA YA MATUMIZI	**100.0%**	**100.0%**	**100.0%**	**100.0%**
MATUMIZI YA KAWAIDA	62.7%	62.7%	63.3%	63.0%
Mfuko Mkuu wa Serikali	29.2%	29.0%	29.9%	30.6%
Mishahara	22.2%	23.2%	22.7%	21.9%
Matumizi Mengineyo	8.0%	7.5%	7.7%	7.6%
MATUMIZI YA MAENDELEO	37.3%	37.3%	36.7%	37.0%
Fedha za Ndani	29.2%	29.5%	28.8%	29.5%
Fedha za Nje	8.1%	7.7%	7.8%	7.5%

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango*

Jedwali Na. 3.6: Mgawanyo wa Bajeti Kisekta katika Muda wa Kati

Shilingi Milioni

SEKTA	BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2021/22	MAKADIRIO 2022/23	MAKADIRIO 2023/24	MAKADIRIO 2024/25
1 - Elimu	**5,257,287**	**5,699,096**	**5,883,767**	**6,132,379**
1.1 - Elimu Msingi	4,043,374	4,383,169	4,525,199	4,716,406
1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi	137,565	149,125	153,957	160,463
1.3 - Elimu ya Juu	915,462	992,395	1,024,552	1,067,844
1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu	61,347	66,502	68,657	71,558
1.5 - Huduma za Utawala	99,540	107,905	111,401	116,108
2 - Afya	**2,019,188**	**2,188,875**	**2,259,802**	**2,355,288**
2.1 - Huduma za Tiba	824,226	893,492	922,444	961,421
2.2 - Huduma za Kinga	259,146	280,924	290,027	302,282
2.3 - Hospitali za Rufaa za Mikoa	2,606	2,825	2,916	3,039
2.4 - Zahanati	210,190	227,854	235,237	245,177
2.5 - Vituo vya Afya	221,004	239,576	247,339	257,790
2.6 - Hospitali za Wilaya	442,479	479,663	495,206	516,131
2.7 - Huduma za Utawala	59,538	64,541	66,632	69,448
3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali	**14,396,872**	**15,229,720**	**16,327,405**	**17,530,221**
3.1 - Mihimili	3,032,889	3,287,765	3,394,301	3,537,723
3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi	2,337,227	2,533,642	2,615,741	2,726,266
3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa	191,934	208,064	214,806	223,882
3.4 - Deni la Serikali	8,834,822	9,200,249	10,102,558	11,042,350
4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama	**3,532,718**	**3,829,599**	**3,953,692**	**4,120,750**
4.1 - Ulinzi	2,357,276	2,555,375	2,638,179	2,749,652
4.2 - Usalama wa Umma	931,752	1,010,054	1,042,784	1,086,845
4.3 - Mahakama	243,690	264,169	272,730	284,253
5 - Maendeleo ya Uchumi	**8,330,671**	**9,030,759**	**9,323,388**	**9,717,337**
5.1 - Kilimo	630,356	683,330	705,472	735,281
5.2 - Madini	66,728	72,336	74,680	77,835
5.3 - Nishati	2,385,946	2,586,455	2,670,265	2,783,094
5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	4,377,541	4,745,418	4,899,186	5,106,196
5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira	556,629	603,407	622,960	649,282
5.6 - Viwanda	82,513	89,447	92,345	96,247
5.7 - Biashara	209,366	226,961	234,315	244,216
5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi	21,591	23,406	24,164	25,185
6 - Hifadhi ya Jamii	**1,853,409**	**2,009,165**	**2,074,269**	**2,161,915**
6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu	38,363	41,587	42,935	44,749
6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	1,572,784	1,704,957	1,760,203	1,834,579
6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya	242,262	262,621	271,131	282,587
7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii	**1,291,752**	**1,400,308**	**1,445,683**	**1,506,769**
7.1 - Maji	706,207	765,554	790,361	823,757
7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu	104,203	112,960	116,620	121,548
7.3 - Maendeleo ya Jamii	426,603	462,454	477,439	497,613
7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni	54,739	59,340	61,262	63,851
Jumla	**36,681,898**	**39,387,521**	**41,268,006**	**43,524,658**

Chanzo: Wuzara ya Fedha na Mipango

SURA YA NNE

VIHATARISHI VYA UKUAJI WA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

4.1 Utangulizi

70. Sura hii inaainisha vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23. Aidha, inaainisha hatua ambazo Serikali itachukua ili kukabiliana na vihatarishi hivyo kwa kuzingatia Kifungu Na. 4 (2) (c) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439.

4.2 Vihatarishi vya ukuaji wa uchumi

71. Mwenendo chanya wa ukuaji wa shughuli za kiuchumi ni kichocheo cha ukuaji wa Pato la Taifa. Aidha, kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kina matokeo ya moja kwa moja kwenye utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Hata hivyo, mabadiliko hasi ya viashiria vya ukuaji wa uchumi huathiri mapato ya mtu mmoja mmoja, kampuni na Serikali kwa ujumla. Vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa uchumi ni pamoja na:

(i) Mfumuko wa bei;
(ii) Mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha;
(iii) Mabadiliko ya bei ya bidhaa na huduma katika soko la dunia;
(iv) Mdororo wa uchumi wa dunia;
(v) Migogoro ya kisiasa ya ndani na nje;
(vi) Vikwazo vya kiuchumi;
(vii) Mabadiliko ya viwango vya riba katika soko la fedha;
(viii) Mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili kama vile mafuriko, ukame, matetemeko, vimbunga, wadudu waharibifu wa mimea na mazao; na
(ix) Mlipuko wa magonjwa kama UVIKO – 19 n.k.

72. Baadhi ya athari ambazo zinaweza kujitokeza ni pamoja na: Kupungua kwa uzalishaji; kupungua kwa mapato ya Serikali; kuongezeka kwa gharama za bidhaa, malighafi, huduma na gharama za utekelezaji wa miradi; kupungua kwa faida na mapato ya kampuni na watu binafsi; kuongezeka kwa gharama za upatikanaji wa mitaji na uwekezaji; uharibifu wa mali na miundombinu; kuongezeka kwa gharama za usambazaji wa bidhaa, malighafi na huduma; na kupungua kwa ujuzi na nguvu kazi.

4.3 Vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali

73. Malengo na shabaha za Mpango na Bajeti ya Serikali ni kuchochea shughuli za kiuchumi na kuboresha huduma za jamii pamoja na ustawi wa watu. Kufikiwa

kwa malengo na shabaha za Mpango na Bajeti ni matokeo ya kufikiwa kwa misingi ya maoteo ya mapato na matumizi. Hata hivyo, vihatarishi vya mapato na matumizi vinaweza kujitokeza na kuathiri malengo na shabaha za Mpango na Bajeti ya Serikali. Vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ni pamoja na:

(i) Kudorora kwa shughuli za kiuchumi;
(ii) Uwiano wa mikopo ya masharti ya kibiashara dhidi ya masharti nafuu kuongezeka kutoka asilimia 8.9 hadi asilimia 44.5 katika kipindi cha muda wa miaka 10 iliyopita;
(iii) Kuongezeka kwa vitendo vya ukwepaji kodi na biashara za magendo;
(iv) Kuongezeka kwa sekta isiyo rasmi na biashara za mitandao;
(v) Uwepo wa walipa kodi na watumishi wasiozingatia sheria na kanuni za usimamizi wa kodi;
(vi) Mabadiliko ya viwango vya kodi, tozo na ada za huduma;
(vii) Kupungua kwa ukwasi katika soko;
(viii) Ufanisi mdogo wa Taasisi na Mashirika ya Umma;
(ix) Kuwepo kwa madeni sanjari;
(x) Mabadiliko ya sera za nje za misaada na mikopo;
(xi) Uhalifu wa kimtandao kwenye mifumo ya Serikali; na
(xii) Uharibifu na upotevu wa mali za Serikali.

74. Baadhi ya athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na: Kutofikiwa kwa makadirio ya mapato na matumizi; kusitishwa au kuahirishwa kwa baadhi ya miradi na programu za maendeleo; malimbikizo ya mashauri ya kodi; mabadiliko ya utumiaji wa bidhaa na huduma; kuongezeka kwa gharama za uuzaji, uagizaji na usafirishaji wa malighali, bidhaa na huduma; kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali, mikataba na mashauri ya kimahakama; kuongezeka kwa gharama za mikopo, dhamana na misaada; kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali; na uharibifu na upotevu wa mali na miundombinu ya Serikali.

4.4 Hatua za kukabiliana na vihatarishi

75. Ili kufikia malengo na shabaha za ukuaji wa uchumi pamoja na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2022/23, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Hatua hizo ni pamoja na:

(i) Kuimarisha mifumo ya kubaini vihatarishi vya shughuli za kiuchumi na kuchukua hatua stahiki za kisera na kiutawala kabla, wakati na baada ya mdororo wa kiuchumi kutokea;
(ii) Kujenga na kuimarisha uwezo wa Serikali katika kupambana na vitendo vya ukwepaji kodi, biashara za magendo na mifumo dhaifu ya usimamizi na udhibiti

wa mapato na matumizi ya Serikali (vitendea kazi, vifaa vya TEHAMA na ujuzi);

(iii) Kuboresha na kurahisisha mifumo ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi pamoja biashara za mitandao;

(iv) Kusimamia kwa weledi sera za fedha na bajeti ili kufikia malengo na shabaha za Mpango na Bajeti. Hatua hizo ni pamoja na: Kudhibiti mzunguko wa fedha kulingana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi; na kuweka sera rafiki za uwekezaji na biashara, hususan uzalishaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi, uvutiaji wa uwekezaji kutoka nje ya nchi na upanuzi wa biashara zilizopo;

(v) Kusimamia kwa weledi sheria za usimamizi wa kodi, hususan ukadiriaji na ukaguzi wa hesabu za walipakodi, elimu kwa mlipakodi na kuweka mifumo rafiki ya kushughulikia malalamiko ya walipakodi;

(vi) Kiwango cha nakisi ya bajeti kisizidi asilimia 3.0 ya pato la Taifa katika kipindi cha muda wa kati;

(vii) Kuelimisha na kuhamasisha matumizi ya mifumo ya mikataba ya uuzaji na ununuzi wa bidhaa na huduma (forward contracts) kutoka katika soko la ndani na nje;

(viii) Kupanua wigo wa Washirika wa Kibiashara na Maendeleo ili kupunguza athari za utegemezi wa wadau au washirika wachache;

(ix) Taasisi na Mashirika ya Umma kutoa taarifa za mwenendo wa mashauri yaliyopo mahakamani, ikiwa ni pamoja na dhamana chechefu ili madai husika yazingatiwe katika Mpango na Bajeti ya Serikali;

(x) Kuimarisha mifumo ya ndani ya usimamizi na udhibiti wa maadili na weledi wa watumishi wa umma ili kudhibiti matumizi na usalama wa mali na fedha za umma;

(xi) Kuimarisha uwezo wa Serikali wa kukabiliana na majanga ya asili na milipuko ya magonjwa;

(xii) Taasisi, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoingia miadi zaidi ya ukomo na kiwango cha juu kilichowekwa;

(xiii) Kuzingatia taarifa za tabianchi na majanga ya asili katika Mpango na Bajeti ya Serikali;

(xiv) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xv) Kuhamasisha ubunifu, matumizi ya teknolojia na ushirikishaji wa wadau katika uandaaji wa mipango ya Serikali;

(xvi) Kuimarisha akiba ya fedha za kigeni, usalama wa chakula na bidhaa za petroli; na

(xvii) Kulinda, kuimarisha na kudumisha amani, umoja, usalama, mshikamano na mahusiano ya kiuchumi na kisiasa ya ndani na nchi washirika.

SEHEMU YA PILI

MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

SURA YA KWANZA
MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

1.1. Utangulizi

76. Sura hii inatoa maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, uwasilishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23.

1.2. Uandaaji wa Mpango na Bajeti

77. Wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia vipaumbele vya Mipango ya Kitaifa, Sera na Miongozo iliyorejewa katika Mwongozo huu wa Mwaka 2022/23 pamoja na Sera na Mpango Mkakati wa taasisi husika. Aidha, wanapaswa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/21, mapitio ya nusu mwaka 2021/22 na kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza.

78. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya mipango ya maendeleo, mishahara na shughuli muhimu za uendeshaji wa ofisi ikiwemo umeme, maji, simu, ulinzi, usafi pamoja na kulipa madeni ya watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma kwa kuzingatia ukomo ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni, riba na faini.

79. Taasisi za Serikali zinazotarajia kupokea mikopo, misaada na dhamana zitapaswa kupata idhini kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha, kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134.

1.3. Uzingatiaji wa Masuala ya Muungano

80. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Umma zinaelekezwa kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ikijumuisha:

(i) Kuendelea kufanya vikao vya ushirikiano kwa lengo la kuimarisha Muungano;
(ii) Kuendeleza majadiliano ya kutafuta ufumbuzi wa hoja za mashirikiano na Muungano ambazo hazijapatiwa majibu; na
(iii) Kuimarisha hatua za uandaaji, utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara/Taasisi za Muungano.

1.4 Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

81. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwasilisha Muundo wa Mapato na Matumizi OR-TAMISEMI; na Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina wiki ya pili ya Januari, 2022 kabla ya kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa mpango na bajeti ambayo ni shirikishi kwa kuzingatia Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Mawasilisho hayo yanatakiwa kufanyika wiki ya tatu ya Januari, 2022 baada ya kuidhinishwa katika ngazi za maamuzi husika ikijumuisha Mabaraza ya Madiwani na Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura 105.

1.4.1 Kamati za Bajeti

82. Katika maandalizi na utekelezaji wa Bajeti za Mafungu kwa mwaka 2022/23, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa:

(i) Kamati za Bajeti zinaundwa na zinafanya kazi kwa mujibu wa Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti Sura 439; na

(ii) Taarifa ya utekelezaji wa Kamati za Bajeti kuhusu maandalizi na ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa kila mwezi wakati wa utekelezaji wa bajeti ijumuishwe katika Taarifa za Utekelezaji za robo mwaka na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango.

1.4.2 Maandalizi ya Makadirio na Mgawanyo wa Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

83. Wakati wa kuandaa makadirio ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2022/23, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutambua na kutenganisha vyanzo vyote vya mapato katika makundi ya vyanzo vinavyolindwa kama vile ada za shule, michango ya wananchi ya chakula cha watoto shuleni, iCHF, TIKA, NHIF, mapato yanayotokana na taka ngumu na malipo ya papo kwa papo na vyanzo visivyolindwa ;

(ii) Kutenganisha na kuhasibu michango ya nguvu za wananchi kwenye vyanzo vya mapato ya ndani;

(iii) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa shilingi bilioni tano au zaidi zinaelekezwa kutenga asilimia 60 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ikijumuisha asilimia 10 kwa ajili ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na asilimia 10 ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA;

(iv) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa chini ya shilingi bilioni tano zinaelekezwa kutenga asilimia 40 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

ikijumuisha asilimia 10 kwa ajili ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu;

(v) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, asilimia 60 ya kiasi hicho kielekezwe kwenye miradi yenye tija itakayozalisha ajira; na

(vi) Halmashauri zinazopokea mapato mengine kama vile michango ya kijamii (*Corporate Social Responsibility*) na fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo zihakikishe mapato hayo yanajumuishwa kwenye bajeti kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

1.4.3 Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara

84. Wakati wa kuandaa ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka 2022/23, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuzingatia Mwongozo wa Katibu Mkuu (UTUMISHI) kuhusu uandaaji wa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa Mwaka 2022/23;

(ii) Kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2021 kuhusu Matumizi ya Mfumo Mpya wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali watu na Mishahara (New HCMIS);

(iii) Kuhakikisha maslahi ya watumishi wa umma ikiwemo upandishaji vyeo unazingatia bajeti, ikama na Miundo ya Maendeleo ya Utumishi na Kanuni D.51 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Mwaka 2009;

(iv) Kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 2015 na Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 6 wa Mwaka 2015 kuhusu Marekebisho ya Mishahara kwa watumishi wa Umma na Taasisi za Serikali; na

(v) Kujumuisha makisio ya nyongeza za mwaka za mishahara (annual increment) katika bajeti ya mishahara kwa mwaka 2022/23.

1.5 Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti

(a) Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo

85. Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea kutekelezwa inatengewa fedha kwa ajili ya kuikamilisha kabla ya kuanza miradi mipya;

(ii) Wizara za Kisekta ambazo zinaratibu miradi na programu zinazoshirikisha utekelezaji wa Mafungu mengine kuhakikisha bajeti za miradi na programu zinazohusu Mafungu hayo zinatengwa kwenye Mafungu husika;

(iii) Kuzingatia Mwongozo wa Uandaaji Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na Upokeaji wa Misaada wa mwaka 2020;

(iv) Kuzingatia Sheria ya Kodi ya Ongozeko la Thamani (VAT), Sura 148 na kanuni zake kuhusu Utaratibu wa Kutoa Msamaha wa VAT kwa Miradi inayotekelezwa kwa Fedha za Serikali na za Washirika wa Maendeleo;

(v) Kuhakikisha misamaha ya kodi inayotolewa katika miradi ya maendeleo inatumika ipasavyo ili kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha hiyo;

(vi) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka 2020/21 kuhusu Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS);

(vii) Kuzingatia Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 21(1-3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015 (Marekebisho yake ya Mwaka 2021), kinachoelekeza kuhusu uombaji wa idhini ya kuvusha matumizi ya fedha kwa mwaka unaofuata ifikapo tarehe 30 Juni kila mwaka.

(b) Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

86. Katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ya kimkakati. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti ya miradi husika kwa ajili ya ukamilishaji ili kufikia malengo tarajiwa na kuzingatia thamani ya fedha. Aidha, marekebisho yoyote ya gharama ya mradi wa kimkakati yafanyike baada ya kupata ridhaa za OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango. Vilevile, uendeshaji wa miradi iliyokamilika isimamiwe kwa kutumia wataalam/Kampuni ya uendeshaji.

(c) Ugharamiaji wa Miradi Kupitia Fedha za Nje

87. Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo itaendelea kutekeleza na kugharamia programu na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo. Hivyo, katika kuandaa bajeti ya miradi inayogharamiwa na fedha za nje, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutoingia Mikataba ya Makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha kwa mujibu wa Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134;

(ii) Kuwasilisha maoteo ya bajeti za Mafungu yanayonufaika na Mifuko ya Pamoja ya Kisekta (kwa Wizara zinazoratibu Mifuko ya Pamoja ya Kisekta) Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya tarehe 20 Januari, 2022 ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za Mafungu;

(iii) Kuwasilisha takwimu za ahadi za fedha za nje Wizara ya Fedha na Mipango wiki ya nne ya Januari, 2022 ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za Mafungu; na

(iv) Kutenga counterpart fund katika miradi ya maendeleo yenye masharti hayo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo katika mwaka husika.

(d) Usimamizi wa Fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (D – Fund)

88. Katika usimamizi wa fedha za Misaada au Mikopo zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo moja kwa moja katika Mafungu kwa ajili ya kutekeleza

miradi ya maendeleo (*D- Fund*), Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia:

(i) Matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha Zinazopelekwa Moja kwa Moja kwenye Miradi (*D – Fund Management Information System*); na

(ii) Maelekezo ya Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019 kuhusu Utaratibu wa Kuomba na Kuhamisha Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwenda Moja kwa Moja kwenye Miradi ya Maendeleo (*Direct to Project Funds*).

(e) Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

89. Maafisa Masuuli wanaokusudia kutekeleza miradi kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 7 wa Mwaka 2020/21 kuhusu utekelezaji wa miradi ya Ubia Baina ya Sekta za Umma na Binafsi (PPP);

(ii) Kuanzisha dawati la PPP katika Wizara, litakalowajibika kuratibu utelekezaji wa miradi ya PPP inayoibuliwa kutoka kwenye Wizara husika, na Taasisi na Idara zilizo chini ya Wizara hiyo;

(iii) Kuwajengea uwezo maafisa dawati na wengineo wanaohusika na utekelezaji wa programu ya PPP kwenye sekta husika;

(iv) Kuibua na kuandaa miradi ya ubia yenye manufaa kwa Taifa, gharama nafuu kwa Serikali na watumiaji, na yenye kuhakikisha vihatarishi vinashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 na Kanuni zake za mwaka 2020;

(v) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango Andiko Dhana la mradi au Upembuzi Yakinifu wa Awali wa miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP kila mwanzo wa mzunguko wa bajeti, baada ya kuidhinishwa na Waziri anayesimamia sekta husika kwa kuzingatia Kifungu cha 4 (6) (a)-(b) cha Sheria ya PPP, Sura 103; na Kifungu cha 7 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439;

(vi) Kupokea na kuchambua maandiko ya Upembuzi Yakinifu wa Awali wa miradi iliyoibuliwa na wabia kutoka Sekta Binafsi (Unsolicited Proposals) kwa kuzingatia kikamilifu Kanuni za PPP, 2020;

(vii) Kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya miradi ya PPP ikiwemo taarifa za Upembuzi Yakinifu na/au gharama za Mshauri Elekezi; na

(viii) Kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma unaotaka miradi ya kibiashara na yenye kuvutia sekta binafsi kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

(f) Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint):

90. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kutekeleza mipango mbalimbali ikiwemo Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara. Maboresho hayo yatajumuisha: kuwianisha kodi na tozo;

miundombinu ya reli, barabara, nishati, viwanja vya ndege na bandari; ununuzi na ukarabati wa meli za abiria na mizigo; ununuzi na ukarabati wa vivuko; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; kuongeza wigo wa Mkongo wa Taifa; kuharakisha uondoaji wa mizigo bandarini; na kuendelea kuimarisha mahusiano na sekta binafsi. Hivyo, Maafisa Masuuli husika wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuondoa muingiliano wa majukumu ya kitaasisi ikiwemo mabaraza ili kurahisisha utoaji huduma;

(ii) Kukamilisha kanuni za udhibiti wa Sekta binafsi ili kuwezesha mazingira bora ya ufanyaji biashara na yenye kuleta ushindani sawa; na

(iii) Kuendelea kutekeleza *Blueprint* kwa kuboresha sheria mbalimbali ili kuweka misingi mizuri ya kusimamia mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

(g) Uchumi wa Rasilimali za Maji

91. Serikali inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mkakati wa Uchumi wa Rasilimali za Maji (Blue economy). Shughuli mahususi zinazotekelezwa katika Uchumi wa Rasilimali za Maji ni uvuvi, ukuzaji viumbe maji,utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, nishati jadidifu, utalii, kilimo, usafiri na usafirishaji na uvunaji wa madini. Aidha, mifumo imara ya ulinzi na usalama ni muhimu katika kuvutia uwekezaji wa rasilimali za maji. Hivyo, katika utekelezaji wa Mpango huu, Serikali itaweka mazingira wezeshi ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta hii kwenye uchumi. Maafisa Masuuli wa sekta husika (Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Uvuvi, Mambo ya Ndani, Ulinzi, Utalii, Nishati, Madini, Maji na Uchukuzi) wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya:

(i) Kuendelea kuwezesha tafiti ili kubaini fursa za rasilimali za maji;

(ii) Kuhamasisha uwekezaji na matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za kiuchumi za rasilimali za maji;

(iii) Kuimarisha na kufungamanisha miundombinu ya utafiti, uwekezaji, uzalishaji, utunzaji, utalii na usafirishaji wa bidhaa na huduma za majini;

(iv) Kuhamasisha ushirikishwaji wa wananchi katika fursa za kiuchumi zinazotokana na rasilimali za maji;

(v) Kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama wa shughuli na huduma za majini; na

(vi) Kuimarisha ushirikiano na taasisi za kikanda na kimataifa katika usimamzi wa rasilimali za maji.

(h) Mikakati ya Mapambano Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Nchini

92. Serikali inaendelea kuchukua hatua za kushughulikia tatizo la Rushwa ikiwemo kuandaa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne ambao ni

mwendelezo wa jitihada za kukabiliana na rushwa. Maafisa Masuuli wanasisitizwa kuendelea kutenga bajeti ya utekelezaji wa Mikakati ya Mapambano Dhidi ya Rushwa nchini.

(i) Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu

93. Serikali inaendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PSRP III, 2021 – 2026). Katika kutekeleza Programu hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya:

(i) Kuwajengea uwezo viongozi na watumishi wa ngazi zote Serikalini;
(ii) Kuweka misingi itakayoimarisha uwajibikaji;
(iii) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu kwa kuboresha taratibu za ajira, uteuzi, upandishaji vyeo na muda wa matazamio kwa kuzingatia sifa na vigezo;
(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya maendeleo, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Serikali; na
(v) Kufanya utafiti kabla ya kuandaa au kuhuisha Sera na mipango.

(j) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili

94. Katika kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II, 2017 - 2028) katika maeneo ya vipaumbele yafuatayo;

(i) Kusimamia matumizi endelevu ya maji na ardhi;
(ii) Kuongeza tija na faida kwenye kilimo, mifugo na uvuvi;
(iii) Kuimarisha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuleta ushindani kwenye soko; na
(iv) Kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji wa kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

(k) Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

95. Katika kutekeleza Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali inalenga kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Maafisa Masuuli wa Wizara ambazo zina watumishi katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuendelea kutekeleza ugatuaji wa madaraka kisiasa, kifedha, kiutawala na kuimarisha mahusiano ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;
(ii) Kuwajengea uwezo watumishi waliopo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye maeneo ya uratibu, utawala bora, usimamizi wa fedha, mpango na bajeti, uandaaji wa maandiko ya miradi ya

maendeleo, elimu ya uraia, ufuatiliaji na tathmini, na usimamizi wa miradi ili kuboresha huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kuweka mazingira wezeshi ya kuboresha shughuli za kiuchumi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(iv) Kuimarisha ushiriki wa jamii katika utekelezaji na utoaji wa maamuzi kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(l) Uendelezaji wa Sekta ya Fedha

96. Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha pamoja na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa rasilimali fedha kwenye shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi, Serikali inaendelea kutekeleza sera, sheria na mikakati mbalimbali ili kujenga mfumo thabiti katika sekta ya fedha. Maafisa Masuuli husika wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/21 - 2029/30) na kuujumuisha katika Mpango na Bajeti wa Fungu husika;

(ii) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika usambazaji wa huduma na bidhaa za fedha kwa wananchi katika sekta ya fedha;

(iii) Kuendelea kutoa elimu ya fedha kwa umma kuhusu: utoaji na upatikanaji wa huduma za fedha nchini; upatikanaji na matumizi ya masoko ya mitaji na dhamana; soko la bidhaa; na fursa zilizopo katika taasisi za fedha za maendeleo;

(iv) Kuhakikisha kuwa mipango na bajeti za Mikoa na Halmashauri inajumuisha masuala ya huduma za fedha ikiwa ni pamoja na kuhuisha sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuboresha taratibu za usajili wa hati miliki za ardhi na mali ili kuwawezesha wananchi kutumia hati miliki kama dhamana za mikopo katika benki, taasisi za fedha na watoa huduma ndogo za fedha;

(vi) Kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vya fedha vya kijamii na kusaidia kuviunganisha na watoaji wengine wa huduma za fedha;

(vii) Kuendelea kutumia fursa zitokanazo na soko la Bidhaa (Tanzania Mercantile Exchange- TMX) kwenye mazao ya kilimo na bidhaa nyingine pamoja na kuboresha mifumo ya mauzo kwa njia ya kielectroniki na kushirikiana na Taasisi nyingine za masoko ili kupanua wigo wa masoko hasa ya nje ya nchi ili kuongeza ushindani na hivyo kupata bei nzuri kwa mazao na bidhaa za Tanzania; na

(viii) Kutumia fursa zitokanazo na Mkakakati wa Serikali wa ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa njia mbadala (Alternative Project Financing-APF). Mkakati huu unalenga kutoa nafasi kwa MDAs, RSs na LGAs kufaidika na fursa zitokanazo na Sekta ya Fedha kwa kugharamia miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara kwa kutumia njia mbadala kama vile mikopo, hisa,

hatifungani, ubia baina ya sekta ya umma na binafsi na nyinginezo.

(m) Usimamizi wa Mali za Umma

97. Katika kuimarisha usimamizi wa mali za umma kwa kuzingatia: Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019; Waraka wa Hazina Na. 2 wa mwaka 2021/22 kuhusu Usimamizi wa Mali za Serikali kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki *(*GAMIS*)* na Waraka wa Hazina Na.7 wa Mwaka 2018/19 kuhusu Utaratibu wa Umiliki wa Magari na Mali zinazotumika kwenye Miradi inayogharamiwa na Serikali na Fedha za Washirika wa Maendeleo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutumia Mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Mali za Serikali *(*GAMIS*)* katika kusimamia mali baada ya upatikanaji wake hadi kuondoshwa kwake;

(ii) Kuandaa na kuhuisha taarifa za mali katika Daftari la Mali lililopo kwenye mfumo wa GAMIS (Electronic Asset Register) kwa kuzingatia muundo uliopo kwenye mfumo huo kulingana na kundi husika la mali (asset classes) ili kuwa na kumbukumbu sahihi za mali;

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kupima, kuweka alama na kurasimisha maeneo ya ardhi yanayomilikiwa na Serikali ikijumuisha mashamba, viwanja, shule/vyuo, vituo vya kutolea huduma za afya na ofisi za taasisi za Umma pamoja na kudhibiti usalama na ulinzi wa mali za umma;

(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya mali za Serikali kulingana na Mpango wa Matengenezo wa Mali (Asset Maintenance Plan);

(v) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango orodha ya mali, nyaraka za umiliki na mali husika zinazotokana na miradi inayogharamiwa na Serikali pamoja na Washirika wa Maendeleo baada ya miradi kukamilika na mali zilizotaifishwa au kutelekezwa; na

(vi) Kuhuisha muda wa uhai wa mali uliobaki (Estimated Remaining Economic Life - EREL) kwa lengo la kuipa thamani na kuiwezesha mali kuendelea kutoa huduma iliyokusudiwa kwenye Taasisi.

(n) Mifumo ya Kielektroniki ya Ukusanyaji wa Mapato na Ulipaji Serikalini

98. Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 pamoja na Kanuni za GePG za mwaka 2019 zinaelekeza matumizi ya Mfumo wa GePG katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha mapato yote katika Taasisi za Umma yanaendelea kukusanywa kupitia Mfumo wa GePG.

99. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha Taasisi zao zinatumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) kwa mujibu wa Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka 2019 kuhusu Uanzishaji na Utumiaji wa Mifumo ya Kieletroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(o) Hatua za Kudhibiti Matumizi

100. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma ili kuongeza tija na kupata thamani ya fedha. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 pamoja na Kanuni zake katika usimamizi wa fedha za umma;

(ii) Kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja na Kanuni zake kwa kufanya ununuzi wa pamoja na kutumia Mwongozo wa Matumizi ya Force Account wa Mei, 2020 ili kupata thamani halisi ya fedha;

(iii) Kuzingatia maelekezo kuhusu maandalizi na utekelezaji wa ujenzi wa Ofisi za Wizara Awamu ya Pili katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma yaliyotolewa kupitia barua Kumb.Na. 1/CAB.2/341/01 ya tarehe 29 Julai, 2021 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha tathmini na mtiririko wa mahitaji ya fedha za ujenzi;

(iv) Kutoingia mikataba bila kuwa na bajeti ili kuepuka malimbikizo ya madai kwa kuzingatia Mwongozo Kuhusu Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

(v) Kuendelea na utaratibu wa kutumia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kwenye ununuzi wa magari baada ya kupata ushauri wa kiufundi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) na kibali cha ununuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(vi) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi;

(vii) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali na kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika usimamizi wa mifumo ili kupunguza gharama;

(viii) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa Mwaka 2019 kuhusu Uanzishaji na Utumiaji wa Mifumo ya Kieletroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika ununuzi, uandaaji na usimikaji wa mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa fedha za Umma ili kuondoa urudufu wa mifumo;

(ix) Kuepuka uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi iwapo zinazalishwa na kupatikana nchini;

(x) Kuingia mikataba na watoa huduma wa ndani kwa kutumia Shilingi ya Tanzania ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha;

(xi) Taasisi zinazojenga miundombinu zizingatie ushirikishwaji wa wadau husika wakati wa upangaji na utekelezaji wa miradi; na

(xii) Kutumia vifaa vyenye teknolojia inayopunguza matumizi ya nishati.

(p) Ulipaji na Udhibiti wa Uzalishaji na Ulimbikizaji wa Madeni

101. Katika kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni Maafisa Masuuli

wanaelekezwa kuzingatia maelekezo ya kifungu cha 52(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kikamilifu na kusimamia Mkakati wa Kudhibiti Madeni kwa:

(i) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 4 wa Mwaka 2014/15, Waraka wa Hazina Na.1 wa Mwaka 2018/19 na Waraka wa Hazina Na. 3 wa Mwaka 2019 kuhusu Uzuiaji, Udhibiti na Ulipaji wa Madeni ya Serikali;
(ii) Kutoingia mikataba ya utekelezaji wa shughuli za Serikali bila kuwa na bajeti;
(iii) Kutenga bajeti na fedha kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa;
(iv) Kufanya uhakiki wa madeni kupitia Mkaguzi wa Ndani wa Fungu husika kabla ya kuingizwa katika Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Madai na Madeni ya Serikali (Government Arrears Management System – GAMS) na kutunza kumbukumbu na nyaraka/vielelezo vya madeni;
(v) Kuwasilisha madeni kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki; na
(vi) Kuhakikisha Hati za Madai zinazotakiwa kulipwa ndani ya siku 28, maombi ya fedha yanawasilishwa Hazina siku 16 kabla. Aidha, kwa Hati za Madai zinazotakiwa kulipwa ndani ya siku 56 maombi yawasilishwe Hazina siku 28 kabla.

(q) Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

102. Makadirio yote ambayo yanatumia fedha za kigeni, yatumie kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha za kigeni cha Dola Moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,326.1 katika kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23.

(r) Masuala Mtambuka katika Mpango na Bajeti

103. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mtambuka ikiwemo Jinsia, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, utawala bora, madawa ya kulevya, UKIMWI na Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU), Lishe pamoja na Watu Wenye Ulemavu na Wazee. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu (2008), pamoja na masuala ya Jinsia, VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa;
(ii) Kujenga au kukarabati miundombinu ya majengo ili yawe rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee;
(iii) Kuzingatia Mwongozo wa Udhibiti wa Ugonjwa wa Korona (UVIKO – 19) kupitia afua ya kudhibiti misongamano katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi;
(iv) Kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA);
(v) Kutekeleza Mkakati wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee (2018/19 – 2022/23);
(vi) Kutekeleza mkakati wa kukabiliana na changamoto ya lishe duni/utapiamlo

nchini kwa kutekeleza Mpango wa Pili Jumuishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP – II) wa mwaka 2021/22 – 2025/26;

(vii) Kuzingatia miongozo kuhusu madawa ya kulevya ili kudhibiti matumizi na athari zake kwa vijana; na

(viii) Kuendelea kuzingatia utekelezaji wa shughuli za hifadhi ya Mazingira katika maeneo yao kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004.

(s) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

104. Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kutekeleza makubaliano, itifaki na mikataba iliyoridhiwa katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia masuala ya ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mashirika ya Kimataifa pamoja na masuala mengine ya mtangamano katika Mpango na Bajeti za Mafungu;

(ii) Kuainisha na kutumia fursa zinazopatikana kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kukuza uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu;

(iii) Kuwasilisha makadirio ya michango ya uanachama ya Kikanda na Kimataifa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujumuishwa na kutengewa bajeti pamoja na kufuatilia nyaraka muhimu baada ya malipo; na

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) kama ilivyoainishwa katika Mpango Kazi (API-DCF) wa mwongozo huo.

1.6 Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma

105. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kuboresha utendaji na usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuongeza ufanisi na tija kwenye utoaji huduma na michango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika kufikia azma hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutumia mifumo ya kielektroniki ya OTRMIS, MUSE, GePG na PlanRep katika kuhuisha taarifa za Bodi za Wakurugenzi na kuingiza taarifa za fedha, matumizi na uandaaji wa taarifa za kiuhasibu, makusanyo ya mapato na uandaaji wa Mpango na Bajeti mtawalia;

(ii) Kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kutenga na kuwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi na asilimia 70 ya ziada ya mapato baada ya kutoa matumizi yaliyoidhinishwa;

(iii) Kutumia geresho la kibajeti (GFS Code 2014) 28211124 - Contribution to Consolidated Fund wakati wa kuingiza takwimu za michango itakayowasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali;

(iv) Kuandaa na kuwasilisha Mikakati ya Uwekezaji, sera ya gawio (dividend policy) na Mipango ya Biashara katika Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupata idhini;

(v) Kuingia Mkataba wa Utendaji Kazi pamoja na kuwasilisha utekelezaji wa Mikataba kila robo mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina; na

(vi) Kubuni mikakati endelevu ya kuongeza ufanisi ikiwemo kutumia njia mbadala za kutafuta mitaji (alternative sources of financing).

1.7 Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

1.7.1 Sekretarieti za Mikoa

106. Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kutekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kuendelea kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo ya utawala;

(ii) Kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na uwazi kwa kufanya Vikao vya Ushauri vya Wilaya na Mikoa pamoja na Vikao vya Kamati za Usalama za Wilaya na Mikoa;

(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa katika Mikoa na Halmashauri na Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto;

(iv) Kuendelea kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Mikoa, Wilaya na Tarafa;

(v) Kuendelea kutekeleza maelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Ilani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kuzingatia Mipango Mkakati ya Mikoa iliyohuishwa na Mwongozo wa Fursa na Vikwazo vya Maendeleo Ulioboreshwa mwaka 2019;

(vi) Kutumia na kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA ikiwemo mifumo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi, Mipango na Bajeti na uwekaji wa taarifa katika Tovuti za Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri;

(vii) Kuzingatia matumizi sahihi ya takwimu za kibajeti wakati wa kuingiza kwenye Mfumo wa CBMS, fedha za ruzuku ya uendeshaji wa kisekta katika Serikali za Mitaa kwa kutumia vifungu maalum vilivyoainishwa kwa ajili ya fedha za mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo;

(viii) Kusimamia utekelezaji wa Kamati za Bajeti kuhusu maandalizi na ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa kila mwezi wakati wa utekelezaji wa bajeti na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji za robo mwaka Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(ix) Kutenga fedha za ujenzi, ukamilishaji, ukarabati na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ofisi na makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa;

(x) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa Sekretarieti za

Mikoa ili kutoa ushauri wa kitaalam kwa watumishi wa Serikali za Mitaa;

(xi) Kutenga fedha za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xii) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za huduma ndogo za fedha katika ngazi ya Mkoa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2017 na Mkakati wa Utekelezaji wake pamoja na Sheria ya Huduma ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018;

(xiii) Kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kubuni, kuandaa maandiko ya miradi kwa kutumia Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (2021) ikiwa ni pamoja na miradi ya ubia kati ya Sekta za Umma na Binafsi;

(xiv) Kusimamia miradi na ukusanyaji wa mapato katika miradi inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha miradi ya TARURA;

(xv) Kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda;

(xvi) Kusimamia utekelezaji wa malengo ya Programu ya Uimarishaji wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (2021 - 2031);

(xvii) Kupitia na kuridhia maombi ya ahadi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayopendekezwa kutekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO's) kwenye maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(xviii) Kuratibu na kuzisimamia Halmashauri kuhusu ufanikishaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

1.7.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa

107. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Masuuli wanapaswa kutekeleza maelekezo yafuatayo:

A. Maelekezo ya jumla

(i) Kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama;

(ii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika maeneo ya utawala kwa kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto na kuwezesha kufanyika kwa vikao vya kisheria vya Kamati za Maendeleo za Kata na mikutano ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji;

(iii) Kupitia, kurekebisha na kutunga Sheria Ndogo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na Utawala Bora;

(iv) Kutumia Mpango Mkakati wa Halmashauri uliohuishwa, Mwongozo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa mwaka 2019, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 katika kuainisha vipaumbele vya maendeleo na kujumuishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;

(v) Kutumia mifumo ya TEHAMA ikiwemo mifumo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi, Mipango na Bajeti, utoaji na uwekaji wa taarifa za Umma katika Tovuti za Halmashauri;

(vi) Kuhakikisha Kamati za Bajeti zinaandaa na kusimamia mpango na bajeti, ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa kila mwezi na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kila robo mwaka kwa Sekretarieti za Mikoa kwa mujibu wa Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Aidha, muhtasari wa kikao cha mgao wa kila mwezi uwasilishwe HAZINA na nakala OR – TAMISEMI na utakuwa ni kigezo cha kutengewa fedha kwa mwezi unaofuata;

(vii) Kuandaa mipango na makadirio ya mapato na matumizi ya vituo vya kutolea huduma kama shule, vituo vya afya, zahanati, hospitali na Vijiji/Mitaa na kuijumuisha kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;

(viii) Kutenga fedha za ujenzi, ukamilishaji, ukarabati na ununuzi wa samani kwa ajili ya majengo ya utawala na nyumba za viongozi wa Halmashauri, Ofisi za Kata na Vijiji/Mitaa;

(ix) Kutenga fedha kutoka makusanyo ya mapato ya ndani ikiwa ni sehemu ya fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(x) Kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa viuadudu ili kutokomeza mazalia ya mbu;

(xi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutatua migogoro, kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji pamoja na maeneo ya hifadhi;

(xii) Kutenga kiasi kisichopungua shilingi 200,000 kila robo mwaka kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kila Kijiji/Mtaa. Aidha, kwa Halmashauri zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni moja zinaelekezwa kutenga kiasi cha shilingi 100,000 kwa kila robo mwaka kwa Kijiji/Mtaa;

(xiii) Kuendelea kutenga na kuweka fedha kwenye akaunti ya mikopo kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu na kufungua akaunti kwa ajili ya marejesho ya mikopo hiyo pamoja na kutoa taarifa za utekelezaji;

(xiv) Kutenga fedha za ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mujibu wa marekebisho ya kanuni za utoaji na usimamizi wa Mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2021;

(xv) Kutenga fedha kwa ajili ya marejesho ya mikopo na michango ya wanachama kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na ALAT;

(xvi) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa vikundi vya Watu Wenye Ulemavu, Vijana na Wanawake;

(xvii) Kubuni na kuandaa maandiko ya miradi kwa kutumia Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (2021) ikiwa ni pamoja na miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi;

(xviii) Kutekeleza Mwongozo wa OR -TAMISEMI wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa uliotolewa Machi, 2018;

(xix) Kuwezesha mazingira rafiki ya kibiashara kwa kuzingatia Mkakati wa Kuboresha Mazingira Wezeshi ya Biashara Nchini wa Mwaka 2018;

(xx) Kuendelea kuboresha huduma ndogo za fedha kwa kuimarisha Kamati za Usimamizi katika usajili, kujenga uwezo wa vikundi vya fedha vya kijamii pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini;

(xxi) Kutenga maeneo na kuweka miundombinu wezeshi kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo (Wamachinga) na kuwapatia elimu ya biashara na ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za fedha na masoko ili kukuza fursa za ajira na uchumi wa maeneo husika;

(xxii) Kuimarisha mifumo ya uratibu, utekelezaji na usimamizi wa maafa ikiwa ni pamoja na usimamizi wa utekelezaji wa Muundo wa Usimamizi wa Maafa; kuzijengea uwezo na kuhakikisha Kamati za Maafa katika ngazi zote za Serikali zinaandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango na mikakati ya kukabiliana na maafa kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004, Mwongozo wa Taifa wa Menejimenti ya Maafa 2014 na Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2015;

(xxiii) Kuwasilisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa ahadi za fedha na miradi inayopendekezwa kutekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO's);

(xxiv) Kutenga bajeti kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi, makazi na biashara na kutoa taarifa ya utekelezaji kila robo mwaka;

(xxv) Kuzingatia Kifungu cha 41 cha Sheria ya Bajeti Sura 439, taratibu na miongozo wakati wa kuomba kibali cha kubadili matumizi ya fedha endapo mradi umekamilika na fedha zimebaki katika mradi huo au kuna sababu za kubadili matumizi ya fedha za mradi huo ili kutekeleza mradi mwingine wenye tija zaidi. Aidha, maombi hayo yawasilishwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwa ajili ya kuomba kibali kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kutoa taarifa OR-TAMISEMI. Vilevile, kubadili eneo la utekelezaji wa mradi maombi yawasilishwe kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa;

(xxvi) Kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi yote ikijumuisha fedha zinazopokelewa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na fedha za mapato ya ndani zinazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinabandikwa kwenye ubao wa matangazo na kuchapishwa katika tovuti husika;

(xxvii) Kutoa kipaumbele katika uzingatiaji wa masuala ya uchumi wa buluu na uchumi wa kidigitali katika bajeti kwa sekta husika; na

(xxviii) Kuhakikisha miradi inayoanzishwa na wananchi inapatiwa ushauri wa

kitaalamu kabla ya kuanza kutekelezwa.

B. Maelekezo kuhusu Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Ardhi na Mazingira

(i) Kuboresha huduma za afya na lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya huduma za afya kwa kutenga bajeti ya uratibu, usimamizi na kujenga uwezo kuhusu masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe;

(ii) Kuboresha huduma za afya kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya na kuviwekea vifaa na vifaa tiba na dawa; kuimarisha Bodi za afya za Halmashauri, Timu ya Uendeshaji wa Shughuli za Afya ngazi ya Wilaya, kamati za vituo vya afya, zahanati na huduma za rufaa; huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za chanjo; kudhibiti magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza, huduma za tiba asili na tiba mbadala; na kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya (NHIF), Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) na mifuko mingine inayotoa huduma za bima na Afya;

(iii) Kuwatambua, kuwasajili na kuwatengamanisha na huduma watoto walio katika mazingira hatarishi wakiwemo wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wazee na watu wenye mahitaji maalum na kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa mashauri ya watoto walio katika mazingira hatarishi;

(iv) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kupitia OR-TAMISEMI takwimu zenye uhalisia za Elimu kulingana na Mahitaji ya bajeti zikijumuisha idadi ya Wanafunzi walioandikishwa kuingia Elimumsingi, idadi ya Wanafunzi; Shule za awali, Msingi, Sekondari, Shule za bweni, Maafisa Elimu Kata pamoja na shule mpya zinazostahili kupatiwa vibali vya usajili ifikapo tarehe 30 Januari, 2022 ili kuwezesha utengaji wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Elimumsingi bila Malipo;

(v) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule; kuwezesha michezo shuleni; kuwapatia nyenzo na vifaa wanafunzi wenye mahitaji maalum; kuimarisha masuala ya malezi na makuzi, unasihi, usalama wa mtoto, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na nyumbani na kuandaa mikakati ya kushirikisha jamii katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula shuleni;

(vi) Kutambua na kuendeleza bunifu katika teknolojia kwa ajili ya kuziendeleza na kuboresha huduma;

(vii) Kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo kupata utaalam na mbinu bora kutoka kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wakubwa ambao wapo kwenye maeneo yao ili kukuza uwezo na kuendeleza kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara;

(viii) Kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Kilimo ngazi ya Halmashauri (DADPs);

(ix) Kuwawezesha Maafisa Ugani kutoa huduma bora za ugani na kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na mamlaka za utafiti na udhibiti;

(x) Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda;

(xi) Kutenga asilimia 20 ya mapato yatokanayo na tozo ya mazao ya kilimo (crop cess) kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwemo kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kimkakati;

(xii) Kutenga asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mazao ya mifugo kwa ajili ya shughuli za kuendeleza ufugaji kwa mujibu wa Waraka wa Rais Na. 01 wa mwaka 2002 kuhusu Hatua za Kuchukua Kuzuia Kuenea kwa Magonjwa ya Mifugo Nchini;

(xiii) Kutenga asilimia 5 ya mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009;

(xiv) Kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya Ushirika pamoja na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika;

(xv) Kuendeleza mipango miji na matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango kabambe (master plan) ya miji ili kuwa na miji iliyopangika hususan miji midogo inayochipukia na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura 113 na kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019;

(xvi) Kuendeleza na kuhamasisha matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ili kuwa na vijiji vilivyopangika na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114 na kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019;

(xvii) Kuboresha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kuimarisha kamati za mazingira katika ngazi za Halmashauri, Kata, Mtaa/Kijiji na kuhakikisha teknolojia za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira; uzoaji na uondoshaji wa taka; na kuendelea kuzingatia kanuni za udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki kwa mujibu wa zuio lililotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais Mwaka 2019;

(xviii) Kutenga fedha kwa ajili ya kuhifadhi maeneo oevu, vyanzo vya maji, upandaji miti, utunzaji misitu na maeneo ya hifadhi; na

(xix) Kutafsiri sheria, sera, kanuni na miongozo ya Serikali katika kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa miradi na shughuli za hifadhi ya mazingira

zinazotekelezwa na wadau mbalimbali zikiwemo asasi za kiraia, sekta binafsi na jamii zilizopo katika maeneo yao.

1.8 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep

108. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kukamilisha uingizaji wa takwimu sahihi za bajeti kwenye Mifumo ya *CBMS* na *PlanRep* kwa kuzingatia muda uliopangwa pamoja na mambo muhimu yafuatayo:

(i) Utumiaji wa Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF);

(ii) Usahihi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kuzingatia ukomo wa Bajeti kwa mwaka 2022/23 na makisio yanayoonesha uhalisia kulingana na ukomo wa miaka miwili inayofuata (2023/24 - 2024/25);

(iii) Ukadiriaji sahihi wa stahili za kisheria ikiwemo posho ya nyumba, umeme, simu na samani kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Katibu Mkuu (UTUMISHI);

(iv) Matumizi sahihi ya namba za miradi zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, mageresho ya kibajeti (GFS codes 2014), vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep na bei za bidhaa kama ilivyoainishwa katika orodha ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA); na

(v) Takwimu sahihi za Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha ya shughuli zilizopangwa kwenye bajeti.

1.9 Uchambuzi wa Mpango na Bajeti

109. Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi utafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, OR -TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuanzia tarehe 24 Januari, 2022. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala mango (*hard copy*) mbili (2) ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi ili kuwezesha uchambuzi wa kina kwa ajili ya kuboresha Mpango na Bajeti. Aidha, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwasilisha muhtasari wa makadirio ya mapato na matumizi katika nakala mango. Vile vile, uchambuzi wa Mpango na Bajeti utazingatia Muundo wa uwasilishaji wa MTEF uliobainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo.

110. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wanatakiwa kuwasilisha nakala mango (*hard copy*) moja (1) na nakala tete (*soft copy*) Wizara ya Fedha na Mipango, OR -TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina zilizofanyiwa

marekebisho ndani ya siku tano (5) baada ya uchambuzi.

1.10 Uwasilishaji wa Randama

111. Maafisa Masuuli wa Mafungu wanaelekezwa kuwasilisha Randama kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya kamati husika itakayotolewa na Ofisi ya Bunge. Uwasilishaji wa Randama uzingatie: Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/22 kwa kipindi kinachoishia Februari, 2022; changamoto na utatuzi wake; maelekezo ya Kamati za Bunge za Kisekta; na Mpango na Bajeti wa Mwaka 2022/23.

1.11 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

112. Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti utazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 na miongozo mingine iliyopo kwenye sekta mbalimbali.

1.11.1 Ufuatiliaji na Tathmini

113. Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuandaa Mpango Kazi shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya maendeleo ili kuendana na matakwa ya Mpango Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26);

(ii) Kutenga fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(iii) Kuandaa viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ya Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili viwe vipimio vya mafanikio ya taasisi husika;

(iv) Kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kuwa malengo, shabaha na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) vinatafsiriwa vema katika Mpango na Bajeti;

(v) Kujenga uwezo wa watumishi katika vitengo vya ufuatiliaji na tathmini na kuandaa mpango wa kurithisha watumishi wapya maarifa ili kuwa na mfumo wa ufuatiliaji endelevu;

(vi) Kuendelea kutumia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti;

(vii) Kujenga uwezo wa wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi kupitia mifumo ya

kielektroniki (system-based auditing) ili kuongeza ufanisi;

(viii) Kutoa kipaumbele na kutenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera hususan zilizotekelezwa kwa zaidi ya miaka mitano;

(ix) Kuhakikisha taarifa za ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya maendeleo zinaandaliwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (National Projects Management Information System - NPMIS); na

(x) Kufanya vikao vya Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa za ufualiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka kwa ajili ya kuleta uwazi na uwajibikaji.

1.11.2 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

114. Kwa kuzingatia Kifungu Na. 55(4) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 29(5) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka pindi inapomalizika. Aidha, taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishwe OR – TAMISEMI na Taasisi na Mashirika ya Umma ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Hazina na nakala kwa Wizara mama. Taarifa za utekelezaji ziandaliwe na kuwasilishwa katika nakala mango na tete kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo. Vilevile, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha nakala tete za taarifa za utekelezaji Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Dashibodi ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya Utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Taarifa zote ziwasilishwe katika muda wa siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika. Kadhalika, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji za Mwaka (*Annual Perfomance Report*) Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya tarehe 15 Oktoba kila mwaka wa fedha.

SURA YA PILI
MUUNDO WA UANDAAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

1.1 Utangulizi

115. Sura hii inaainisha muundo na fomu mbalimbali zinazopaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma katika hatua za uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti.

116. Katika kuandaa na kuwasilisha taarifa za Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika sheria, mpango, mifumo na miongozo ya uandaaji na usimamizi wa bajeti kama ifuatavyo: Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake; Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 pamoja na Kanuni zake; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 pamoja na Kanuni zake; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS); Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Mapato Serikalini (GePG); Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE); Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS); Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); Mfumo wa D – Fund *MIS*; Mfumo wa Uandaaji wa Mipango na Utoaji wa Taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma (PlanRep); Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikali za Mitaa (LGRCIS); Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Vituo vya Afya (GoTHoMIS); Mfumo wa Malipo na Utoaji wa Taarifa za Matumizi ya Fedha Katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS); Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati na Bajeti (MTSPBM); na Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (PIM-OM).

1.2 Maandalizi ya Mpango na Bajeti

117. Katika kuandaa Mpango na Bajeti Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) wakati wa kujaza fomu za makadirio ya mapato na matumizi ikijumuisha Fomu Na. 1 (Summary of Annual and Forward Budget Estimates for Revenue, Recurrent and Development Expenditure) na Fomu Na. 7 (Institutional Results Framework). Ufafanuzi wa fomu hizo ni kama ifuatavyo:

(a) Makadirio ya Mapato

118. Katika kuandaa na kuwasilisha makadirio ya mapato, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza kikamilifu Fomu Na. 4 (Revenue Estimates and Projections) kwa kutumia geresho la bajeti toleo la 2014 (GFS Codes 2014 Series) zilizo sahihi.

(b) Makadirio ya Matumizi

119. Katika kuandaa na kuwasilisha makadirio ya matumizi, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Matumizi ya Kawaida

120. Maafisa Masuuli wanatakiwa kujaza Fomu za mishahara Na. 8A (Summary of Personnel Emoluments Estimates at Vote Level); 8B (Summary of Personnel Emoluments Estimates at Subvote Level); 8C (Summary of Existing Employees on Payroll); 8D (Summary of Expected Employees with Employment Permit before end of the Current Year); 8E (Summary of New Employees to be Recruited); 8F (List of Employees Expected to Retire) na Fomu Na. 9 (Schedule of Personnel Emoluments - Establishment and Strength) kwa kuzingatia Ikama iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kipindi kinachoishia Juni 2023. Aidha, katika matumizi mengineyo, wanatakiwa kujaza Fomu Na. 3A (MTEF Sheet for Objectives, Targets and Activity Costing); 3B (Other Charges Expenditure Details of Annual and Forward Budget) na 3C (Recurrent Expenditure Summary of Draft Estimates) kwa kutumia vizio sahihi vya vipimo na gharama.

(ii) Matumizi ya Maendeleo

121. Katika kuandaa makadirio ya matumizi ya maendeleo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza Fomu Na. 6 (Development Expenditure Details of Annual and Forward Budget) na Fomu Na. 6.1 (Summary of Development Projects Expenditure Estimates). Aidha, taarifa muhimu za miradi zinapaswa kujazwa katika Fomu Na. 10A (Project Profile Data Form – Non-Strategic Projects) na Fomu Na. 10C (Summary of Project Forward Budget Estimates at Vote Level -All Sources).

(iii) Makadirio ya Ajira Zitakazozalishwa

122. Katika kuandaa makadirio ya ajira mpya zitakazozalishwa kutokana na utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo, Maafisa Masuuli wanapaswa kujaza kikamilifu Fomu Na. 15A (Framework for Mainstreaming Employment Creation in Sector Development Plans – Planning Level) na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu.

1.3 Utekelezaji wa Bajeti

123. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza kikamilifu Fomu Na. 11A (R) (Current Year MTEF Target Value Form - Recurrent Expenditure), 11A (D) (Current Year

MTEF Target Value Form - Development Expenditure), 11B (R) (Annual Cash Flow Plan for Recurrent Budget), 11B (D) (Annual Cash Flow Plan for Development Budget), 14B (R) (Annual Action Plan for Recurrent Budget for FY) na 14B (D) (Annual Action Plan for Development Budget for FY) kupitia mifumo ya CBMS na PlanRep kabla ya kuanza utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

1.4 Taarifa za Utekelezaji

124. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti za robo mwaka na mwaka mzima kwa kujaza kikamilifu Fomu Na. 6.2 (Fund Disbursement for Development Projects Implemented by Votes), 12A (Quarterly Cumulative MTEF Target Monitoring Form), 12B (Quarterly Cumulative Milestone Monitoring Form), 12C (Outcome Indicator Monitoring Form), na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Fomu Na. 15B (Framework for Mainstreaming Employment Creation in Sector Development Plans – Execution Level) inapaswa kujazwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu.

125. Kwa upande wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza Fomu Na. 5 (Quarterly Cumulative Revenue Detailed Form). Aidha, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatakiwa kujaza kikamilifu Fomu Na. 13A (Quartely Cumulative Financial Overview), 13B (Quarterly Cumulative Financial Details), na 13C1 (Quarterly Financial Progress Report – Own Source) 13C2 (Quarterly Financial Progress Report – Transfers) , 13C3 (Quarterly Financial Progress Report – Expenditure), 13C4 (Quarterly Financial Progress Report – Sectors) na 13C5 (Quarterly Financial and Physical Progress Report for LGA Development Activities).

MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2022/23 - 2024/25

Maelezo ya Kisera kwa Ufupi

(i) Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Mwenyekiti wa Bodi/Baraza

(ii) Maelezo ya Afisa Masuuli.

Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo

1.1 Uchambuzi wa Wadau

1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi

Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2020/21

2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2019/20

2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa

2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2021/22

2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2020/21

2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana

2.3 Changamoto zilizojitokeza 2021/22 na Mikakati ya kukabiliana na changamoto

Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2022/23 – 2024/25)

3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.1)

3.2 Malengo Makuu, Shabaha na Shughuli zitakazofanyika (Fomu Na. 3A)

3.3 Makadirio ya Matumizi ya Mengineyo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na. 3B)

3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (Fomu Na. 3C)

3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (Fomu Na.4)

3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.6)

3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fomu Na. 6.1)

3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (Fomu Na.7)

3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (Fomu Na. 8A)

3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (Fomu Na. 8B)

3.11 Kipengele Na.I – Muhtasari wa Wafanyakazi Walio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu Na. 8C)

3.12 Kipengele Na.II - Muhtasari wa Watumishi Wenye Kibali Wanaotarajiwa Kuajiriwa Katika Mwaka husika (Fomu Na. 8D)

3.13 Kipengele Na.III - Muhtasari wa Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kuajiriwa (Fomu Na. 8E)

MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2022/23 - 2024/25

3.14 Orodha ya Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kustaafu (Fomu Na. 8F)

3.15 Jedwali la Mishahara kulingana na Ikama (Fomu Na. 9)

3.16 Fomu ya Taarifa za Miradi (Fomu Na. 10A)

3.17 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi kwa mwaka unaofuata kwa Fungu (Fomu Na. 10C)

MUUNDO WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA ROBO MWAKA

Mada/ukurasa wa mbele
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno
Muhtasari

SURA YA KWANZA
Kifungu 1.1 Utangulizi na hali halisi
Elezea kwa ufupi majukumu ya taasisi, lengo la taarifa, mbinu na njia zilizotumika
Kifungu 1.2 Vipaumbele/malengo ya Mwaka
Eleza kwa ujumla vipaumbele vya mwaka kama inavyoonekana kwenye MTEF ya taasisi

SURA YA PILI: UTEKELEZAJI KWA UJUMLA
Kifungu 2.1 Hatua iliyofikiwa
Elezea kwa kifupi utekelezaji wa vipaumbele/malengo ya mwaka
Kifungu 2.2 Hatua za kuboresha utoaji wa Huduma
Elezea mabadiliko yaliyotokea kwenye taasisi yako katika kuboresha utoaji wa huduma
Kifungu 2.3 Changamoto na Mbinu za kukabiliana na Changamoto
Elezea kwa kifupi changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji na mbinu zitakazotumika kukabiliana na changamoto hizo.

SURA YA TATU : HALI YA KIFEDHA
Kifungu 3.1 Mapitio ya makusanyo ya mapato
Eleza malengo ya ukusanyaji wa mapato, makusanyo halisi, mwenendo na mwelekeo wa ukusanyaji, mafanikio na changamoto.
Kifungu 3.2 Mapitio ya Matumizi
Eleza hali ya kifedha kwa ujumla kwa kuainisha kiasi cha b ajeti iliyoidhinishwa, iliyotolewa na matumizi

- Kiambatisho Na 1: Fomu Na. 12A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Ufuatiliaji wa Malengo kwa Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF).
- Kiambatisho Na. 2: Fomu Na. 12B: Fomu ya Ujumla ya Robo mwaka ya Hatua Muhimu (Vipaumbele)
- Kiambatisho Na. 3: Fomu Na. 13A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka inayotoa Maelezo ya Hali ya Kifedha kwa Ufupi.
- Kiambatisho Na. 4: Fomu Na. 13B: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Kina ya Hali ya Kifedha.
- Kiambatisho Na. 5: Fomu Na. 13C1-C5: Fomu za Ujumla za Robo Mwaka kuhusu Taarifa za Hali ya Kifedha kwa Kina Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kiambatisho Na. 6 Fomu Na. 5: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Mapato kwa Kina

MUUNDO WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MWAKA MZIMA

Mada/Ukurasa wa Mbele
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno
Maelezo ya Waziri/ Mkuu wa Mkoa/ Meya/ Mwenyekiti wa Halmashauri/ Mwenyekiti wa Bodi/ Baraza
Maelezo ya Afisa Masuuli
Muhtasari

SURA YA KWANZA

Kifungu 1.1 Utangulizi na hali halisi
Elezea kwa ufupi majukumu ya taasisi, lengo la taarifa, mbinu na njia zilizotumika kufikia malengo
Kifungu 1.2 Dira na Dhima ya Taasisi
Elezea Dira na Dhima ya taasisi kama ilivyo kwenye Mpango Mkakati
Kifungu 1.3 Malengo ya Taasisi
Elezea malengo ya taasisi kama yalivyo kwenye Mpango Mkakati/MTEF
Kifungu 1.4 Vipaumbele/malengo ya Mwaka
Eleza kwa ujumla vipaumbele vya mwaka kama inavyoonekana kwenye MTEF ya taasisi

SURA YA PILI: UTEKELEZAJI KWA UJUMLA

Kifungu 2.1 Hatua iliyofikiwa
Elezea kwa kifupi utekelezaji wa vipaumbele/malengo ya mwaka
Kifungu 2.2 Hatua za kuboresha utoaji wa Huduma
Elezea mabadiliko yaliyotokea kwenye taasisi yako katika kuboresha utoaji wa huduma
Kifungu 2.3 Changamoto na Mbinu za kukabiliana na Changamoto
39.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya	3,511,860,191.35	351,186,019	352,043,629.45	100
40.	Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama	1,226,105,542.08	122,610,554	122,800,000.00	100
41.	Halmashauri ya Mji wa Kasulu	1,371,334,532.28	137,133,453	134,904,746.09	98
42.	Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi	2,237,125,703.00	223,712,570	220,000,000.00	98
43.	Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Vijijini	1,123,957,380.16	112,395,738	110,371,728.42	98
44.	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe	3,335,619,802.34	333,561,980	327,322,042.00	98
45.	Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	2,030,771,492.08	203,077,149	198,920,455.65	98
46.	Halmashauri ya Mji wa Bariadi	1,733,621,968.04	173,362,197	169,258,392.79	98
47.	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	6,906,695,231.35	690,669,523	674,318,800.00	98
48.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbarari	4,409,431,434.05	440,943,143	427,794,462.58	97
49.	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo	14,222,781,898.86	1,422,278,190	1,378,342,272.70	97
50.	Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	1,831,995,790.52	183,199,579	177,524,000.00	97
51.	Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa	2,032,099,216.92	203,209,922	196,221,217.35	97
52.	Halmashauri ya Wilaya ya Uyui	2,079,103,389.37	207,910,339	200,610,762.00	96
53.	Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale	1,549,105,863.54	154,910,586	149,179,918.16	96
54.	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	1,081,367,778.33	108,136,778	103,951,769.84	96
55.	Halmashauri ya Wilaya ya Gairo	680,641,313.97	68,064,131	65,408,886.00	96
56.	Halmashauri ya Wilaya ya Bahi	1,103,964,773.75	110,396,477	105,659,410.55	96
57.	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	2,000,400,951.37	200,040,095	191,317,280.00	96

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
58.	Halmashauri ya Wilaya ya Magu	2,422,161,839.67	242,216,184	231,051,500.00	95
59.	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	3,769,238,065.29	376,923,807	359,180,419.15	95
60.	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe	2,387,010,955.50	238,701,096	226,890,804.53	95
61.	Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma	562,616,257.05	56,261,626	53,433,683.20	95
62.	Halmashauri ya Mji wa Nzega	1,733,489,800.71	173,348,980	164,589,247.35	95
63.	Halmashauri ya Wilaya ya Songwe	2,737,221,890.24	273,722,189	258,786,056.20	95
64.	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	33,116,970,993.89	3,311,697,099	3,126,964,062.80	94
65.	Halmashauri ya Wilaya ya Itigi	1,061,999,059.15	106,199,906	100,000,000.00	94
66.	Halmashauri ya Wilaya ya Muheza	1,975,354,133.33	197,535,413	186,000,000.00	94
67.	Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi	6,365,286,344.65	636,528,634	598,484,366.00	94
68.	Halmashauri ya Wilaya ya Newala	885,340,048.56	88,534,005	83,214,357.02	94
69.	Halmashauri ya Mji wa Kahama	7,983,258,216.60	798,325,822	747,802,300.00	94
70.	Halmashauri ya Manispaa ya Arusha	12,366,407,953.18	1,236,640,795	1,157,878,508.87	94
71.	Halmashauri ya Mji wa Tarime	1,162,109,259.44	116,210,926	108,793,568.00	94
72.	Halmashauri ya Wilaya ya Tarime	5,661,909,578.35	566,190,958	530,007,481.00	94
73.	Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa	2,436,426,420.84	243,642,642	227,232,219.44	93
74.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi	2,897,901,440.59	289,790,144	267,891,787.38	92
75.	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	4,735,332,981.60	473,533,298	436,596,987.13	92
76.	Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa	2,337,856,042.99	233,785,604	214,144,936.00	92
77.	Halmashauri ya Manispaa ya Moshi	5,216,283,551.61	521,628,355	472,646,056.00	91

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
78.	Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe	1,361,453,278.42	136,145,328	123,136,405.09	90
79.	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	7,135,436,457.84	713,543,646	638,721,286.62	90
80.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu	1,355,590,982.89	135,559,098	120,890,212.67	89
81.	Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo	1,815,869,998.07	181,587,000	161,628,729.23	89
82.	Halmashauri ya Jiji la Tanga	11,071,621,172.90	1,107,162,117	985,150,075.85	89
83.	Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa	1,307,857,308.75	130,785,731	116,200,000.00	89
84.	Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua	3,543,601,732.73	354,360,173	314,239,400.00	89
85.	Halmashauri ya Wilaya ya Meru	2,236,368,835.00	223,636,884	198,117,268.26	89
86.	Halmashauri ya Mji wa Korogwe	1,012,627,694.74	101,262,769	89,172,772.00	88
87.	Halmashauri ya Wilaya ya Maswa	1,602,368,247.34	160,236,825	139,829,129.47	87
88.	Halmashauri ya Wilaya ya Iramba	1,100,952,806.58	110,095,281	95,399,426.79	87
89.	Halmashauri ya Mji wa Tunduma	6,338,990,742.54	633,899,074	549,000,000.00	87
90.	Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto	1,318,459,758.29	131,845,976	114,140,000.00	87
91.	Halmashauri ya Wilaya ya Madaba	676,995,757.31	67,699,576	58,386,000.00	86
92.	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	2,166,062,724.22	216,606,272	186,500,000.00	86
93.	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu	1,582,775,983.71	158,277,598	136,175,795.77	86
94.	Halmashauri ya Wilaya ya Makete	2,382,004,325.09	238,200,433	204,859,520.06	86
95.	Halmashauri ya Wilaya ya Nzega	1,755,013,092.89	175,501,309	150,220,000.00	86
96.	Halmashauri ya Wilaya ya Itilima	687,355,491.19	68,735,549	58,224,208.05	85
97.	Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo	1,769,217,343.67	176,921,734	149,639,959.54	85

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
98.	Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	2,264,654,880.15	226,465,488	191,506,000.00	85
99.	Mbinga	1,443,587,818.27	144,358,782	120,910,000.00	84
100.	Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	1,923,533,878.78	192,353,388	160,495,259.22	83
101.	Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo	2,147,335,602.01	214,733,560	178,405,331.80	83
102.	Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi	3,489,153,001.84	348,915,300	287,855,660.68	83
103.	Halmashauri ya Wilaya ya Msalala	3,921,400,026.82	392,140,003	323,138,394.00	82
104.	Halmashauri ya Mji wa Handeni	750,127,792.22	75,012,779	61,500,000.00	82
105.	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	2,604,660,462.47	260,466,046	212,503,810.00	82
106.	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba	1,154,397,617.56	115,439,762	93,881,000.00	81
107.	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	1,379,085,746.69	137,908,575	111,999,895.14	81
108.	Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza	1,239,487,545.94	123,948,755	100,000,000.00	81
109.	Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo	1,237,751,434.66	123,775,143	99,830,795.01	81
110.	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	1,391,845,799.42	139,184,580	111,000,000.00	80
111.	Halmashauri ya Mji wa Mafinga	4,363,344,903.92	436,334,490	346,807,204.08	79
112.	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	3,704,842,443.33	370,484,244	294,212,688.91	79
113.	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje	1,042,658,022.68	104,265,802	82,300,000.00	79
114.	Halmashauri ya Mji wa Geita	9,381,909,302.28	938,190,930	735,987,570.80	78
115.	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	1,695,047,628.37	169,504,763	132,905,000.00	78
116.	Halmashauri ya Wilaya ya Njombe	3,426,763,560.49	342,676,356	268,323,160.50	78
117.	Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi	1,623,410,613.79	162,341,061	125,000,000.00	77

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
118.	Halmashauri ya Manispaa ya Iringa	3,207,801,655.31	320,780,166	245,281,000.00	76
119.	Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	3,201,298,666.22	320,129,867	243,700,312.48	76
120.	Halmashauri ya Wilaya ya Iringa	2,484,148,948.83	248,414,895	188,458,028.67	76
121.	Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo	1,086,604,582.41	108,660,458	82,380,000.00	76
122.	Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda	2,418,963,346.74	241,896,335	183,000,000.00	76
123.	Halmashauri ya Wilaya ya Same	1,717,822,381.42	171,782,238	129,091,013.77	75
124.	Halmashauri ya Wilaya ya Mafia	1,055,592,357.78	105,559,236	78,826,741.28	75
125.	Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji	4,861,683,651.33	486,168,365	362,010,000.00	74
126.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe	1,216,287,639.85	121,628,764	90,267,600.00	74
127.	Halmashauri ya Wilaya ya Rwangwa	3,321,407,597.13	332,140,760	241,234,632.53	73
128.	Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga	3,612,359,093.59	361,235,909	262,095,501.00	73
129.	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	1,000,371,157.76	100,037,116	72,504,390.00	72
130.	Halmashauri ya Wilaya ya Rombo	1,581,263,972.56	158,126,397	112,400,000.00	71
131.	Halmashauri ya Manispaa ya Tabora	3,443,797,712.26	344,379,771	244,363,975.88	71
132.	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	2,693,200,255.12	269,320,026	190,934,880.00	71
133.	Halmashauri ya Wilaya ya Rorya	874,568,659.13	87,456,866	60,400,000.00	69
134.	Halmashauri ya Mji wa Ifakara	2,804,312,424.49	280,431,242	193,442,229.95	69
135.	Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe	2,769,416,105.20	276,941,611	190,877,884.59	69
136.	Halmashauri ya Wilaya ya Ngara	2,328,663,535.75	232,866,354	160,000,000.00	69
137.	Halmashauri ya Wilaya ya Hanang	3,795,695,441.59	379,569,544	259,652,000.00	68

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
138.	Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe	2,087,861,596.52	208,786,160	141,966,000.00	68
139.	Halmashauri ya Wilaya ya Handeni	1,813,857,979.63	181,385,798	122,924,802.13	68
140.	Halmashauri ya Wilaya ya Busega	1,342,100,556.58	134,210,056	90,511,200.00	67
141.	Halmashauri ya Wilaya ya Songea	1,327,174,667.28	132,717,467	89,127,571.40	67
142.	Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi	1,548,887,633.21	154,888,763	102,385,567.55	66
143.	Halmashauri ya Manispaa ya Musoma	1,668,517,941.87	166,851,794	110,000,000.00	66
144.	Halmashauri ya Wilaya ya Mtama	1,610,547,527.54	161,054,753	105,000,000.00	65
145.	Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro	3,559,988,897.54	355,998,890	227,974,700.00	64
146.	Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani	3,468,056,556.83	346,805,656	215,800,943.74	62
147.	Halmashauri ya Manispaa ya Makambako	2,628,968,095.59	262,896,810	163,180,000.00	62
148.	Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli	463,015,549.94	46,301,555	28,600,000.00	62
149.	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	3,275,939,559.44	327,593,956	201,348,655.49	61
150.	HAlmashauri ya Mji wa Babati	1,817,553,912.98	181,755,391	110,055,605.94	61
151.	Halmashauri ya Mji wa Newala	1,832,248,537.83	183,224,854	110,114,000.00	60
152.	Halmashauri ya Mji wa Mbulu	629,230,172.86	62,923,017	37,000,000.00	59
153.	Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea	3,961,876,691.02	396,187,669	228,240,922.48	58
154.	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	1,770,397,942.69	177,039,794	100,000,000.00	56
155.	Halmashauri ya Mji wa Njombe	7,504,967,721.41	750,496,772	419,181,400.00	56
156.	Halmashauri ya Jiji la Dodoma	36,321,177,409.58	3,632,117,741	1,963,868,190.73	54
157.	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	2,498,470,202.66	249,847,020	134,727,525.00	54

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
158.	Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni	1,731,416,761.26	173,141,676	90,950,100.00	53
159.	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro	7,184,505,329.61	718,450,533	375,135,632.02	52
160.	Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga	2,822,180,478.95	282,218,048	142,942,179.41	51
161.	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema	1,255,241,112.63	125,524,111	61,200,000.00	49
162.	Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji	2,075,354,764.48	207,535,476	100,500,000.00	48
163.	Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya	15,272,407,057.68	1,527,240,706	729,934,600.00	48
164.	Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	1,313,586,811.61	131,358,681	61,752,120.00	47
165.	Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga	2,404,229,499.45	240,422,950	111,792,500.00	46
166.	Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	3,233,705,054.33	323,370,505	148,798,800.00	46
167.	Halmashauri ya Mji wa Kondoa	927,304,464.55	92,730,446	42,000,000.00	45
168.	Halmashauri ya Wilaya ya Singida	1,033,635,667.52	103,363,567	46,628,318.17	45
169.	Halmashauri ya Manispaa ya Singida	2,070,209,967.82	207,020,997	93,000,000.00	45
170.	Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo	1,472,705,541.75	147,270,554	66,000,000.00	45
171.	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	1,409,824,655.75	140,982,466	60,000,000.00	43
172.	Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	2,280,481,657.22	228,048,166	96,646,450.00	42
173.	Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti	949,221,447.70	94,922,145	40,000,000.00	42
174.	Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa	1,088,064,949.61	108,806,495	43,200,000.00	40
175.	Halmashauri ya Wilaya ya Masasi	3,529,194,705.43	352,919,471	134,400,183.20	38
176.	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	3,000,537,423.57	300,053,742	110,000,000.00	37
177.	Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga	2,084,547,697.31	208,454,770	73,528,494.40	35

Na.	HALMASHAURI	MAPATO YALIYOKUSANYWA (YASIYOLINDWA)	ASILIMIA 10	MIKOPO ILIYOTOLEWA	%
178.	Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	1,998,688,174.33	199,868,817	68,493,216.70	34
179.	Halmashauri ya Wilaya ya Momba	1,627,697,263.81	162,769,726	50,000,000.00	31
180.	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	1,664,127,638.94	166,412,764	50,418,871.00	30
181.	Halmashauri ya Mji wa Lindi	1,944,435,139.81	194,443,514	58,151,768.46	30
182.	Halmashauri ya Mji wa Masasi	1,585,701,305.15	158,570,131	33,100,000.00	21
183.	Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe	1,838,474,374.21	183,847,437	28,000,000.00	15
184.	Halmashauri ya Wilaya ya Chemba	1,061,174,732.56	106,117,473	14,000,000.00	13
		626,831,692,299	**62,683,169,230**	**53,817,764,696**	**86**

KIAMBATISHO B

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

1.1 Utangulizi

126. Sura hii inaeleza mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/21 kwa kuzingatia malengo na shabaha za bajeti. Mapitio hayo yamefanyika katika miradi ya maendeleo ya kielelezo, kimkakati na maeneo mengine ya kipaumbele. Aidha, mapitio ya utekelezaji wa bajeti katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 yamefanyika. Vilevile, sura hii inabainisha mafanikio, changamoto na mikakati ya kuboresha uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23.

1.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2020/21

127. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21, ulizingatia vipaumbele vilivyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Agenda 2063 ya Umoja wa Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Aidha, usimamizi katika utekelezaji ulizingatia sheria na miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134; na Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania. Vilevile, Serikali ilisimamia utekelezaji wa Sera za Mapato na Matumizi za Muda wa Kati zilizolenga kuwezesha utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

1.2.1 Mapato na Matumizi

128. Katika mwaka 2020/21, Serikali ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 34,879.8 kutoka vyanzo mbalimbali. Kati ya kiasi hicho, Serikali imekusanya shilingi bilioni 31,280.1 sawa na asilimia 89.7 ya bajeti iliyoidhinishwa ikijumuisha shilingi bilioni 20,594.6 mapato ya ndani; na shilingi bilioni 10,685.5 ni misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ilitumia shilingi bilioni 31,280.1 kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo na kawaida. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 20,613.0 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 10,667.1 ni matumizi ya maendeleo. Jedwali Na.1 linaonesha mchanganuo wa makadirio ya mapato na matumizi ikilinganishwa na ufanisi halisi uliofikiwa katika kila kipengele cha mapato na matumizi.

Jedwali Na. 1: Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2020/21

Shilingi Bilioni

	Bajeti	Halisi	Asilimia
Mapato ya Ndani	**24,065.5**	**20,594.6**	**85.6%**
Mapato ya Kodi (TRA)	20,136.0	17,317.5	86.0%
Mapato Yasiyo ya Kodi (TRA)	189.8	306.8	161.6%
Mapato Yasiyo ya Kodi	2,924.8	2,213.2	75.7%
Mapato ya Halmashauri	815.0	757.1	92.9%
Misaada	**949.3**	**702.9**	**74.0%**
Misaada ya Kibajeti	138.3	-	0.0%
Misaada ya Maendeleo	614.5	527.5	85.8%
Mifuko ya Kisekta	196.5	175.4	89.2%
Mikopo Nafuu	**1,925.0**	**1,957.2**	**101.7%**
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	-	210.2	-
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,846.0	1,669.9	90.5%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	79.0	77.1	97.6%
Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje	**3,035.6**	**3,121.2**	**102.8%**
Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani	**4,904.2**	**4,904.2**	**100.0%**
Mikopo ya Kugharamia Miradi	1,588.2	1,905.0	120.0%
Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani	3,316.1	2,999.1	90.4%
JUMLA YA MAPATO	**34,879.8**	**31,280.1**	**89.7%**
Matumizi ya Kawaida	**22,100.5**	**20,613.0**	**93.3%**
Mishahara	7,762.4	7,638.5	98.4%
Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni & CFS)	10,376.8	8,020.1	77.3%
Matumizi Mengineyo	3,961.3	4,954.4	125.1%
Matumizi ya Maendeleo	**12,779.3**	**10,667.1**	**83.5%**
Miradi ya Fedha za Ndani	10,043.2	9,381.6	93.4%
Miradi ya Fedha za Nje	2,736.0	1,285.5	47.0%
JUMLA MATUMIZI	**34,879.8**	**31,280.1**	**89.7%**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Sababu za kufikia na kutokufikia malengo

(i) Kuvuka kwa lengo la mapato yasiyo ya kodi (TRA) kumetokana na kuboreshwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa vyanzo hivi;

(ii) Kuvuka kwa lengo katika mikopo nafuu kulitokana na kupatikana kwa mikopo nafuu ya kibajeti kwa ajili ya kupambana na janga la ugonjwa wa UVIKO-19;

(iii) Kufikiwa kwa lengo la mikopo ya kibiashara kutoka ndani kulichangiwa na

mwenendo mzuri wa soko la ndani uliotokana na jitihada za Serikali katika kutoa elimu kwa umma juu ya faida za kuwekeza katika dhamana za Serikali na kuongezeka kwa ukwasi kwenye mabenki ya kibiashara;

(iv) Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, uwepo wa Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa fedha za ndani, umeongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(v) Kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa sehemu kubwa kumetokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi, hususan uzalishaji wa viwandani na uingizaji wa mizigo toka nje uliochangiwa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19;

(vi) Kutofikiwa kwa malengo ya misaada kulitokana na janga la UVIKO-19 lililoathiri baadhi ya nchi washirika wa maendeleo kushindwa kutoa fedha kulingana na ahadi pamoja na changamoto ya kushindwa kutumia fedha kwa wakati katika miradi ya maendeleo na hivyo kuathiri mtiririko wa fedha. Aidha, kutopatikana kwa misaada ya kibajeti kulitokana na kutotolewa kwa fedha zilizobaki katika programu ya Economic and Fiscal Government (EFGP) kutokana na kutofikiwa kwa lengo la baadhi ya viashiria vya utendaji wa programu;

(vii) Kuvuka kwa lengo la mikopo ya kibiashara kutoka nje kulitokana na mikopo iliyokopwa ili kufidia upungufu wa makusanyo ya mapato kutoka vyanzo vya ndani ili kugharamia miradi ya maendeleo; na

(viii) Kwa upande wa matumizi, kuvuka kwa lengo la matumizi mengineyo kulitokana na kugharamia shughuli za kitaifa pamoja na malipo ya madeni ya watumishi na wazabuni. Aidha, lengo la matumizi ya miradi kwa fedha za nje halikufikiwa kutokana na misaada pamoja na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo kutopatikana kama ilivyotarajiwa kulikosababishwa na janga la UVIKO-19.

1.2.2 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

129. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 umekuwa na mafanikio makubwa katika nyanja na sekta mbalimbali. Mafanikio hayo ni pamoja na:

130. **Ulipaji wa Mishahara:** Hadi Juni, 2021 jumla ya shilingi bilioni 7,638.5 sawa na asilimia 98.4 ya lengo la shilingi bilioni 7,762.4 zililipwa kwa wakati kwa kutumia mapato ya ndani. Aidha, kiasi cha shilingi 2,053.0 kimetumika kwa robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya ulipaji mishahara.

131. **Upandishaji Vyeo Watumishi**: Hadi Juni, 2021 shilingi bilioni 67.7 zimetumika kwa ajili ya kugharamia upandishaji vyeo watumishi 145,553 waliostahili. Aidha, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi bilioni 26.9 zimetumika kwa ajili ya kugharamia upandishaji vyeo watumishi 55,851 waliostahili.

132. **Ulipaji wa Madeni ya Makandarasi, Wazabuni, Watumishi na Watoa Huduma:** Hadi Juni 2021, Serikali imehakiki na kulipa madeni yenye jumla ya shilingi bilioni 850.7. Kati ya kiasi hicho, wakandarasi shilingi bilioni 465.5, wazabuni shilingi bilioni 85.1, watumishi shilingi bilioni 167.9 na watoa huduma na madeni mengineyo shilingi bilioni 132.2. Aidha, katika kipindi hicho, kiasi cha shilingi bilioni 10.2 zimetumika kulipa madeni ya makandarasi, wazabuni na watoa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha shilingi bilioni 8.7 zilizolipwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri . Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kiasi cha shilingi bilioni 5.3 zimetumika kwa ajili ya ulipaji madeni.

133. **Ulipaji wa Deni la Serikali:** Hadi Juni 2021, Serikali ilitumia shilingi bilioni 7,904.7 sawa na asilimia 93.44 ya lengo kwa ajili ya kulipa mitaji na riba ya mikopo mbalimbali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,473.20 zilitumika kulipa mitaji sawa na asilimia 96.63 ya lengo na shilingi bilioni 2,431.50 zilitumika kulipa riba sawa na asilimia 87 ya lengo. Kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kiasi cha shilingi 1,935.6 zilitumika. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,300.7 zilitumika kulipa mitaji na shilingi bilioni 634.9 zilitumika kulipa riba.

134. **Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji**

Katika mwaka 2020/2021, Serikali ilikamilisha tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 ambapo tathmini hiyo imeonesha mafaniko mbalimbali yaliyopatikana katika kipindi hicho pamoja na changamoto mbalimbali za kisera, kisheria na kiutendaji. Kutokana na tathmini hiyo, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imeendelea na maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Uwekezaji ikiwa ni pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji na utungaji wa Sheria mpya ya Uwekezaji ili kuimarisha uratibu, usimamizi, uhamasishaji na ufuatiliaji wa masuala ya uwekezaji nchini. Pia, Serikali imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ikiwemo Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (The Government Roadmap) wa Mwaka 2010, Mpango wa Kuboresha Mifumo ya Udhibiti wa Biashara (Blueprint) wa Mwaka 2019 na kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya wawekezaji (Online Investors Feedback Platform). Vilevile, Serikali ilifanya maboresho ya utoaji wa

vibali vya kazi ambapo kwa sasa maombi yanaweza kutolewa hata ndani ya siku moja kama nyaraka zote zinakuwapo na wahusika pia. Hivi sasa vibali hivyo vinaweza kupatikana kwa njia ya mtandao na vinaunganishwa na vibali vya ukaazi *e permit*.

135. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imeanza maandalizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Huduma za Upatikanaji wa Vibali vya Uwekezaji (Tanzania Electronic Investment Window) utakaotoa huduma za Taasisi zote zilizo katika Kituo cha Utoaji wa Huduma kwa Pamoja TIC. Vilevile, Serikali imeanzisha Kituo cha Mawasiliano kwa Wawekezaji (Tanzania Investment Call Centre) ambayo mtu yeyote anayetaka ufafanuzi, elimu na taratibu kuhusu masuala ya uwekezaji anaweza kupiga simu na kupata ufafanuzi na ufumbuzi.

136. **Kuendeleza Kongani za Kiuchumi**

Katika kuendeleza kongani za kiuchumi ikiwemo za viwanda, teknolojia, bandari za kisasa, na uendelezaji vituo vya biashara mipakani, katika mwaka 2020/21, Serikali ilitekeleza mikatati ya kuvutia uwekezaji katika eneo hili. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeweza kuhamasisha uanzishaji wa kongani kwa wawekezaji wa ndani katika eneo la Kitaraka, Manyoni na Dumila, Morogoro ambazo zitakuwa mahususi kwa ajili ya uendelezaji kilimo cha kisasa cha alizeti na uzalishaji mafuta ya kisasa ya alizeti (double refined) pamoja na sukari. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Kanda za Manyoni, Singida na Dumila, Morogoro pamoja na kuanza majadiliano ya uendelezaji wa Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo (BSEZ), ujenzi wa kongani ya viwanda eneo la Kwala Mkoa wa Pwani na kongani ya Viwanda eneo la Kigamboni, Dar es Salaam.

137. **Benki ya Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji (Land Bank)**

Katika mwaka 2020/21, Serikali imeanza maandalizi ya kuweka Benki ya Ardhi kwa kubainisha ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji nchi nzima ambapo jumla ya hekta 1,606,193.40 zimeainishwa. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imeendelea na ujenzi wa Mfumo ambao utatumika kuhifadhi taarifa za ardhi hiyo ili kurahisisha upatikanaje wake kwa wawekezaji. Uanzishaji wa Mfumo (Portal) utawezesha wawekezaji kujua maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na upatikanaji wake utakuwa kwa njia ya mtadao. Ardhi, iliyobanishwa ni kwa ajili ya kilimo, biashara, makazi, viwanda, hoteli, hospitali, Shule za Sekondari, kumbi za mikutano, n.k.

138. **Uhamasishaji Uwekezaji**

Ili kuhakikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wanapata taarifa za fursa za uwekezaji zinazotokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, katika mwaka 2020/21, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kiliratibu utafiti wa kuibua na kuchambua fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali zitakazotokana na mradi wa Reli ya kisasa (SGR) ili kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Serikali iliandaa mikutano ya uwekezaji iliyojumuisha nchi 14 iliyofanyika nchini, mikutano 14 iliyofanyika nje ya nchi na mikutano 20 kwa njia ya mtandao. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, TIC iliwezesha uandaaji wa makongamano ya uwekezaji manne (4) yaliyofanyika katika mikoa ya Mara, Tabora, Katavi, Pwani, Singida na Tanga. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 mikutano kama hiyo imefanyika kwa mikoa ya Kilimanjaro na Rukwa.

139. Katika mwaka 2021, jumla ya miradi ya uwekezaji **235** ilisajiliwa na TIC ikiwa ni ongezeko la **asilimia 8** ikilinganishwa na mwaka 2019/20 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni **3,301.82** na inatarajiwa kuzalisha ajira **36,849**. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, jumla ya miradi mipya **62** imesajiliwa na TIC inayotarajiwa kuwekeza mitaji ya Dola za Marekani milioni **477** na kutoa ajira **7,598** ikilinganishwa na miradi 46 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni **309** na ajira **4,273** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/21. Ongezeko hili limetokana na jitihada za kuboresha utoaji wa huduma kwa wawekezaji. Vilevile, Serikali imeanza kuandaa video ya kuhamasisha uwekezaji itakayotumika ndani na nje ya nchi.

Mafanikio katika Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati

140. **Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa *(SGR):*** Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya *SGR* ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300), umefikia asilimia 93.0 na majaribio ya uendeshaji wa treni yanatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka 2021. Aidha, kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutopora (km 422) umefikia asilimia 70.1. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa tuta, makalavati, mahandaki, madaraja ya juu, madaraja, stesheni, miundombinu ya umeme, mifumo ya ishara ya mawasiliano na njia za reli katika eneo la bandari. Aidha, utekelezaji wa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341) upo katika hatua za awali ambapo hadi Juni 2021, kazi ya usanifu, ujenzi wa kambi na upelekaji wa vifaa, mitambo na wataalamu ilikuwa inaendelea. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 1,726.53 zimetumika na kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 79.3 zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

141. **Uboreshaji Huduma na Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli ya Kati:** Serikali iliendelea kugharamia mradi wa ukarabati wa njia kuu ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Isaka (km 970) ambapo hadi Juni, 2021 jumla ya km 553.6 kati ya km

970 na madaraja 370 yalikarabatiwa. Aidha, Serikali ilinunua mabehewa 44, kukarabati mabehewa 200 ya mizigo na kukamilisha uundwaji wa vichwa vya treni vitatu (3). Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 187.52 zilitumika.

142. **Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania:** Katika kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), hadi Juni 2021, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 73.11 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya mwisho yenye ya ununuzi wa ndege moja (1) aina ya *De Havilland D8-400* na ununuzi wa jozi ya injini ya ndege aina ya *Dash 8 Q400*. Aidha, katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imetumia jumla shilingi bilioni 557.8 kwa ajili ya malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tano (5) mpya na kati ya ndege hizo, moja (1) ni aina ya *Boeing 787-8*; mbili (2) aina ya *Boeing 737-9*; moja (1) aina ya *De Havilland D8-400* na moja (1) aina ya *Boeing 767-300F* ya mizigo pamoja na malipo ya mwisho ya ndege mbili (2) aina ya *Airbus A220 – 300* yalifanyika.

143. **Ujenzi wa Miundombinu, Ununuzi wa *RADAR* na Vifaa vya Hali ya Hewa:** Katika kuimarisha huduma za hali ya hewa**,** Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu na vifaa. Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali imenunua *RADAR* mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa mkoani Dodoma na Kilimanjaro, ujenzi wa miundombinu ya *RADAR* mkoani Mtwara, Kigoma na Mbeya, ukarabati wa vituo saba (7) na ununuzi wa vifaa vya hali ya hewa. Kukamilika kwa ununuzi wa *RADAR* hizo kutakamilisha malengo ya muda mrefu ya kuwa na mtandao wa *RADAR* saba (7) za hali ya hewa hapa nchini. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 16.98 zilitumika na shilingi bilioni 3.2 zimetolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

144. **Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP (MW 2,115):** Ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia 55.6 ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa tuta kuu la bwawa, ujenzi wa njia za kupeleka maji kwenye mitambo, ujenzi wa jengo la mitambo, ujenzi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme, utengenezaji wa mitambo tisa ya kuzalisha umeme na ujenzi wa kingo za bwawa. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 1,171.53 zimetumika na shilingi bilioni 81.4 zimetolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

145. **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti (kV) 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Kinyerezi - Dodoma:** Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi mahsusi wa kusafirisha umeme kutoka JNHPP (MW 2,115) hadi Chalinze ambapo hadi Juni 2021, shilingi bilioni 112.9 zimetumika. Aidha, shilingi bilioni 29.4 zimetumika kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa njia ya umeme kutoka Chalinze - Kinyerezi.

146. **Usambazaji wa Umeme Vijijini:** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa umeme vijijini ambapo hadi mwezi Juni, 2021 vijiji 10,312 kati ya vijiji 12,317 sawa na asilimia 83.72 vilikuwa vimeunganishwa na huduma ya umeme. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 346.92 zimetumika na shilingi bilioni 88.1 zimetolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

147. **Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia – (LNG):** Serikali iliendelea na maandalizi ya kuandaa mazingira wezeshi ya uwekezaji katika mradi wa kusindika gesi asilia nchini katika eneo la Likong'o mkoani Lindi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: utwaaji wa ardhi; kutoa elimu kwa wananchi na wadau; kuandaa Mwongozo wa Majadiliano na Nyenzo za Majadiliano zitakazoongoza majadiliano ya Mikataba Hodhi kati ya Serikali na Kampuni za uendelezaji mradi. Katika mwaka 2020/21, jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika.

148. **Usambazaji wa Gesi Asilia Nchini:** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia nchini ambapo mtandao wenye jumla ya km 130 umejengwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara na kuwezesha nyumba 1,191, viwanda 52, taasisi tisa (9) na magari 750 kutumia gesi asilia. Aidha, katika mwaka 2020/21 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa km 12 itakayounganisha zaidi ya nyumba 6,000 katika Mkoa wa Dar es Salaam; kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa km 7.1 itakayounganisha viwanda zaidi ya 20 katika Mkoa wa Pwani; kukamilisha mradi wa kuunganisha nyumba 300 katika Mkoa wa Mtwara; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha nyumba 200 katika Mkoa wa Lindi; na kuendelea na taratibu za kuwapata wakandarasi wa miradi ya ujenzi wa vituo vipya vya *Compressed Natural Gas (CNG)* kwa ajili ya matumizi ya magari katika Mkoa wa Dar es Salaam. Vilevile, gesi asilia imeendelea kusambazwa katika vituo vya uzalishaji wa umeme ambapo kwa sasa takriban Megawati 901.32 sawa na asilimia 60 ya umeme wote unaozalishwa nchini unatokana na gesi asilia.

149. **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania):** Hadi Juni 2021, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika majadiliano na kusainiwa kwa Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji *(Host Government Agreement – HGA)* na Mkataba wa Ubia *(Shareholding Agreement - SHA)* kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji; Serikali ya Tanzania kufikia maamuzi ya ushiriki wake katika Mradi wa EACOP kwa asilimia 15; kukamilika kwa majadiliano na kuridhiwa kusainiwa *(initialed)* kwa mikataba ya uendeshaji wa Bandari ya Tanga, mikataba ya ukodishaji wa ardhi kwa ajili ya mkuza na maeneo

ya kipaumbele ya mradi; na kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi katika maeneo ya kipaumbele. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 262.7 zimetumika ikiwa ni pamoja na kugharamia hisa za Serikali katika mradi huo.

150. **Ujenzi na Ukarabati wa Meli Katika Maziwa Makuu:** Serikali iliendelea kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji wa maji katika maziwa makuu kwa kutekeleza yafuatayo: Ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo umefikia asilimia 74; na ukarabati wa meli mbili (2) za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu umekamilika. Aidha, Serikali ilikamilisha taratibu za manunuzi na kusaini mikataba ya ujenzi na ukarabati wa meli zifuatazo: Meli mpya ya kubeba mizigo na ukarabati wa meli ya MV Umoja katika Ziwa Victoria; na meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo, meli ya MT Sangara, na MV Liemba katika Ziwa Tanganyika. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 26.72 zimetumika na kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi bilioni 4.9 zimetolewa.

151. **Ujenzi wa Barabara na Madaraja:** Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali imejenga mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa km 599.45 (barabara kuu km 415.50 barabara za mikoa km 43.25 na barabara za mijini na vijijini km 140.70). Hivyo, hadi kufikia Juni 2021, mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami umefikia km 13,643.45. Aidha, Serikali iliendelea na ujenzi na matengenezo ya barabara zenye urefu wa km 25,981.98 mijini na vijijini ambapo, barabara za kiwango cha changarawe ni km 3,725.52 na matengenezo ya kawaida na sehemu korofi km 22,256.46.

152. Miradi ya ujenzi wa barabara iliyokamilika ni pamoja na: barabara za Manyoni – Itigi – Tabora, sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4); Masasi – Songea – Mbambabay (km 66); Mtwara – Mnivata (km 50); Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112.0); Mpemba – Isongole (km 51.2); na Kyaka – Bugene – Kasulo, sehemu ya Kyaka Bugene (km 59.1).

153. Miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea ni pamoja na: Upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 19.2) njia nane umefikia asilimia 88.0; Makutano - Natta – Mugumu, sehemu ya Makutano – Natta (Sanzate) (km 50) umefikia asilimia 88.0; Itoni – Ludewa – Manda, sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) umefikia asilimia 69.0; Chunya – Makongolosi (km 43) umefikia asilimia 92.0; Njombe - Makete – Isyonje, sehemu ya Njombe - Moronga (km 53.9) umefikia asilimia 88.0; Kidawe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi sehemu ya Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (km 50) umefikia asilimia 98.0; Loliondo – Mto wa Mbu sehemu ya Waso – Sale (km 50) imefikia aslimia 66.0; Tabora – Ipole – Koga – Mpanda sehemu za

umefikia asilimia 82.0, na Kasinde – Mpanda (km 118) asilimia 66.0; barabara za ndani ya Usesula – Komanga (km 115) umefikia asilimia 77.0, Komanga – Kasinde (km 120) Ikulu (Chamwino - km 15.1) umefikia asilimia 96.0; na Nanganga – Ruangwa – Nachingwea sehemu ya Nanganga - Ruangwa (km 53.2) umefikia asilimia 10.0.

154. Serikali iliendelea na ujenzi wa madaraja makubwa ya Kitengule (Kagera) asilimia 50.0, Daraja Jipya la Wami (Pwani) asilimia 53.9, Msingi (Singida) asilimia 75.0, Kiyegeya (Morogoro) asilimia 80.0, Sibiti (Singida) asilimia 95.2, Daraja Jipya la Tanzanite (Dar es Salaam) asilimia 92.0 na daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) asilimia 27.5. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa madaraja 88, makalvati 268, na mifereji ya maji km 109.25 inayosimamiwa na TARURA. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 1,431.70 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi bilioni 295.8 zilitumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja.

155. **Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege:** Serikali ilikamilisha upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza sehemu ya kwanza na ya pili. Miradi mingine inayoendelea na hatua iliyofikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Songea (asilimia 93.6), Songwe (asilimia 77) na Mtwara (asilimia 60). Aidha, Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 51.2 zimetumika na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 bilioni 22.1 zimetolewa.

156. **Ujenzi wa Nyumba za Makazi Magomeni:** Serikali iliendelea na ujenzi wa nyumba za Makazi za Magomeni Kota zenye uwezo wa kuhudumia kaya 656, ujenzi huo umefikia asilimia 99. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 16.5 zilitumika na shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

157. **Uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma**: Serikali ilikamilisha ubunifu na usanifu wa majengo ya awamu ya pili ya wizara 24, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao. Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara (km 51.2) kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali umefikia asilimia 82. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 44.7 zilitumika na shilingi bilioni 50.0 zilitolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

158. **Miradi ya Vivuko:** Serikali ilikamilisha malipo ya mwisho ya ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia (Pwani) na Chato – Nkome (Geita), ujenzi wa boti mpya tatu (3) za uokozi kwa ajili ya Ukerewe na Lindi na ukarabati wa MV Kigamboni. Aidha, Serikali iliendelea na ukarabati wa MV Sengerema, MV

Tegemeo, MV KIU na MV Misungwi. Jumla ya shilingi bilioni 5.6 zimetumika mwaka 2020/21.

159. **Uboreshaji na uimarishaji wa Bandari:** Shughuli zilizotekelezwa katika Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na; kukamilisha uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 kwa kuongeza kina kufikia mita 14.5 kwa asilimia 100 na gati la kushushia magari (RoRo Berth), yadi ya kuhudumia makasha (Container Yard) ujenzi umefikia asilimia 84 na ujenzi wa bandari kavu ya Kwala - Ruvu uliofikia asilimia 58. Katika bandari ya Tanga, ukarabati wa maghala, gati namba 1 na 2, na uongezaji wa kina cha lango la kuingia na kugeuzia meli ulikamilika. Serikali ilikamilisha ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300, ujenzi wa uzio na sakafu ngumu eneo la mita za mraba 600 katika Bandari ya Mtwara. Aidha, shilingi bilioni 29.5 zilitumika katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

160. Ujenzi wa gati za Lushamba, Bukoba, Ntama, Nyamirembe, Chato awamu ya kwanza, Magarini, Muleba; na gati mbili (2) za Majahazi katika bandari ya Mwigobero, Musoma katika Bandari za Ziwa Victoria zimekamilika. Katika bandari za Ziwa Tanganyika, ujenzi wa gati za Kagunga, Kalya (Sibwesa), Lagosa, na Kabwe (Nkasi); Bandari ya Karema umefikia asilimia 45; ujenzi na ukarabati wa Bandari za Kigoma, Kibirizi na Ujiji umefikia asilimia 53. Aidha, ujenzi wa tishari 2 (Self-Propelled cargo Barges) na sakafu ngumu katika Bandari ya Kiwira na Itungi katika Ziwa Nyasa umekamilika. Shilingi bilioni 264.15 zimetumika kwa mwaka 2020/21.

161. Katika mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, upembuzi yakinifu na utwaaji wa ardhi kwa ajili ya kutekeleza mradi umekamilika. Serikali imeunda Kamati ya Majadiliano (Government Negotiation Team) kwa lengo la kuandaa nyaraka za majadiliano na kuona namna bora ya Serikali kuishirikisha sekta binafsi kutekeleza mradi huo kwa kuzingatia Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi PPP, Sura 103.

162. **Uimarishaji wa Sekta ya Kilimo:**

(i) **Hali ya Chakula:** uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2020/21 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2021/22 umefikia tani 18,425,250, sawa na ongezeko la tani 228,517 ikilinganishwa na tani 18,196,733 za msimu wa 2019/20. Hivyo, kwa kuzingatia kuwa mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/22 ni tani 14,796,751, nchi imezalisha ziada ya tani 3,628,499. Kuongezeka kwa uzalishaji kumesababisha utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 125.

(ii) **Usalama wa Chakula**: Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula iliendelea kununua chakula ili kuimarisha hifadhi ya chakula nchini. Katika kipindi cha Julai 2020, hadi Septemba 2021, jumla ya tani 20,800.8 za

mazao ya chakula zimenunuliwa hivyo kuwezesha nchi kuwa na akiba jumla ya tani 128,184.9 katika ghala za hifadhi ya taifa.

(iii) **Miundombinu ya Umwagiliaji**: Serikali, imekamilisha ujenzi wa skimu sita (6) za umwagiliaji zenye uwezo wa kuhudumia hekta 1,849 na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya skimu tatu (3) za umwagiliaji za Maliwanda - Mara asilimia 97, Orumwi - Siha asilimia 55, na Madibira - Mbeya asilimia 8.

(iv) **Utafiti:** Tafiti mbalimbali zimefanyika ambapo aina 14 (ngano 5, mpunga 2, karanga 3, mahindi 2 na mchicha 2) za mbegu za mazao zilizofanyiwa utafiti zilipelekwa katika Taasisi ya Uthibiti wa Mbegu kwa ajili ya kuangalia ubora wake ambayo ni hatua za mwisho za uhakiki kabla ya uthibitisho.

(v) **Upatikanaji wa Pembejeo:** Upatikanaji wa mbegu uliongezeka kufikia tani 32.8 za mbegu za alizeti na tani 365 za ngano. Serikali ilifanikisha uzalishaji wa miche 754,300 ya michikichi na 8,200 ya zabibu kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Magereza Tanzania na Halmashauri sita (6) za Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA) ilisambaza miche ya michikichi 40,000 kwa wakulima katika Wilaya ya Kaliua – Tabora. Vilevile, maeneo mapya kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu za alizeti katika mashamba matatu (3) yenye ukubwa wa hekta 420 yalifunguliwa. Kwa upande wa mbolea, vibali 85 ambavyo vitawezesha kuingiza tani 124,815.4 vilitolewa ambapo hadi robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, tani 108,769.1 zimeingizwa nchini.

(vi) **Masoko ya mazao ya kilimo**: Serikali ilinunua tani 27,457.3 za nafaka kutoka kwa wakulima ambapo kati ya hizo tani 23,745.97 ni za mahindi. Aidha, Mkataba na Kampuni ya Grain Industries LTD ya Nchini Kenya wa kuiuzia mahindi tani 144,000 umesainiwa. Vilevile, mikataba mipya ya uuzaji wa mahindi na nchi ya Sudani Kusini, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na Zimbabwe inaendelea kukamilishwa. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 71.1 zimetumika na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 19.0 zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa mahindi. Aidha, katika kukabiliana na bei ndogo ya mahindi, Serikali inatarajia kutoa shilingi bilioni 50.0 kwa ajili ya ununuzi wa mahindi.

163. **Uendelezaji wa Sekta ya Mifugo**:

(i) **Ujenzi wa majosho**; Serikali ilikamilisha ujenzi wa majosho mapya 89 na kukabrabati majosho 161 na hivyo kuongeza idadi ya majosho kutoka 2,763 mwaka 2019/2020 hadi 2,348 mwaka 2020/2021 ambapo josho moja lina uwezo wa kuhudumia mifugo 9,500 hadi 18,000 kwa mwaka. Pia, Kliniki 2 za mifugo zimejengwa katika Halmashauri za Babati Mjini na Busekelo.

(ii) **Uzalishaji wa mazao ya mifugo**; mwenendo wa uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo umekuwa ukiongezeka kama ifuatavyo: uzalishaji wa nyama uliongezeka kufikia tani 738,166 mwaka 2020/21 kutoka tani 701,679.1 mwaka 2019/20; jumla ya nyama tani 1,774.29 iliuzwa nje ya nchi mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na nyama tani 692.36 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2019/2020; uingizaji wa nyama nchini umepungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 4.06 (shilingi bilioni 4.06) mwaka 2019/20 hadi Dola za Kimarekani milioni 1.06 (shilingi bilioni 2.4) mwaka 2020/21; zipo machinjio za kisasa na viwanda vya nyama 34 vinavyofanya kazi, machinjio za kisasa na viwanda 7 vinaendelea kujengwa; uzalishaji wa maziwa ni lita bilioni 3.1 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na lita bilioni 3.01 mwaka 2019/20; uzalishaji wa vipande vya ngozi umefikia milioni 11.77 vyenye thamani ya shilingi bilioni 25.93 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na vipande milioni 11.23 vyenye thamani ya shilingi bilioni 22.8 mwaka 2019/20. Aidha, uuzaji wa ngozi nje ya nchi uliongezeka hadi kilo milioni 7.9 zenye thamani ya shilingi bilioni 16.1 mwaka 2020/21 kutoka kilo milioni 6.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 12.9 kwa mwaka 2019/20 na kuongezeka kwa usindikaji wa maziwa kufikia lita milioni 75.9 mwaka 2020/21 kutoka lita milioni 74.3 mwaka 2019/20.

(iii) **Utengaji wa Maeneo ya Malisho;** Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazohusu utengaji na upimaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo malisho ya mifugo. Katika mwaka 2020/2021 Halmashauri za Wilaya kumi na saba (17) zimetenga jumla ya Hekta 271,661.11 kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hivyo, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yameongezeka kufikia hekta 3,060,562.27 mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na hekta 2,788,901.17 katika mwaka 2019/2020.

(iv) **Udhibiti wa magonjwa ya Mifugo;** Jumla ya michovyo ya kuogesha mifugo 446,997,857 imefanyika sawa na asilimia 110 ya lengo la kuogesha mifugo 405,000,000 ambapo michovyo ya ng'ombe ni 342,968,774 mbuzi 89,649,306 na kondoo 14,364,827. Jumla ya dozi 35,474,800 za Chanjo ya Matone ya Ugonjwa wa Mdondo (I2) zimezalishwa na kusambazwa katika mikoa yote. Aidha, jumla ya kuku 57,773,685 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo kwa chanjo ya Matone (35,474,800) ambapo kuku 22,298,885 walichanjwa kwa kutumia chanjo ya maji (Lasota) inayonunuliwa na kusambazwa na sekta binafsi. Jumla ya ng'ombe 1,036,769, mbuzi 680,906 na kondoo 192,906 walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta katika mikoa ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 shilingi bilioni 2.18 zimetumika.

(v) **Kuboresha Huduma ya Uzalishaji Mifugo na Masoko;** Shughuli zilizotekelezwa ni; kuwezeshwa kwa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kupatiwa madume bora nane (8) ya mbegu kutoka nchini Afrika Kusini;

kuhimilishwa kwa ng'ombe 78,575 katika Mikoa ya Dodoma (Kongwa), Katavi (Sumbawanga), Simiyu (Meatu), Geita (Chato na Bukombe), Kagera (Misenyi na Kyerwa), Pwani (Mkuranga na Kisarawe), Lindi (Ruangwa), Mara (Butiama, Musoma, Bunda na Serengeti), Morogoro (Kilosa na Mvomero) na Tanga (Muheza, Tanga Jiji na Korogwe); kuzalishwa na kusambazwa kwa mitamba 18,012 kwa wafugaji; kuzalisha vifaranga vya kuku 88,348,000 nchini; kuongeza idadi ya vituo vya doria vya kimkakati kutoka vituo vitatu (3) vya Lamadi (Busega), Nderema (Handeni) na Makuyuni (Monduli) hadi vituo 10 katika maeneo ya Kyaka (Missenyi), Wasso (Loliondo), Makambako (Njombe), Msolwa (Chalinze), Tunduma (Momba), Darajani (Serengeti) na Buhigwe (Buhigwe); kutolewa kwa mafunzo ya uchunaji ngozi kwa wakaguzi wa ngozi 60 kati ya 113 walioteuliwa; kukamilika kwa ukarabati wa minada ya Igunga, Nata, Ipuli, Kirumi, Kizota, Pugu na Murusagamba na kuendelea na ujenzi wa mnada wa Buzirayombo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 83. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 shilingi bilioni 3.2 zimetumika.

(vi) **Kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo:** Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kisima kirefu katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Usolanga) ambapo utekelezaji umekamilika kwa takriban asilimia 100; kukamilika kwa ukarabati wa mabwawa matatu (3) ya Chamakweza (Chalinze), Kimokoua (Longido), Narakauo (Simanjiro); kutolewa kwa mafunzo rejea kwa wakaguzi 66 wa ubora na usalama wa vyakula vya mifugo katika mikoa ya Morogoro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Mara, Geita, Shinyanga, Iringa, Njombe, Mbeya na Ruvuma; kusajiliwa kwa maeneo 45 ya kuzalisha, 78 kuuza na 18 kuhifadhia rasilimali za vyakula vya mifugo. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 shilingi bilioni 1.6 zilitumika.

164. **Uendelezaji wa Sekta ya Uvuvi:** Serikali iliendelea na hatua za kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uandaaji wa muundo wa shirika na ukarabati wa jengo la ofisi la makao makuu Dar es Salaam. Tafiti mbalimbali za uvuvi zimefanyika ikiwa ni pamoja na Utafiti wa Pweza na mazingira yake, kupunguza upotevu baada ya mavuno, kuchunguza virutubisho vilivyomo kwenye samaki aina ya Jodari kwa afya ya binadamu, kutambua maeneo ya uvuvi na wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Victoria. Aidha, Serikali imetoa mafunzo kwa wadau 3,573 wa uvuvi kuhusu masuala ya uendeshaji boti kwa usalama; mbinu bora za uvuvi endelevu; ufugaji wa samaki kibiashara; utunzaji wa mazingira na baioanuai katika maji; uhifadhi, ubora na uchakataji samaki viwandani; na mbinu za upunguzaji wa upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa.

165. Serikali imehamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika ukuzaji viumbe maji ambapo hadi sasa kuna vitotoleshi vya vifaranga vya samaki 27 vyenye uwezo wa kuzalisha takribani vifaranga milioni 25 kwa mwaka, viwanda 11 vya kutengeneza chakula cha samaki vyenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani 500 kwa mwaka na vizimba 471 vya kufugia samaki vyenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani 3,000 kwa mwaka. Uendelezaji wa uvuvi katika maeneo mengine ni kama ifuatavyo:-

(i) **Ununuzi wa Meli za Uvuvi:** Serikali iliendelea na utaratibu wa ununuzi wa meli tatu (3) za uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 12.9. Meli hizo zinazotarajiwa kufika nchini mwaka 2022 na zitatumika katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu.

(ii) **Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi:** Serikali iliendelea na upembuzi yakinifu ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi. Ujenzi wa bandari hiyo utachochea fursa za uwekezaji katika shughuli za uvuvi na kuzalisha ajira takribani 30,000.

(iii) **Ujenzi wa Mialo, Masoko, Maabara na Ofisi:** Serikali ilikamilisha ujenzi wa soko jipya la samaki katika mwalo wa Mbamba-Bay (Nyasa), maabara ya utafiti wa uvuvi Dar es Salaam na ofisi tano (5) za Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Halmashauri tano (5) za Mkinga, Pangani, Chalinze, Bagamoyo na Lindi Vijijini. Aidha, Serikali imekarabati mialo mitano (5) ya Ihale (Busega), New Igombe na Kayenze (Ilemela), Igabilo (Bukoba), na Chifunfu - Kijiweni (Sengerema). Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 4.7 zimetumika.

166. **Uendelezaji wa Sekta ya Madini:** Katika mwaka 2020/21 Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini na kukamilisha: ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kusafisha dhahabu kilo 480 kwa siku kwa kiwango cha kimataifa (999.9 *purity*) kilichopo Mwanza; ujenzi wa vituo vya umahiri wa mashapo, uchimbaji na uchenjuaji madini vya Chunya, Songea na Mpanda; ujenzi wa kituo cha huduma ya pamoja Mirerani; mafunzo kwa wachimbaji wadogo 10,338; mkataba wa nyongeza wa kandarasi za uchorongaji wa kutafuta dhahabu Geita Gold Mine na kutafuta joto ardhi yenye thamani ya shilingi bilioni 17.5; ununuzi wa mitambo minne (4) ya kuchoronga miamba ya thamani ya shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya STAMICO; na kuendelea na ujenzi wa makao makuu na ununuzi wa magari na vitendea kazi mbalimbali ambayo imegharimu shilingi bilioni 11.7. Aidha, Serikali iliweza kununua vipande vikubwa vitatu vya tanzanite vyenye thamani ya shilingi bilioni 12 kutoka kwa wachimbaji wadogo wa migodi ya tanzanite Mirerani.

167. Uanzishwaji wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini umewezesha kuimarisha udhibiti wa utoroshaji wa madini na hivyo kuongezeka kwa ajira na

mapato. Ushiriki wa Serikali katika shughuli za uwekezaji kupitia Kampuni ya *Twiga Minerals Corporation Limited* umewezesha kupatikana kwa gawio la shilingi bilioni 100. Serikali ilitoa leseni 6,389 za utafutaji, uchimbaji mdogo, uchimbaji wa kati, uchenjuaji, uyeyushaji na biashara ya madini; na kufuta kodi ya Ongezeko la Thamani na Kodi ya Zuio kwa wachimbaji wadogo. Kutokana na jitihada hizo, mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 5.2 mwaka 2019 hadi asilimia 6.7 mwaka 2020 na mapato yasiyo ya kodi ya madini yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 588.04 sawa na asilimia 111.64 ya lengo la makusanyo ya shilingi bilioni 526.72. Jumla ya shilingi bilioni 19.72 zimetumika kwa mwaka 2020/21 na shilingi milioni 302.1 zimetolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

168. **Uboreshaji wa Huduma za Maji:** Katika kuendeleza sekta ya maji nchini kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama pamoja na kusimamia usafi wa mazingira na maji taka kwa mwaka 2020/21, Serikali ilitoa shilingi bilioni 495.3 kwa ajili ya kusimamia uendelezaji na utekelezaji wa miradi na programu za maji zikiwemo:

(i) **Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**: Rasilimali za maji nchini zinasimamiwa na kuendelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa ambazo zina majukumu ya kutathmini na kufuatilia rasilimali hizo; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji. Katika kutekeleza majukumu hayo, Serikali imejenga na kukarabati vituo 159 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji; kuweka mipaka katika vyanzo vya maji 25; na kutoa vibali vya matumizi ya maji 1,096. Vilevile, Serikali imeendelea na mpango wa ujenzi wa miradi ya kimkakati ya mabwawa ya Farkwa (Dodoma), Lugoda/Ndembera (Iringa), Songwe (Songwe), Kidunda (Morogoro) na Bwawa la Dongo (Manyara). Usanifu wa Mabwawa hayo umekamilika na sehemu ya fidia ya kiasi cha Shilingi bilioni 18.5 kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mabwawa ya Farkwa na Kidunda imelipwa. Kwa upande wa Bwawa la Kidunda, visima vya maji vimechimbwa katika maeneo ambayo wananchi waliopisha ujenzi wa bwawa hilo wamehamishiwa. Aidha, Serikali imekamilisha ukarabati wa bwawa la Mwadila lililopo Wilaya ya Maswa mkoa wa Simiyu.

(ii) **Uboreshaji wa Huduma za Maji Mijini na Vijijini:** Hadi Juni 2021, miradi ya maji 750 ilikamilika na kuanza kutoa huduma. Kati ya miradi hiyo, miradi 666 yenye vituo 11,421 vya kuchotea maji inahudumia wananchi 3,828,180 vijijini na miradi 84 ya mijini inahudumia wakazi 2,418,641. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Isaka, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega; Mradi wa kuboresha

huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza; na Mradi wa maji kutoka Ruvu Juu kupeleka Mji wa Kisarawe. Aidha, miradi 115 kati ya 177 ambayo haikukamilika kwa wakati na mingine iliyokamilika bila kutoa huduma ya maji ilipatiwa ufumbuzi na imeanza kutoa huduma ya maji. Miradi hiyo ni pamoja na miradi ya maji ya Ntomoko – Dodoma, Nyamtukuza – Geita, Mibono – Tabora, Rugeye – Mwanza, Malinyi – Morogoro, Muze *group* – Rukwa, Kinesi – Mara na Imalabupina - Ichwankima – Geita. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa asilimia 72.3 na mijini asilimia 86. Vilevile, utekelezaji wa Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha unaendelea na umefikia asilimia 68.

(iii) **Ubora wa maji:** Serikali imeboresha maabara za Dar es Salaam, Singida, Shinyanga, Musoma, Bukoba na Kigoma ambazo zimepata ithibati na kukidhi viwango vya kimataifa vya upimaji wa ubora wa maji hivyo kuongeza idadi ya maabara za ubora wa maji zenye ithibati nchini kutoka moja (1) ya Mwanza hadi saba (7).

169. **Uimarishaji wa Elimu na Mafunzo**: Serikali iliendelea kuboresha utoaji wa huduma ya elimumsingi, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

(i) **Elimumsingi:** Shilingi bilioni 249.6 zimetumika kugharamia Programu ya Elimumsingi Bila Ada na kuwezesha uandikishwaji wa wanafunzi wapya 1,198,564 wa elimu ya awali; 1,549,279 wa darasa la kwanza na usajili wa wanafunzi 721,425 wa kidato cha kwanza sawa na asilimia 87 ya wanafunzi 833,872 waliofaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka 2020. Aidha, Serikali iliendelea na uimarishaji wa miundombinu ya shule kwa kukamilisha ujenzi wa: vyumba vya madarasa 5,524; maabara za sayansi 1,422; matundu ya vyoo 24,667; nyumba za walimu 31; mabweni 112; mabwalo 6 na ofisi za walimu 4 ambapo hadi Juni 2021 shilingi bilioni 193.2 zilitumika. Vilevile, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali ilitoa shilingi bilioni 62.41 kwa ajili ya kugharamia Elimumsingi Bila Ada na shilingi bilioni 7.0 kutokana na makusanyo ya tozo ya miamala ya simu kwa ajili ya umaliziaji wa maboma 560 katika shule za sekondari 365;

(ii) **Uchapaji na Usambazaji wa Vitabu na Miongozo**: Serikali imechapa na kusambaza vitabu na miongozo mbalimbali ikiwemo nakala 4,925,864 za vitabu vya kiada kwa wanafunzi wa darasa la VI na VII na wanafunzi wenye mahitaji maalum; nakala 253,968 za Kiongozi cha Mwalimu Darasa la VII; nakala 349,368 za mtaala na mihtasari kwa ajili ya shule za msingi; na nakala 2,000 za Mwongozo wa Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum Tanzania Bara na Zanzibar

na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule 1,418. Vitabu na Miongozo imesambazwa katika Halmashauri zote nchini. Hadi Juni, 2021 shilingi bilioni 46.2 zilitumika;

(iii) Kuanza upya ujenzi wa vyuo vitatu (3) vya ualimu ambavyo ni Dakawa, Muhonda na Sumbawanga; shule ya sekondari ya mfano Dodoma; na ukarabati wa vyuo saba vya ualimu. Hadi Juni 2021, shilingi bilioni 36.0 zilitumika;

(iv) Serikali imeajiri jumla ya walimu 14,949 ambapo kati ya hao, 6,300 ni wa shule za sekondari na 8,649 ni wa shule za msingi;

(v) **Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**: Serikali ilikamilisha ujenzi wa vyuo vitano (4) na upanuzi wa vyuo vinne (4) vya Ufundi Stadi vya Wilaya; kuandaa mitaala tisa (9) na ambavyo ni: Ileje, Mabalaga, Paramawe, Chekileni, Ndolage, Nyamidaho, Kanadi, Samunge na Golowa. Aidha, mitaala 11 imehuiswa kulingana na mahitaji ya soko la ajira; kuanzishwa kwa Kituo cha Kitaifa cha Atamizi kwa ajili ya Ubunifu na Ujasiriamali (NICIE); kufanya pimaji kwa wanagenzi 10,178 ambapo wanagenzi 9,736 walishinda pimaji na kupata vyeti vya utambuzi (Recognition of Prior Learning); kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa vijana takribani 6,000; kuwezesha vijana 23,844 kukuza ujuzi kupitia programu ya Mifuko ya Maendeleo ya Ujuzi; na wanafunzi 380,748 walidahiliwa katika mafunzo ya Ufundi Stadi na wanafunzi 157,420 katika mafunzo ya ufundi. Hadi Juni 2021, kiasi cha shilingi bilioni 71 kimetumika. Vilevile, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali imeanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa chuo cha ufundi Dodoma kitakachokuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 3,000 ambapo shilingi bilioni 1.7 zimetolewa.

(vi) **Elimu ya Juu:** Hadi Juni 2021, Serikali ilitoa mikopo kwa wanafunzi 149,472 yenye thamani ya shilingi bilioni 415.0 na kukusanya mikopo iliyoiva ya shilingi bilioni 163.8. Aidha, Serikali ilikamilisha sehemu ya bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 352 katika Chuo Kikuu cha Ardhi; maabara ya Kemia na hosteli za wanafunzi katika Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Miradi mingine ni kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Umahiri wa Kutibu Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; maabara changamano (multi purpose laboratory) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo; na jengo la Shule Kuu tarajiwa ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vilevile, Serikali iliendelea na upanuzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe na Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Aidha, jumla ya wanafunzi 87,934

wa mwaka wa kwanza katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu walidahiliwa. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya 2021/22, shilingi bilioni 50.3 zilitolewa.

(vii) **Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**: Hadi Juni 2021, Serikali imetekeleza yafuatayo: kutambua na kuhakiki teknolojia 79 zilizozalishwa na kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa nchini kufikia 389; kuendeleza wabunifu 130 waliopatikana katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambapo bunifu 26 zipo katika hatua ya kubiasharishwa; kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wathibiti Ubora wa shule katika mikoa 26 ya namna ya kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu; kutoa mafunzo, fedha za utafiti na ubunifu kwa miradi 204 inayoendelea na vibali vya utafiti 576 kwa miradi mipya ya utafiti; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara na karakana kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani za Sayansi na Teknolojia; ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na Maktaba kwa awamu ya pili katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; na kuendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili katika Tume ya Nguvu za Atomiki. Hadi Juni 2021, shilingi bilioni 16.4 zimetumika.

170. **Uimarishaji wa Huduma za Afya**: Serikali iliendelea kuboresha huduma za afya nchini katika ngazi zote kama ifuatavyo:

(i) **Huduma za Afya ya Msingi:** Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali za Halmashauri 102 ambapo Hospitali 3 za; Jiji la Arusha, Jiji la Mwanza na Hospitali ya Manispaa ya Kinondoni (Mabwepande) zinajengwa kwa mapato ya ndani. Hospitali 67 zilianza ujenzi katika awamu ya kwanza, Hospitali 27 awamu ya pili na Hospitali 5; Hospitali ya UHURU, Hospitali ya Tunduma, Hospitali ya Kyela, Ubungo na Misungwi zilianza ujenzi kwa maombi maalumu; ujenzi wa Vituo vya afya 71; ukarabati wa Zahanati 289 na ukamilishaji wa maboma ya Zahanati 555. Jumla ya Shilingi bilioni 131.8 zimetumika kwa mwaka 2020/21. Aidha, katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi bilioni 37.5 zilizotokana na tozo ya miamala ya simu zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 150 kwenye tarafa zisizokuwa na vituo vya afya.

(ii) **Huduma za Rufaa:** Serikali iliendelea na ujenzi wa Hospitali mpya za mikoa sita (6) (Katavi, Geita, Simiyu, Songwe, Njombe na Mara); Hospitali mbili (2) mpya za rufaa za Kanda (Burigi - Chato na Mtwara). Aidha, ukarabati na upanuzi wa hospitali 16 za rufaa za mikoa upo katika hatua mbalimbali. Vilevile, ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya uliendelea kufanyika katika hospitali za rufaa za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Kanda ya Ziwa Bugando na Kanda ya Kaskazini KCMC. Hadi

Juni 2021, jumla ya shilingi bilioni 37.4 zimetumika.

(iii) **Huduma za Kibingwa**: Serikali iliendelea na uimarishaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa kuwajengea uwezo katika fani mbalimbali wataalamu 642 kati ya 1,098 ya madaktari bingwa na ubingwa bobezi waliopo nchini. Aidha, katika kipindi hicho, vifaa tiba vya kisasa vilinunuliwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na *Ocean Road Cancer Institute*, ambapo ununuzi wa vifaa hivyo ulienda sambamba na ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Jitihada hizo, zimewezesha kuongezeka kwa huduma za kibingwa kwa wananchi na kuanza kupata wagonjwa kutoka nje ya nchi ambapo katika mwaka 2020/21 wagonjwa waliopatiwa matibabu kutoka nje ya nchi walikuwa 55. Hadi Juni 2021, shilingi bilioni 15.8 zimetumika.

(iv) **Rasilimali watu:** Serikali iliajiri watumishi 4,598 katika sekta ya Afya wa kada mbalimbali ikiwemo madaktari bingwa 5, madaktari 113, matabibu 725, wauguzi 914, wasaidizi wa afya 843, wateknolojia 229 na wafamasia 11. Uwepo wa watumishi hao umewezesha kuboresha utoaji huduma kwa ufanisi katika maeneo mbalimbali nchini.

(v) **Ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi:** Hadi Juni 2021, shilingi bilioni 260.9 zilitumika kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya mipakani. Hatua hii iliwezesha upatikanaji wa dawa muhimu aina 312 kufikia asilimia 80.

(vi) **Huduma za Chanjo:** Serikali iliendelea kuboresha huduma za chanjo muhimu kwa asilimia 100 kwa kuchanja watoto, akina mama wajawazito na wasichana ambapo shilingi bilioni 32 zilitumika. Aidha, Serikali ilipokea chanjo 1,023,400 ya UVIKO-19 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo viongozi wakuu wa serikali na viongozi wa dini walipata chanjo wakati wa uzinduzi kama sehemu ya kuanza utoaji na uhamasishaji wa wananchi kupata chanjo.

(vii) **Huduma za Tiba Asili na Mbadala**: Serikali iliimarisha afua za afya za Tiba Asili na Tiba mbadala ikiwemo kufanya utafiti wa dawa na kusajili dawa 42 zikiwemo zinazotumika kupambana na UVIKO-19, usajili wa waganga 2,142, usajili wa maduka na vituo 210 na mafunzo ya kujiendeleza kwa waganga 81. Waganga na watengeneza dawa walishiriki katika maonesho ya wiki ya Tiba Asili ya Mwafrika yaliyofanyika mjini Dodoma ambapo dawa 65 za Tiba Asili na Tiba mbadala zilioneshwa.

(viii) **Kliniki Tembezi (Mobile Clinic):** Serikali ilitumia shilingi bilioni 4.0 kununua Magari matano (5) yatakayotoa huduma za Kliniki Tembezi zinazojumuisha upimaji na tiba ya ugonjwa wa Kifua Kikuu. Aidha, kliniki

hizo zitatumika kutoa huduma za upimaji wa magonjwa kama vile UKIMWI, Kisukari, mapafu na magonjwa mengine. Magari hayo yamesambazwa katika Kanda tano (5) ambazo ni: Kanda ya Ziwa (Hospitali ya Kanda Bugando), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Hospitali ya Kanda Mbeya), Kanda ya Kati (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma), Kaskazini (Hospitali ya Taifa ya Tiba ya magonjwa ambukizi Kibong'oto) na Mashariki (Maabara Kuu ya Taifa ya Kifua Kikuu - Muhimbili).

171. **Uendelezaji wa Sekta ya Viwanda na Biashara:** Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo: makaa ya mawe Mchuchuma na chuma Liganga ambapo zoezi la uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha ujenzi limekamilika; ujenzi wa Kongano ya Viwanda vya Ngozi katika eneo la Zuzu Mkoani Dodoma (Leather Cluster); ufungaji wa mashine za kisasa katika viwanda vya *ACE Leather* cha Morogoro na *Kilimanjaro International Leather;* na kukamilisha upembuzi yakinifu wa Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka. Aidha, Serikali iliendelea na ukamilishaji, mapitio, tathmini na utunzi wa sera zifuatazo: Sera ya Taifa ya Ubora; Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP, 1996- 2020); na Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003. Vilevile, leseni za makampuni mapya 12 zilitolewa na kusajiliwa kwa utaratibu wa EPZ na SEZ. Katika mwaka 2020/21 shilingi bilioni 46.5 zilitumika.

172. **Uboreshaji wa Sekta ya Maliasili na Utalii**: Serikali iliendelea kusimamia, kulinda maliasili na kuendeleza shughuli za utalii kwa kufanya yafuatayo: Kuimarishwa kwa uhifadhi kwa kutokomeza matukio ya ujangili wa wanyamapori kwa asilimia 90; kuimarishwa kwa ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi katika kazi za uhifadhi na uwekezaji wa rasilimali za maliasili, malikale na utalii; kuimairshwa kwa ulinzi wa jamii inayoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu; na kuimarishwa kwa shughuli za upatikanaji wa mazao ya misitu na yuki na thamani ya mnyororo wake. Shughuli nyingine zilizofanyika ni:- Kuboresha miundombinu ya huduma za utalii kwa kujenga barabara km 73.4 na kukarabati km 8,599.8; kujenga kambi za kitalii na nyumba za kulala wageni zenye jumla ya vitanda 670; kujenga njia za utalii wa kutembea kwa miguu zenye urefu wa km 927; kuendelea kutumia ofisi za balozi na mabalozi wa utalii wa hiari kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini; na kupunguza ada ya leseni za wakala wa tiketi za ndege nchini kutoka Dola za Marekani 2,000 hadi 500. Jitahada hizi zimehamasisha na kuvutia watalii 620,867 wakimataifa na watalii 571,353 wa ndani na kuongeza ushiriki wa Watanzania katika biashara na shughuli za utalii katika kipindi cha UVIKO - 19. Vilevile, Serikali iliendelea kuratibu uandaaji wa Makala maalum inayojulikana kama *Royal Tour* kwa lengo la kuitangaza Tanzania Duniani.

173. Serikali iliendelea kutumia michezo kutangaza na kuhamasisha utalii nchini ambapo yafuatayo yamefanyika: kuanzisha mashindano ya ndondi yanayohusisha mabondia wa kigeni na wa ndani ambapo washabiki huhamasika kutembelea tovuti ambazo huitangaza nchi yetu; kutumia Vilabu vya Soka vya Mpira wa Miguu vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini kupitia matangazo yaliyo kwenye Jezi; na kutumia washindi wa mashindano ya urembo kutangaza vivutio vya kitalii wanapowakilisha nchi kwenye mashindano ya Kimatafa.

174. Serikali iliendelea kuimarisha mfumo wa Jeshi Usu; kutoa mafunzo ya uhifadhi wa maliasili za wanyamapori, misitu na nyuki kwa watumishi 6,706; kudhibiti mimea vamizi hekta 7,570 katika eneo la Kreta ya Ngorongoro na hifadhi za Taifa; kuongezeka kwa hifadhi ya misitu ya mazingira asilia kutoka 19 hadi 20 kwa kupandishwa hadhi msitu wa Essmingori; kupandishwa hadhi maeneo 30 mapya ya misitu yenye ukubwa wa hekta 139,969 kuwa hifadhi; kuongeza hifadhi za nyuki kutoka moja (1) hadi saba (7) na kuanzisha mashamba mapya mawili (2) ya miti ya Makere Kusini lenye hekta 30,000 na Mwanhala lenye hekta 3,000. Hadi Juni 2021, shilingi bilioni 40.3 zimetumika na kwa robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi milioni 106.0 zimetolewa.

175. **Uboreshaji wa Huduma za Mahakama:** Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu Sumbawanga; Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi; nyumba za Mahakimu Loliondo; Jengo la Kuhifadhia Kumbukumbu - Tanga; na Mahakama za Wilaya Rungwe, Chemba, Bahi Wanging'ombe na Makete. Miradi mingine iliyoendelea kutekelezwa ni pamoja na: Ujenzi wa jengo la makao makuu ya Mahakama Dodoma; Mahakama ya Hakimu Mkazi Lindi; Mahakama za Wilaya Sikonge, Kilindi, na Bunda; Mahakama za mwanzo Mlimba na Mang'ula; Ujenzi wa majengo sita ya vituo jumuishi vya kutoa ushauri wa kisheria Arusha, Dodoma, Dar es Salaam (Temeke na Kinondoni), Mwanza na Morogoro. Aidha, Serikali iliendelea kuboresha mfumo wa kielekroniki wa usimamizi wa mashauri. Hadi Juni 2021, shilingi bilioni 76.0 zilitumika na kwa robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi bilioni 6.3 zimetolewa.

176. Katika mwaka 2020/21 Serikali ilendelea kuboresha huduma za mahakama kwa kutumia mahakama zinazotembea katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza ambapo mashauri 484 sawa na asilimia 88.2 ya mashauri yaliyofunguliwa kwa mkoa wa Dar es Salaam na mashauri 286 sawa na asilimia 92 ya mashauri yaliyofunguliwa kwa mkoa wa Mwanza yalimalizika. Aidha, kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, Serikali kwa kutumia mahakama inayotembea imefanikiwa kumaliza jumla ya mashauri 150 sawa na asilimia 61.2 ya mashauri yaliyofunguliwa

katika mikoa hiyo.

177. **Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato Katika Halmashauri:** Serikali ilikamilisha ujenzi wa miradi 12 kati ya miradi 38 ambayo ni: Ujenzi wa Soko la Kisasa la Chifu Kingalu - Morogoro, Soko la Mpakani Muhange – Kakonko, Soko la Mburahati, Kisutu na Magomeni; Ghala la Kuhifadhia Mazao Ruangwa; Kituo cha Mabasi cha Magufuli na Stendi ya Mangaka; Machinjio ya Kisasa ya Vingunguti; Maegesho ya Malori Mpakani mwa Tanzania na Rwanda; na Kiwanda cha Chaki na Vifungashio Maswa. Miradi hiyo itaziwezesha Halmashauri kuzalisha mapato na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi. Aidha, miradi mingine 26 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hadi Juni 2021, jumla ya shilingi bilioni 81.4 zimetumika.

178. **Majengo ya Utawala ya Halmashauri**: Serikali ilikamilisha ujenzi wa Ofisi mpya saba (7) za Halmashauri za Wilaya ya Chalinze, Kibaha, Buchosa, Malinyi, Itigi, Ikungi na Mji Makambako na inaendelea na ukamilishaji wa majengo 87. Hadi Juni 2021, kiasi cha shilingi bilioni 77.3 zilitumika.

1.2.3 Mafanikio mengine yaliyopatikana

179. **Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2020:** Serikali ilisimamia na kuratibu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 katika majimbo 264 na kata 3,953. Kiasi cha shilingi bilioni 268.5 fedha za ndani zilitumika. Aidha, katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 shilingi bilioni 3.7 zimetolewa kugharamia uchaguzi mdogo katika majimbo mbalimbali.

180. **Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo:** Kwa mwaka 2020/21, jumla ya shilingi bilioni 13.0 zilitumika kwa ajili ya Majimbo yote ya Uchaguzi ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na; kuchangia ukamilishaji wa miradi ya huduma za jamii katika sekta mbalimbali zikiwemo elimu, afya, maji na ustawi wa jamii.

181. **Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji pamoja na Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (Blueprint):** Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali iliendelea kuboresha mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini kwa kutekeleza yafuatayo: kupunguza jumla ya ada na tozo 60 ambazo zilikuwa zinatozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea; kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo ya Ushindani, Bodi ya Sukari, Makampuni, Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, Serikali imefanya marekebisho ya sheria ya Tume ya Ushindani kwa kuondoa kifungu cha 60, kinachohusu adhabu ya makosa ya ushindani ili ihusishe tu pato ghafi lililopatikana ndani ya Tanzania Bara na si duniani kote kama

husika inapofanya shughuli zake za kibiashara. Hii iliwezesha kuondoa migogoro ya makampuni yanayofanya shughuli zake kwenye sekta ya Kilimo cha Tumbaku na sekta nyingine, ambapo mengine yalikwisha kufunga viwanda kutokana na changamoto ya sheria hii. Vilevile, Serikali imefanya maboresho kwenye sheria ya makampuni kwa kufuta kifungu cha 16(2) ili kuondoa takwa la kugongewa muhuri na Kamishna wa Viapo wakati wa kufungua kampuni na kuhuisha usajili. Kifungu cha 14(4) kinatosheleza matakwa yote hayo na hivyo hatua hii itapunguza urasimu na gharama za kupata tamko la kutimiza matakwa ya kisheria (Declaration of Competence).

182. Serikali imefanya maboresho kwenye sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Sura 427 kwa kupunguza ada na tozo mbalimbali, ikiwemo tozo ya cheti cha umahiri (Certificate of Competence) inayotozwa na wauzaji vifaa vya zimamoto na uokoaji kukoka shilingi 500,000 hadi shilingi 200,000; Kupunguza tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye maeneo ya uchimbaji madini yenye ukubwa usiozidi mita za mraba 2,000 kutoka shillingi 6,000,000 hadi shillingi laki moja 100,000; Kupunguza tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye maeneo ya uchimbaki madini yenye ukubwa kati ya mita za mraba 2001 hadi 4000 kutoka shilingi 6,000,0000 hadi shillingi 150,000; kupunguza tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye maeneo ya uchimbaji madini yenye ukubwa kati ya mita za mraba 4001 hadi 9000 kutoka Shillingi 6000,000 hadi 200,000. Maboresho haya yalilenga kuimairisha mazingira ya biashara rafiki na kuwezesha sheria husika kutekelezeka.

183. Serikali imefanya marekebisho kwenye Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263 kwa kupunguza kiwango cha Mchango wa Sekta Binafsi kutoka asilimia 1.0 inayotozwa sasa hadi asilimia 0.6 ya mapato ghafi ya wafanyakazi ili kutoa unafuu na kujenga mazingira mazuri ya ufanyaji biashara Tanzania. Maeneo mengine sheria zilizofanyiwa maboresho zinagusa sekta ya uvuvi, mifugo, maliasili na utalii na sheria ya kazi. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuuganisha mifumo ya kietroniki katika mamlaka za udhibiti ikiwemo mifumo wa *Integrated Standard and Meteology System* (ISQMT) ndani ya TBS ambao unahudumia sekta binafsi hasa katika utaoji wa leseni na vibali; na TRA *Electronic Filling System; Improvement of Mining Cadastre System*. Aidha, maboresho yamefanyika kwenye mfumo wa usajili wa makampuni na utoaji huduma nyingine za BRELA na mfumo wa Pamoja wa Kietroniki wa uondoshaji shehena katika Bandari na Mipaka (Eletronic Single Window) unaojumuisha mamlaka mbalimbali ambapo maboresho hayo yako katika hatua za mwisho kuwezesha mifumo hiyo kufanya kazi kwa ujumla. Hivyo, ujenzi na uboreshaji wa mifumo hiyo ulipelekea kuwa na mamlaka za udhibiti zinazotoa huduma za vibali na leseni kwa njia za mtandao kufikia 42 katika mwaka 2020/21.

184. **Programu ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi:** Programu ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi: Hatua mbalimbali za utekelezaji wa Programu ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ni kama ifuatavyo: Kukamilisha uanzishwaji wa Kituo cha Ubia (PPP Center) na kuendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ambapo, miradi mitano (5) ipo katika hatua ya kutafuta wabia: -sekta ya afya (3), Usafirishaji (1), na Uchukuzi (2). Aidha, miradi 19 ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu: sekta za afya (1), nishati (1), elimu (2), uchukuzi (3), biashara/masoko (9) na mazingira (3). Miradi mitatu (3) ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu wa awali ambapo miradi miwili (2) ni ya sekta ya elimu na mmoja (1) ni wa mazingira; na miradi 14 ipo katika hatua ya andiko dhana katika sekta za ujenzi (3), uchukuzi (3), elimu (3), afya (1) na maji (4). Vile vile, Mamlaka za Serikali zimepokea mapendekezo kutoka kwa wawekezaji mbalimbali katika sekta za nishati, ujenzi na viwanda ambayo yanafanyiwa uchambuzi kwa mujibu wa Sheria ya PPP.

185. **Uboreshaji wa Sekta ya Fedha**

Katika kuendeleza Sekta ya Fedha kwa mwaka 2020/21, mafanikio yafuatayo yamepatikana: -

(i) **Sekta ya benki:** Hadi Juni 2021, uwiano wa mali zinazobadilishika kiurahisi kuwa fedha na amana za wateja wa benki (Liquid Assets to Demand Liabilities) ulikuwa asilimia 33.25 ukilinganisha na asilimia 33.37 Juni 2020; mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 4.1, ukilinganisha na asilimia 5.5 ya Juni 2020; uwiano wa mikopo chechefu ulikuwa ni asilimia 9.30 ukilinganishwa na asilimia 10.84 mwezi Juni 2020 ambao ni juu ya kiwango kinachokubalika na Benki cha asilimia 5; riba za mikopo katika benki za biashara zilifikia asilimia 16.60 kwa mwaka ulioshia Juni 2021 ikilinganishwa na asilimia 16.78 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20; faida katika Sekta ya benki kabla ya kodi kwa wastani wa mali, ilikuwa asilimia 2.42 mwezi Juni 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.19 mwezi Juni 2020; na uwiano wa faida baada ya kodi kwa wastani wa fedha za wanahisa uliongezeka kufikia asilimia 10.47 ikilinganishwa na asilimia 9.88 mwezi Juni 2020.

(ii) **Masoko ya mitaji na dhamana:** Serikali imetoa leseni 144 kwa watendaji na washauri wa uwekezaji; kuidhinisha na kuuza hisa 230,818,216 zenye thamani ya shilingi bilioni 457.7; na mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani kufikia Agosti 2021 uliongezeka kwa asilimia 4.03 na kufikia shilingi trilioni 9.56 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9,190.0 Agosti 2020. Hii ilichangia mtaji wa jumla wa Soko la Hisa kuongezeka kwa asilimia 9.49 na kufikia shilingi bilioni 1,661.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,517.0 Agosti 2020.

(iii) **Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**: Wanachama wapya 235,556 walisajiliwa

ikilinganishwa na wanachama 213,384 waliosajiliwa mwaka 2019/20; kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 2,570.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,440.0 iliyokusanywa 2019/20; na kulipa shilingi bilioni 2,500.0 kwa wastaafu na wanufaika wengine ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,100.0 zilizolipa mwala 2019/20.

(iv) **Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF):**Waajiri wapya 2,289 walisajiliwa katika mwaka 2020/21 ikilinganishwa na waajiri 2,691 waliosajiliwa 2019/20 na hivyo kufanya jumla ya waajiri waliosajiliwa na Mfuko kufikia 25,085; michango ya waajiri ilifikia jumla ya shilingi bilioni 106.93 ikilinganishwa na shilingi bilioni 106.44 za 2019/20; na kiasi cha shilingi bilioni 12.43 kilitumika kwa mwaka 2020/21 kulipia matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki kutokana na kazi ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.09 zilizotumika mwaka 2019/20.

(v) **Bima:** Hadi Juni 2021, Serikali ilisajili kampuni za bima 29, kampuni ya bima mtawanyo moja (1), madalali wa bima 64, madalali wa bima mtawanyo wanne (4), mawakala wa bima 839, wakadiriaji hasara 50, na benki - wakala wa bima 13 ikilinganishwa na kampuni za bima 32, za udalali 77, wakala wa bima 756 na wakadiriaji hasara 60 waliokuwepo kufikia Juni 2020.

(vi) **Huduma Jumuishi za Fedha:** Jumla ya leseni 549 zimetolewa kwa kampuni za huduma ndogo za fedha zisizopokea amana; usajili wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 460 na Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za kifedha 11,149; kukamilika kwa Mpango wa Elimu ya Fedha wa Mwaka 2021 - 2025 na nyenzo za kufundishia elimu ya fedha kwa umma; na kuanzisha mfumo wa kielekroniki wa utoaji leseni kwa kampuni za huduma ndogo za fedha daraja la pili na SACCOS. Aidha, Mango Jumuishi wa Huduma za Fedha umefanikisha yafuatayo: kuundwa kwa kamati ya wanawake ya huduma jumuishi za fedha; kukamilika kwa Mwongozo wa Kutoa Elimu ya Fedha na Nyenzo ya Kufundishia; na kukamilisha Rasimu ya Mpango wa Taifa wa Kumlinda Mlaji wa Huduma za Fedha.

186. **Usimamizi wa Sekta ya Ardhi**

Serikali iliendelea na mikakati mbalimbali ya usimamizi, kupanga, kupima pamoja na kusogeza huduma za umilikishaji wa ardhi kwa jamii kwa kufanya yafuatayo:-

(i) **Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi:** Serikali imetekeleza yafuatayo: kusajili vyeti vya ardhi vya vijiji 195 na kufanya jumla ya vijiji vilivyopimwa na kupewa vyeti vya ardhi kufikia 10,762; kutoa hatimiliki 56,391, miamala na nyaraka za kisheria 84,651 na hati 632 za umiliki wa sehemu ya jengo; kuendelea na upangaji, upimaji na umilikishaji viwanja 87,636 katika Halmashauri 23; utambuzi wa vipande vya ardhi 63,437 umefanyika katika Halmashauri za Majiji, Manispaa na Wilaya Mwanza (12,927), Arusha

(14,364), Mbeya (25,749), Meru (3,050), Misungwi (2,236) na Sumbawanga (5,111) na leseni za makazi 3,008 zimetolewa; michoro ya mipango miji 890 yenye jumla ya viwanja 423,918, ramani za upimaji 4,300 zenye jumla ya viwanja 242,000 imebadilishwa kutoka mfumo wa analogia kwenda mfumo wa digitali ili itumike katika mfumo unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) ulioboreshwa; mwongozo wa utambuzi wa kila kipande cha ardhi na utoaji leseni umeandaliwa; utoaji elimu kuhusu sheria za ardhi katika Halmashauri 39; uchongaji wa barabara katika eneo la mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam; kurasimishwa kwa viwanja 760,092 mijini katika halmashauri mbalimbali nchini; uthamini wa eneo lenye ukubwa wa ekari 458.02 katika kitongoji cha Mawelewele, Bihawana katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma umefanyika na fidia imelipwa; na kununuliwa kwa vitendea kazi mbalimbali vikiwemo vifaa kwa ajili ya kituo cha Taarifa za Ardhi – NLIC kilichopo Dar es Salaam kwa ajili ya kuongeza uwezo (storage system) wa kituo na hivyo kuboresha ufanisi wa utendaji kazi.

(ii) **Upimaji wa Mipaka ya Kimataifa:** Kufanyika kwa vikao vya wataalamu kati ya Tanzania na nchi za Kenya na Burundi ambapo makubaliano yalikuwa ni kuimarisha km 128 za mpaka kati ya Kenya na Tanzania kutoka Ziwa Natron hadi Namanga pamoja na km 100 kutoka Kagunga hadi Manyovu katika mpaka kati ya Tanzania na Burundi.

(iii) **Kusogeza Huduma za Umilikishaji Ardhi kwa Jamii**: Katika mwaka 2020/21, Serikali imeanzisha ofisi 26 za Makamishna wa Ardhi wa Mikoa kwa lengo la kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi na kupunguza migogoro ya ardhi.

(iv) **Upangaji wa Matumizi ya Ardhi (Land Use Planning Project):** Kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 51 katika Wilaya sita (6) zinazopitiwa na Mkuza wa Mradi wa Bomba la Mfuta na kutoa mafunzo kwa timu za usimamizi wa matumizi ya ardhi za wilaya hizo; na Kukamilisha kazi ya tathimini ya matumizi ya ardhi na mazingira katika maeneo yaliyokuwa makambi ya wakimbizi (Ulyankuru, Katumba na Mishamo). Aidha, usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ada na tozo mbalimbali za ardhi umewezesha ukusanyaji wa jumla ya shilingi bilioni 120.4. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 5.5 zimetumika na shilingi bilioni 2.8 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 zimetolewa.

187. **Maendeleo ya Sekta Binafsi**

Serikali imeendelea kushughulikia changamoto ya ukosefu wa masoko ya bidhaa za wafanyabiashara wa Tanzania katika nchi jirani za EAC na SADC na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kufanya Vikao vya majadiliano na Sekta Binafsi ikiwemo kikao kati ya

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wawakilishi wa sekta binafsi kilichofanyika tarehe 31 Mei, 2021 Jijini Dar es Salaam. Vikao kingine ni Kikao cha Kamati Tendaji cha Baraza la Taifa la Biashara kati ya Katibu Mkuu Kiongozi na Wajumbe wa Sekta Binafsi kilichofanyika tarehe 17 Juni, 2021 Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya Mkutano wa 12 wa Baraza la Taifa la Biashara tarehe 26 Juni, 2021 Jijini Dar es Salaam ambalo wajumbe wake wanatoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Vilevile, Serikali ilifanya Kikao maalum cha 42 cha Kamati Tendaji ya Baraza la Taifa la Biashara tarehe 17 Juni, 2021 katika Ukumbi wa IKULU jijini Dar es Salaam. Kikao hiki kilihudhuriwa na Wajumbe kutoka Serikali, Sekta Binafsi, Taasisi za elimu ya juu, Kongano ya usafiri wa anga, Kongano ya kilimo na Kongano ya utalii pamoja na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kutoka Ofisi ya Rais – IKULU; Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji); Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Viwanda na Biashara; Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(ii) Kuvitafutia ufumbuzi vikwazo 30 kati ya vikwazo 64 vilivyokuwa vinawakabili wafanyabiashara wa Tanzania na Kenya. Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa biashara baina ya nchi hizi mbili na kuongeza soko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini;

(iii) Kuimarisha majadiliano na utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta binafsi kwa kufanya mikutano ya majadiliano katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Kigoma na Geita kwenye Wilaya za Mkuranga, Kigamboni, Sengerema, Magu, Ilemela, Kwimba, Misungwi, Ukerewe, Nyamagana, Tabora Mjini, Igunga, Kaliua, Nzega, Sikonge, Uyui na Urambo; na

(iv) Katika kukuza sekta binafsi ili iweze kushiriki na kuwa injini ya kukuza uchumi wa nchi, Serikali imefungua Akaunti za wafanyabiashara nchini zilizokuwa zimefungwa. Hatua hii imewezesha kuchochea uchumi na kurudisha imani kwa wafanyabiashara na wawekezaji kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi. Hatua hii pia imechochea wafanyabiashara kuanza kutumia akaunti zao na kuongeza wigo wa kodi. Serikali pia imekuza ushiriki wa wafanyabiashara ndogo kupunguza adhabu za waendesha bodaboda watakaopatikana na makosa kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 10,000 kwa kila kosa litakalobainika.

188. **Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Katika kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za uchumi na kuongeza

ushiriki wa watanzania kwenye utekelezaji utekelezaji wa miradi ya kimkakati, Serikali imechukua hatua zifuatazo: -

(i) Kuwajengea uwezo vijana ili waweze kujiajiri au kuajirika kwa kutekeleza Mpango wa Kuwajengea Uwezo Vijana (2JIAJIRI Youth Entrepreneurship Training Program) katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Morogoro, Zanzibar, Arusha, Kilimanjaro na Mwanza. Mpango unalenga kutoa mafunzo ya ujuzi, ujasiriamali na kuwaunganisha vijana na watu waliofanikiwa katika biashara. Mpango umewezesha mafunzo kwa vijana 303 wakiwemo wanawake 172 na wanaume 131. Mafunzo yalitolewa katika mikoa yote ambapo: Dar es Salaam (89), Morogoro (33), Zanzibar (44), Arusha (51), Kilimanjaro (40) na Mwanza (46). Mafunzo hayo ni kuhusu: sifa za mjasiriamali; mjasiriamali na familia; vyanzo vya mitaji; masoko; utunzaji kumbukumbu; kumjali mteja; urasimishaji biashara; kupanga bajeti; namna ya kutunza muda; umuhimu wa uwekaji akiba; na mtandao wa biashara;

(ii) Kukuza shughuli za kiuchumi za wajasiriamali wanawake kwa kuimarisha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi 927 yaliyopo katika ngazi za Mikoa (24), Halmashauri (123), Kata (280) na Vijiji (500) kwa kukufua Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (Presidential Trust Fund) ili utumike kulea wanawake wajasiriamali. Aidha, Serikali imeendelea kutenga maeneo wezeshi ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo wakiwemo wanawake ili kuwawezesha wanawake kufanya biashara zenye ubora na kiwango cha kitaifa na kimataifa;

(iii) Kuimarisha utendaji wa Mifuko na Programu za uwezeshaji kwa kufanya tathmini ya utendaji wa Mifuko na Program za uwezeshaji. Tathmini hii itawezesha Serikali kutatua changamoto zinazoikabili mifuko na programu za uwezeshaji kiwemo kuimarisha Mpango wa Uwezeshaji Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ili isitumike katika masuala ya kisiasa bali katika kuchochea uchumi wa wananchi. Serikali pia imefufua Mfuko wa Sanaa na Utamaduni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa lengo kukuza ajira kwa vijana. Hatua hii itakuza ajira kwa vijana katika sekta ya sanaa, utamaduni na michezo kutokana na mchango mkubwa wa sekta hii katika kukuza ajira kwa vijana. Katika mwaka 2020/21, mifuko na programu za uwezeshaji imetoa mikopo na ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 631 kwa wananchi 1,194,155 wakiwemo wanawake 716,493 sawa na asilimia 60 na wanaume 477,662 sawa na asilimia 40. Mifuko na program za uwezeshaji zimetegeneza jumla ya ajira 2,746,557 ambapo ajira za moja kwa moja ni 1,867,656 na ajira zisizo za moja kwa moja 878,898. Kati ya watu waliopata ajira kupitia mifuko na program za uwezeshaji, wanawake 1,345,813 sawa na asilimia 49 na wanaume 1,400,744 sawa na asilimia 51;

(iv) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

ya Mwaka 2004. Taarifa ya Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ilizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9 Februari, 2021 katika Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Jijini Arusha;

(v) Kuanzisha vituo vya Uwezeshaji 15 katika Mikoa ya Singida (1), Kigoma (6), Dodoma (7) na Geita (1) kama iliyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025 katika Ibara ya 26(k). Vituo vya Uwezeshaji vinatoa huduma mbalimbali kwa wananchi 10,893 wakiwemo wanawake 5,781 sawa na asilimia 13 na wanaume 5,112 sawa na asilimia 47. Aidha, Vituo hivi vimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 44,500,000,000 kwa wananchi 4,474 ambapo wanawake 1,903 na wanaume 2,571. Vilevile, vituo vimewezesha urasimishaji wa biashara 5,721 na kutoa mafunzo ya ujuzi na ujasiriamali kwa wananchi 6,339 wakiwemo wanawake 4,226 na wanaume 2,113; na

(vi) Kukuza ujuzi kwa vijana 18,956 wakiwemo wanaume 10,878 na wanawake 8,078 wa kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Kati yao, vijana 5,538 walipata mafunzo ya uanagenzi katika fani ya ufundi stadi na vijana 10,178 walipata mafunzo ya kurasimishiwa ujuzi kupitia mfumo usio rasmi ambapo kati ya wanufaika hao, 28 ni watu wenye ulemavu na vijana 3,240 waliwezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu kazini.

1.2.4 Changamoto zilizojitokeza Katika Utekelezaji wa Bajeti

189. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2020/21 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

(i) Kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kibiashara duniani hususan nchi washirika wa kibiashara zilizoathiriwa na UVIKO – 19. Athari hizo zimesababisha kutofikiwa kwa malengo ya mpango na bajeti;

(ii) Baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kukwepa kodi hususan kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa stakabadhi za kielektroniki wakati mauzo yanapofanyika hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi;

(iii) Baadhi ya Halmashauri kutosimamia kikamilifu matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ikiwemo mashine za kukusanyia mapato; na

(iv) Kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali watu hususan wahandisi wa kusimamia utekelezaji wa miradi pamoja na wataalam wa uendeshaji wa mitambo na vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za kijamii na kiuchumi.

1.2.5 Hatua Zinazochukuliwa Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti

190. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto zilizojitokeza. Miongoni mwa hatua hizo ni:

(i) Kuchukua hatua za kisera na kiutawala ili kuimarisha shughuli za kiuchumi na kibiashara zilizoathirika na kuhamasisha wananchi kupata chanjo na kufuata miongozo mbalimbali ya kujikinga na UVIKO-19;

(ii) Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani, masoko ya bidhaa nje na kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia bajeti yake;

(iii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki;

(iv) Kuanzisha mfumo mpya wa TAUSI ambao utaboresha mfumo wa mapato ya Halmashauri ili kukabiliana na mapungufu yanayosababisha uvujaji wa mapato; na

(v) Kuajiri wahandisi na wataalam watakaosimamia utekelezaji na uendeshaji wa miradi pamoja na kuboresha maslahi yao ili waendelee kubaki katika utumishi wa umma.